

**UWIANO NA UTOFAUTI WA KIISIMU KATI YA KISWAHILI CHA PAJE  
NA MAKUNDUCHI**

**SHOMARI SAID ABDALLAH**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA  
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI - ISIMU) YA  
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## **UTHIBITISHO**

Aliyetia sahihi hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma na kuiangalia tasnifu hii inayoitwa: '**Uwiano na Utofauti wa Kiisimu Kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi**', na napendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa minajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili (Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

**Dkt. ZELDA ELISIFA**

**(Msimamizi)**

**Tarehe .....**

**HAKIMILIKI**

Tasnifu hii hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa vyovyote vile, kama vile kuchukua sehemu ndogo ya kazi hii, kieletroniki, kurekodi, kurudufu au njia nyingine yoyote bila ya idhini na ridhaa ya mwandishi wa tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## **TAMKO**

Mimi, **Shomari Said Abdallah**, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

.....

**Shomari Said Abdallah**

**Tarehe.....**

**TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa familia yangu, mke wangu mpendwa Ashura Kombo, watoto wetu wapendwa, Mansour, Omar, Ummul-kulthum na wengine watakaofuata wote nawambia iwe ni hamasa kwao, na wajitahidi kutafuta elimu kwa bidii na juhudzi zote, kwani Elimu ni ufunguo wa maisha bora.

## SHUKRANI

Kwanza natanguliza shukurani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu, mmiliki wa viumbe vyote vilivyoko Mbinguni na Ardhini kwa kunijaalia uhai, uzima na uwezo wa kufanya utafiti na kuweza kuikamilisha kazi hii kwa kuandika matokeo ya utafiti, ni kweli bila ya msaada wa Allah jambo lolote haliwezi kusimama.

Vile vile niwashukuru wote walioniunga mkono kwenye kazi hii, kwa namna yoyote ile ambayo imeniwezesha kukamilisha utafiti huu. Si rahisi kuwaorodhesha wote waliota mchango wao katika kufanikisha kazi hii, bali nawashukuru wote nitakaowataja na nisiovataja kwa mchango wao wa kufanikisha utafiti huu, wafahamu nao wameshiriki kwenye kazi .

Shukrani zangu za mwanzo kabisa zimwendee msimamizi wa kazi hii Dr. Zelda Elisifa Sam, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, namshukuru kutokana na juhudini na ujasiri wake na ukomavu alionao kwangu kuanzia hatua ya uandishi wa pendekezo la utafiti mpaka pale kazi hii kukamilika kwake, naelewa wazi kuwa amenivumilia sana juu ya mapungufu yangu kama mwanafunzi, kwangu alikuwa muongozaji na mshauri mwelekezi, ni mwalimu mahiri na makini kwenye kazi anayoisimamia, alikubali kukaa nami kwa kunielekeza kwa sauti yenye hekima na upendo pale alipokuwa akinikosoa na kunielekeza, namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie upendo na busara ili wajao nao wavune busara zake.

Haitokuwa vyema nisipotoa shukurani zangu kwa uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya jamii, kwa mashirikiano mwanana waliyonipatia na kuniwezesha kufanikisha utafiti huu, Mungu awape maisha mema.

Shukurani zangu maalum ziwaendee wazee wangu wapendwa, Baba Said Abdallah Mfaume na mama yangu Asha Ameir Jafar, kwa mapenzi na haiba ya hali ya juu waliiyonelea kwa kunitunza na kuniengaenga, ambako kumeniwezesha kusoma hadi kiwango cha elimu ya chuo Kikuu.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila na shukurani pindi nikiacha kumshukuru mke wangu mpendwa Bi Ashura Kombo na watoto wangu wote wapenzi, kwa kuweka uaminifu na ustahamilivu mkubwa kwa muda wote niliokuwa katika harakati za kufanya utafiti huu, walikuwa katika hali nzito na ngumu katika mfumo mzima wa maisha yao.

Sitoweza kuwasahau walimu na wanafunzi ambao nilikuwa nao bega kwa bega kufanikisha kazi hii.

Nawashukuru niliowataja na nisiowataja wote nawambia ahsanteni sana Mungu awaoengezeni ari, kasi na moyo wa kuwasaidia wengine.

### **ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA ZILIZOTUMIKA**

KMK	Kimakunduchi
KPJ	Kipaje
KISW	Kiswahili
TAF	Tafsiri
Sil	Sifa ya usilabi
Na.	Nambari
Kons	Konsonanti
Kiy	Kiyeyusho
Ø	Kudondoka/ kupotea kwa kitamkwa
.....	Kuonesha utofauti katika msamiati
[ ]	Mabano ya fonimu
//	Mabano ya fonetiki
[ ]	Kujumuisha sifa bainifu za kitamkwa
{ }	Kuonesha sifa za ujumla za vitamkwa
/	Mazingira ya utokeaji wa mabadiliko ya kitamkwa
—	Mazingira ambayo kitamkwa kilichopokea michakato
kilipo kuwa	
+	Kuwa na sifa fulani
-	Kutokuwa na sifa hiyo
{ }	Mabano ya mofu

## **IKISIRI**

Utafiti huu uliangazia uwiano na utofauti wa kiisimu kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi. Na ulikuwa na malengo matatu; Kubainisha mfanano na utofauti baina ya fonimu za Kiswahili cha Paje na Makunduchi, pili Kulinganisha na kutofautisha kanuni za kifonolojia na mofolojia zinazotawala mofu ziundazo maneno ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi na Kubainisha uwiano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na Makunduchi.

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa mbinu za usaili, hojaji, ushuhudiaji na Maktabani zilitumika, hata hivyo utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; isimu linganishi na Mofofonolojia pamoja na sampuli ya watoa taarifa sitini (60) ilitumika thelathini kutoka Paje na thelathini kwa Makunduchi.

Kupitia matokeo ya utafiti, imegundulika kuwa Kifonolojia jamii hizi zinatofautiana kifonimi hasa kiidadi na kimatumizi kwa baadhi ya fonimu hizo. Pia, imebainika kuwa Kimakunduchi na Kipaje vinatofautiana katika baadhi ya kanuni za fonolojia na mofolojia kama vile katika udondoshaji na uyeyushaji katika baadhi ya nomino, vitenzi na vivumishi vimilikishi. Pia imebaainika kuwa Kimakunduchi na Kipaje vinatofautiana katika umiliki wa alomofu za nafsi ya kwanza na ya pili pamoja na viambishi vya ung'oekaji wa o-rejeshi, pamoja na hayo imebainika kuwa jamii hizi zinatofautiana kimaana katika baadhi ya maneno na hivyo imeonekana kuwa Wapaje wameathiriwa na Kiswahili sanifu katika utoaji na uwakilishi wa maana zao.

Mwisho mtafiti amependekeza mambo kadhaa kwa watafiti wajao, mambo hayo ni pamoja na tafiti nyingine linganishi zifanyike kwa baadhi ya vipengele vya fonolojia vipande kama vile silabi, fonolojia arudhi pamoja na kipengele cha sintaksia. Pili tumebaini kuwa Kimakunduchi kina vilahaja zaidi ya kimoja hivyo mtafiti anapendekeza eneo hili ni vizuri likafanyiwa uchunguzi wa kiutafiti zaidi.

## YALIYOMO

Uthibitisho.....	i
Hakimiliki .....	ii
Tamko. ....	iii
Tabaruku .....	iv
Shukrani .....	v
Orodha ya Vifupisho ya Alama Zilizotumika.....	vii
Ikisiri .. ....	viii
Yaliyomo.....	ix
Orodha ya Majedwali.....	xv
Orodha ya Chati .....	xviii

## SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1

1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Usuli wa Mada.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	4
1.4 Lengo na Madhumuni ya Utafiti .....	6
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti.....	6
1.4.2 Madhumuni Mahsus i ya Utafiti.....	6
1.5 Maswali ya Utafiti .....	7
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.6.1 Kitaaluma .....	7
1.6.2 Kinadharia .....	8
1.7 Upeo / Mawanda ya Utafiti .....	8

1.8	M pangilio/ M jengeko wa Utafiti .....	8
1.9	Muhtasari wa sura.....	8

## **SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA**

	<b>NADHARIA .....</b>	<b>9</b>
2.1	Utangulizi .....	9
2.2	Dhana ya Lahaja.....	9
2.2.1	Vigezo vya Uainishaji wa Lahaja.....	13
2.2.1.1	Kigezo Pungufu .....	13
2.2.1.2	Kigezo cha Mlingano .....	14
2.3	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Barani Ulaya.....	15
2.4	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Barani Asia.....	17
2.5	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Barani Amerika .....	22
2.6	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi Barani Afrika .....	22
2.6.1	Kazi Tangulizi Kuhusu ulinganishi wa Kilahaja Afrika ya Kaskazini.....	23
2.6.2	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Afrika ya Magharibi .....	24
2.6.3	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilugha Afrika ya Kusini.....	26
2.6.4	Kazi Tangulizi Kuhusu ulinganishi wa lahaja Afrika ya Mashariki .....	27
2.6.4.1	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Nchini Kenya.....	27
2.6.4.2	Kazi Tangulizi Kuhusu Lugha na Ulingenishi wa Kilahaja Nchini Tanzania .....	28
2.6.4.3	Kazi Tangulizi Kuhusu Ulingenishi wa Kilahaja Zanzibar .....	30
2.6.4.4	Kazi Tangulizi Kuhusu Kimakunduchi.....	32
2.7	Pengo la Maarifa.....	34

2.8	Kiunzi cha Nadharia .....	35
2.8.1	Nadharia ya Mofofonolojia .....	35
2.8.2	Nadharia ya Isimu Linganishi .....	37
2.9	Muhtasari wa sura .....	39
<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>		<b>40</b>
3.1	Utangulizi .....	40
3.2	Eneo la Utafiti.....	40
3.3	Usanifu wa Utafiti .....	40
3.4	Kundi lengwa.....	41
3.5	Sampuli na Usampulishaji.....	41
3.5.1	Sampuli Lengwa.....	43
3.5.2	Sampuli Tabakishi.....	43
3.6	Aina za Data .....	43
3.6.1	Data za Msingi.....	43
3.7	Ukusanyaji wa Data.....	44
3.8	Mbinu za Ukusanyaji wa Data .....	44
3.8.1	Mbinu ya Usaili .....	44
3.8.2	Mbinu ya Hojaji .....	45
3.8.3	Mbinu ya Ushuhudiaji .....	46
3.8.4	Mbinu ya Maktaba / Uchambuzi wa Kazi Maalumu .....	47
3.9	Mbinu za Kuchanganua Data .....	47
3.10	Muhtasari wa sura.....	48

<b>SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .....</b>	<b>49</b>
4.0 Utangulizi .....	49
4.1 Uwiano wa Fonimu za Konsonanti Kati ya Kimakunduchi na Kipaje .....	50
4.1.1 Uwiano wa Fonimu za Irabu Kati ya Kimakunduchi na Kipaje .....	53
4.1.2 Tofauti za Matumizi ya Sauti Bainna Kipaje na Kimakunduchi.....	56
4.1.3 Tofauti za Mpishano Huru wa Fonimu [l] na [r].....	56
4.1.4 Tofauti za Mpishano Huru wa Fonimu [v] na [p] .....	58
4.1.5 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti [ly] na [l] .....	60
4.1.6 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti [fw] na [f] .....	61
4.1.7 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti {vw /v} .....	63
4.1.8 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti {pj/t}.....	65
4.2 Uwiano wa Michakato na Kanuni za Kifonolojia na Mofolojia Bainna ya Kipaje na Kimakunduchi .....	66
4.2.1 Uwiano Katika Udondoshaji Irabu [i] .....	66
4.2.2 Uwiano Katika Udondoshaji Nazali {m / n} .....	68
4.2.3 Tofauti Katika Udondoshaji Nazali {m /n}.....	71
4.2.4 Utotofauti Katika Udondoshaji Kitambaza na Kimadende [l] na [r] .....	73
4.2.5 Uwiano Katika Udondoshaji Njeo Iliyopita Timilifu [me] .....	75
4.2.6 Utotofauti Katika Udondoshaji Njeo Iliyopita Timilifu [me] .....	76
4.2.7 Uwiano Katika Ukakaishaji wa Nazali ya Ufizi /n/ .....	77
4.2.8 Uwiano Katika Ukakaishaji wa Kiambishi cha Njeo Ijayo “ta” .....	79
4.2.9 Uwiano Katika Mvutano/Muungano wa Irabu Katika Vitenzi .....	80
4.2.10 Uwiano Katika Mchakato wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Nomino.....	82

4.2.11	Utofauti Katika Mchakato wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Vivumishi Vimilikishi .....	83
4.2.12	Utofauti wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Vitenzi Vinavyochukua Viambishi Nafsi.....	85
4.2.13	Uwiano Katika Ung'oekaji wa Viambishi Nafsi .....	86
4.2.14	Uwiano Wa Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Kwanza (ni) .....	87
4.2.15	Utofauti katika alomofu za ung'oekaji nafsi ya kwanza (ni) .....	88
4.2.16	Uwiano Katika Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Pili [u].....	90
4.2.17	Utofauti Katika Ung'oekaji Nafsi ya Pili {m} wingi.....	90
4.2.18	Uwiano Katika Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Tatu Umoja na Wingi (A-WA).....	91
4.2.19	Utofauti Katika Ung'oekaji wa Viambishi vya O-rejeshi vya Ngeli ya A-WA (Ye – O) .....	92
4.2.19.1	Utofauti Katika Ung'oekaji Viambishi O-rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li).....	92
4.2.19.2	Utofauti Katika Ung'oekaji Viambishi vya O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta).....	94
4.3	Uwiano wa Kimaana Bainya Msamiati wa Kiswahili cha Paje na Kile cha Makunduchi. ....	96
4.3.1	Msamiati wa Msingi Ulionanana Kimofolojia na Kimaana .....	96
4.3.2	Msamiati wa Msingi Uliotofautiana Kimofolojia kwa Sauti Moja Lakini Hufanana Kimaana .....	97
4.3.3	Msamiati wa Msingi Uliotofautiana Kimofolojia Moja kwa Moja Lakini Hufanana Kimaana.....	99

4.3.4 Msamiati wa Msingi Uliofanana Kimofolojia Lakini Umetofatiana Kimaana.....	100
4.4 Muhtasari wa sura.....	102
 <b>SURA YA TANO: UTANGULIZI, MUHTASARI WA MATOKEO,</b>	
<b>HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI .....103</b>	
5.1 Muhtasari wa jumla .....	103
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	103
5.3 Hitimisho .....	110
5.4 Mapendekezo kwa ajili ya tafiti zaidi.....	111
 <b>MAREJELEO .....</b>	<b>112</b>
 <b>VIAMBATANISHO .....</b>	<b>117</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 2.1	Orodha ya leksimu Kipate.....	12
Jedwali Na 2.2	Irabu zote 10 zinavyoweza kutamkika.....	20
Jedwali Na 2.3	Tofauti ya Kimatumizi kwa Sauti zenye Asili ya Kiarabu baina ya Kipemba na Kitumbatu.....	31
Jedwali Na.3.1	Watoa taarifa .....	42
Jedwali. Na 4.1	Sifa za Kimatamshi za Konsonanti na Nusu Irabu za Kima kunduchi.....	51
Jedwali Na. 4.2	Sifa za Kimatamshi za Konsonanti na Nusu Irabu za Kipaje .....	51
Jedwali Na 4.3	Matriki ya Irabu Ndefu za Kimakunduchi. ....	55
Jedwali Na 4.4	Utofauti wa Kimatumizi wa Fonimu {r/l} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	57
Jedwali Na 4.5	Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {v/p} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	58
Jedwali Na 4.6	Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {ly/l} kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	60
Jedwali Na 4.7	Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {fw/f} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	62
Jedwali Na 4.8	Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {vw/v} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	64
Jedwali Na 4.9	Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu pj/t Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	65
Jedwali Na. 4.10	Uwiano Katika Udondoshaji Irabu ya Juu Mbele [i] Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	66

Jedwali na 4.11	Uwiano Katika Udondoshaji Irabu ya Juu Mbele [i] Ikiwa Mwanzoni Kati ya Kipaje na Kimakunduchi.....	67
Jedwali na 4.12	Uwiano Katika Udondoshaji Nazali {m/n} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	69
Jedwali na 4.13	Utofauti wa Udondoshaji Nazali {m/n} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	71
Jedwali na 4.14	Utofauti wa Udondoshaji Kitambaza na Kimadende {r/l} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi.....	73
Jedwali na 4.15	Uwiano Katika Udondoshaji Kiambishi Njeo Iliyopita Timilifu [me] kati ya Kipaje na Kimakunduchi.....	75
Jedwali na 4.17	Data za Mchakato wa Ukaakaishaji wa Nazali /n/ .....	78
Jedwali na 4.18	Uwiano Katika Ukakaishaji Njeo Ijayo “ta”.....	79
Jedwali na 4. 19	Mivutano ya Irabu Katika Kimakunduchi na Kipaje.....	81
Jedwali na 4.20	Utofauti wa Uyeyushaji wa Vivumishi Vimilikishi.....	84
Jedwali na 4.21	Utofauti Katika Uyeyushaji Katika Mnyambuliko wa Vitenzi....	85
Jedwali Na 4.22	linaonesha ug'oejadi wa viambishi nafsi kati ya Kipaje na Kimakunduchi .....	87
Jedwali na 4.23	Uwiano Katika Ung'oejadi Alomofu za Nafsi ya Kwanza (ni)....	88
Jedwali na 4.24	Utofauti wa Ung'oejadi wa Alomofu za Nafsi ya Kwanza (ni) ...	89
Jedwali na 4.25	Utofauti wa Alomofu “cha”/ “sa” Katika Kukiwakilisha Kiambishi Nafsi ya Kwanza (ni).....	89
Jedwali na. 4.26	Uwiano wa Alomofu Zinazoonesha Ung'oejadi Kiambishi Nafsi ya Pili [u] .....	90
Jedwali na 4.27	Utofauti wa Alomofu Zinazowakilisha Nafsi ya Pili wingi (m)..	91

Jedwali na 4.28	Uwiano wa Alomofu Zinazowakilisha Viambishi Nafsi ya Tomu Umoja na Wingi (A-WA) .....	92
Jedwali na 4.29	Ung'oekaji wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li) Kimakunduchi.....	93
Jedwali na 4.30	Ung'oekaji wa O-Rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li) Kipaje.....	93
Jedwali na 4.31	Ung'oekaji Wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta) Katika Kimakunduchi. ....	95
Jedwali na 4.32	Ung'oekaji wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta) Katika Kipaje. ....	95
Jedwali na 4.33	Msamiati Ulionanana Kimofolojia na Kimaana Bainya Kipaje na Kimakunduchi. ....	96
Jedwali na 4.34	Msamiati Uliotofautiana Kimofolojia Lakini Unafanana Kimaana .....	98
Jedwali na 4.35	Msamiati Uliotofautiana Kimofolojia Moja kwa Moja na Kufanana Kimaana.....	99
Jedwali na 4.36	Masamiati Ulionanana Kimofolojia Lakini Maana Tofauti .....	101

## **ORODHA YA CHATI**

Chati Na. 4.1	Mfumo wa Irabu fupi katika Kipaje na Kimakunduchi .....	54
Chati Na. 4.2	Mfumo wa Irabu Ndefu za Kimakunduchi:-.....	54

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### **1.1 Utangulizi**

Sura hii imewasilisha vipengele mbalimbali vyatia kuitangulizi ambavyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti usuli wa mada, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, na mpangilio wa utafiti.

#### **1.2 Usuli wa Mada**

Wataalamu mbalimbali wamejadili dhana ya Isimu Linganifu pamoja na uwiano wa Kisarufi baina ya lugha moja na nyingine au lahaja moja na nyingine. Miongoni mwao ni Matinde (2012) anayeeleza kuwa isimu linganifu hufanya kazi ya kulinganisha na kulinganua vipashio mbalimbali vyatia lugha mbalimbali, ili kudhihirisha kufanana au kutofautiana baina ya lugha hizo. Matinde (keshatajwa) anadai kuwa taaluma hii huangalia kufanana na kutofautiana kwa lugha mbalimbali kuhusu hali ya uundaji wa maneno yao katika kurejelea hali mbalimbali huku akidokeza kuwa lugha ya Kilatini na Kingereza hubadilisha umbo la neno na kudhihirisha hali mbalimbali, kwa mfano kitenzi “*go*” hubadilika na kuwa “*went*” na “*gone*” kurejelea wakati uliopita, hali ambayo haijitokezi katika lugha ya Kichina. Naye Jones (1986) anaungama na dai hilo na kudai kuwa lugha za Kisankriti, Kigiriki na Kilatini zinahusiana na kwamba zimetokana na lugha mame moja. Hata hivyo, akionesha mfano katika neno “*bhratar*” la Kisankriti lenye maana ya ndugu wa kiume, ambalo hufanana na neno “*frater*” la Kilatini na neno “*phrater*” katika lugha ya Kigiriki. Halikadhalika Trudgill (1974) anadai kuwa lugha inapogawanyika na mabadiliko ya lugha hutokea, mabadiliko hayo husambaa kutoka katika mji

mkubwa zaidi kuelekea katika mji unaofuatia kwa ukubwa na kisha kuelekea katika miji mingine midogomidogo na vijiji, kwa kufuata utaratibu unaotabirika kiasi ya kwamba athari ya mji mmoja kwa mji mwengine huwa na uwiano nyooofu na ukubwa wa miji hiyo huwa na uwiano pindu na umbali baina yao. Akifafanua zaidi kuhusu mabadiliko ya lugha anadai kuwa yanachochewa na ueneaji wa nduni za lugha. Sloat (1978) akinukuliwa na Massamba (2012) anaelezea kuhusu ruwaza za sauti katika lugha hutofautiana katika namna tatu; lugha huchagua sauti chache tu kutoka katika bohari la sauti, hivyo sauti zitumikazo katika lugha zote haziwezi kuwa sawa, lugha inakuwa na namna tofauti ya utokeaji wa sauti zake, na michakato inayoleta mabadiliko katika lugha moja si lazima iliete mabadiliko katika lugha nyininge.

Baadhi ya wataalamu walioshughulikia tafiti za mahusiano ya Kisarufi katika Kiswahili pamoja na lahaja zake (Mazrui, 1983; Kipacha, 2003; Bakar, 2015; Khamis, 1984; Juma, 1996; Bavuai, 2017; Juma, 2011). Mazrui (1983) alifanya uchunguzi juu ya tofauti ya vipashio vya njeo za nyakati kati ya lahaja za Kimvita, Kibajuni, Kiamu na Kiunguja. Kipacha (2003) ametafiti lahaja ya Kimakunduchi kwa kuonesha sifa bainifu za kifonolojia. Kipacha (keshatajwa) akifafanua kuhusu lahaja hiyo kuwa haifanani na Kiunguja, Kimtang'ata, Kitumbatu na Kipemba. Sifa bainifu alizozifafanua ni za kimofolojia katika kuonesha leksimu mahususi za Kimakunduchi. Bakar (2015) alitafiti kwa kulinganisha kati ya lahaja ya Kitumbatu na Kipemba. Khamis (1984) alifanya utafiti linganishi kati ya Kipemba cha mjini na kile cha vijijini. Wataalamu wengine waliotafiti kuhusu ulinganishi wa lahaja Juma (1996) ambaye aligundua kuwa kuna lahaja ndogondogo za Kimakundichi pia kuna mfanano wa kimsamiati na maumbo kati ya Kimakunduchi na Kijambiani. Bavuai

(2017) amechunguza muundo wa Kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Juma (2011) alilinganisha msamiati wa Kimakunduchi, Kibwejuu, Kimtende, na Kikizimkazi.

Tafiti mbalimbali zilizopita zimejaribu kulinganisha juu ya mahusiano ya lugha na lahaja mbalimbali kama vile Kitumbatu na Kipemba (Bakari, 2015), Kimakunduchi na vilahaja vyake (Juma, 2011) na Kipemba cha mjini na kile cha vijiji (Khamis, 1984). Mahusiano hayo zaidi yamejitokeza katika fonolojia, mofolojia na msamiati. Hata hivyo Kimakunduchi na vilahaja vyake kama vile Kipaje bado havijaangaliwa kiundani kuilinganishi katika vipengele vyta fonolojia, mofolojia na msamiati na maana zake hivyo kuna haja kubwa ya kufanya utafiti katika maeneo hayo ili kubaini uwiano na utofauti wa kiisimu uliopo baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

Sambamba na hili, baadhi ya watafiti kama (Juma, 2011) anadai kuwa lahaja ya Kimakunduchi na vilahaja vyake kikiwemo Kimtende vinafanana katika ngazi ya msamiati na mjengeko wao, mtafiti huyo ameshindwa kutambua uwiano na utofauti uliopo baina ya Kimakunduchi na vilahaja vyake hivyo, Utafiti huu umechunguza kwa kina mapungufu yaliyojitokeza katika kazi za awali, hivyo mtafiti ametafiti kwa kina katika vipengele vyta uwiano na utofauti wa kifonimu, kanuni za kifonolojia na kimofolojia zinazotawala mofu ziundazo maneno na msamiati na maana zake katika Kiswahili cha Makunduchi na Paje kama ilivyojitokeza katika sura ya nne ya utafiti huu.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Uwiano wa kiisimu kati ya lugha ni suala la kawaida ulimwenguni kote kuonekana jamii ya lugha moja au lahaja moja ikitofautiana au ikifanana kimawasiliano na nyengine kulingana na umbali ama ukaribu uliopo wa kijiografia baina ya kitongoji kimoja na kingine. Pia mara nyingi mfanano huo au tofauti hizo huweza kujidhihirisha katika vipengele vyote vyta kiisimu kama vile matamshi, maumbo ya maneno, msamiati, miundo ya tungo ama sentesi pamoja na maana. Hivyo wazungumzaji wa lugha moja wanaweza kutofautiana kiusemajji kulingana na maeneo wanayosambaa. Tofauti hizo husababishwa na tofauti ndogo ndogo za kijiografia.

Kazi pamoja na tafiti mbalimbali ulimwenguni kote ikiwemo Ulaya, Asia, Amerika, Afrika, Tanzania Bara na hata Visiwani Zanzibar zimefanyika ili kuangalia mahusiano ya kilugha kati ya jamii moja ya lugha na nyingine. Sambamba na hayo, wataalamu mbalimbali walijaribu kuzungumzia muingiliano wa kiisimu. Miongoni mwa hao ni pamoja na Cook (1969, 1999) na Ervin-Trip (1974) waliosema kuwa lugha huwa na sifa za kuathiriana muathiriano huo husababisha lugha ya kwanza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, na kwamba mtu hawezi kujifunza lugha ya pili bila ya kuathiriwa na lugha yake ya kwanza katika vipengele vyta msingi vyta kiisimu. Hata hivyo, kadiri ya Massamba (2004) lahaja ni lugha moja wapo baina ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama lafudhi au msamiati usio wa msingi. Kwa minajili ya fasili hii zipo tofauti nyingi na za waziwazi katika maeneo ambayo lugha ya Kiswahili

inazungumzwa na maranyingi tofauti hizo hujitokeza katika mazingira ya kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati, kimuundo na hata kimaana.

Kwa kuendelea zaidi Massamba (1999) na Deen (2002) wanasema pia kuwa lugha za Kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Nao Swan na Smith (1987) wao walieleza kuwa makosa katika lugha husababishwa na muingiliano kati ya lugha mbili huweza kusababisha ugumu ama utata au uvulivuli na kutatiza matumizi ya lugha. Hata hivyo tafiti mbalimbali lingenishi zimefanyika ili kuonesha muingiliano na muachano wa kilugha pamoja na lahaja zake. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na Bakari (2015) alifanya ulinganishi wa kiisimu kati ya Kipemba na Kitumbatu, katika ulinganishaji wake huo alibaini kuwa Kipemba kinajipambanua na Kitumbatu katika vingele vya fonolojia kama umiliki na matumizi ya kifonimu, ung'oekaji wa viambishi nafsi, michakato ya kimofoloa katika kuyakokotoa maumbo ya maneno kutoka umbo la ndani kwenda nje, pamoja na hayo alibaini kuwa kuna muachano mkubwa wa kimofolojia pamoja na maana katika msamiati wa msingi utumikao katika lahaja hizo. Naye Juma (2011) alilinganisha Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kikizimkazi, katika tafiti yake hii alilinganisha mofolojia ya msamiati unaotumiwa na wazungumzaji wa maeneo hayo na alibaini kuwa msamiati wa Kimakunduchi unawiana sana na ule utumikao katika vitongoji vya Mtende na Bwejuu na kutofautiana na msamiati wa Kizimkazi kutohana na kuwa Kikizimkazi kimeathiriwa na Kiunguja mjini. Ijapokuwa tafiti hizo zimejaribu kuonesha muingiliano na mlingano wa kiisimu baina ya lahaja na vilahaja vya Kiswahili, lakini bado kuna mwanya mkubwa wa kiutafiti katika maeneo ya fonolojia na vipengele vyake, mofolojia na vipengele vyake pamoja na kipengele cha maana katika

msamiati wa msingi, ambavyo vinahitaji kushughulikiwa ili kubaini mahusiano na utofauti uliopo baina ya lugha kuu na lahaja, lahaja moja na nyingine na hata lahaja na vilahaja vyake, kama ilivyo kwa mtafiti katika Kimakunduchi na Kipaje, ambapo mtafiti alishughulikia uwiano na utofauti katika vipengele vyatofauti na mtafiti za kifonolojia na kimofolojia zinazotawala mofu ziundazo maneno ya jamii lugha hizi pamoja na maana katika msamiati wa msingi, vipengele ambavyo vilikuwa bado havijapata fursa ya kushughulikiwa na watafiti waliotangulia katika kukilinganisha na kukilinganua Kimakunduchi na vilahaja vyake kama vile Kipaje, kama ilivyojitekeza katika sura ya nne ya utafiti huu.

## **1.4 Lengo na Madhumuni ya Utafiti**

### **1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini uwiano na utofauti wa kiisimu uliopo baina ya Kiswahili kinachozungumzwa Paje na kile cha Makunduchi.

### **1.4.2 Madhumuni Mahsusini ya Utafiti**

Utafiti huu una madhumuni mahsusini matatu:

- i) Kubainisha mfanano na utofauti baina ya fonimu za Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.
- ii) Kulinganisha na kutofautisha kanuni za kifonolojia na mofofonolojia zinazotawala maumbo ya mofu zinazojenga maneno ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.
- iii) Kubainisha uwiano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

## **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti wa kazi hii uliongozwa na maswali yaliyolenga malengo mahususi hapo juu kama hivi ifuatavyo:-

- i) Ni zipi tofauti na mfanano wa Kifonimu baina Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi?
- ii) Kuna tofauti na ufanano gani kati ya kanuni za kifonolojia na kimofolojia zinazotumika na kutawala maumbo ya mofu ziundazo maneno ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi?
- iii) Je kuna tofauti zipi na mfanano upi wa kimaana baina ya msamiat wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi?

## **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Matarajio yetu ya dhati kabisa ni kwamba kukamilika kwa matokeo ya tafiti hii yatakuwa na mchango mkubwa sana katika mtaala pamoja na taaluma ya isimu kupitia nyanja tofautitofauti kama vile kitaaluma, kijamii ama kiutamaduni na hata kinadharia kama vile.

### **1.6.1 Kitaaluma**

Utafiti huu utakuwa kama chachu na muongozo kwa watafiti wengine wenye nia na dira ya kuandika pamoja na kuibua matatizo ya tafiti mpya zitakazohusiana na mada za kiulinganishi wa kiisimu kwa wasomi wa isimu, hata hivyo tafiti hii itawasaidia wanaisimu mbalimbali katika kufanya marejeo ya kazi zao tarajiwa zitakazohusiana na ulinganishi wa kiisimu Visiwani Zanzibar na hata nje ya visiwa hivyo. Sambamba na hayo, utafiti huu utasaidia uwelewa kuhusu mfanano na utofauti wa kifonimu,

kanuni na michakato ya kifonolojia na kimofolojia pamoja na wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

### **1.6.2 Kinadharia**

Utekelezwaji pamoja na ufanyakaji kikamilifu wa tafiti hii inasaidia watu mbalimbali kuzitambua nadharia mbalimbali za kiisimu na matumizi ya kila nadharia pamoja na kuweza kuzitumia nadharia hizo katika kazi zao mbalimbali kama mtafiti wa tafiti hii alivyozi bainisha na kuzitumia katika kukamilisha tafiti yake hii.

### **1.7 Upeo / Mawanda ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza uwiano na utofauti wa kiisimu uliopo baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Kimakunduchi katika vipengele vya fonimu, kanuni za kifonolojia na kimofolojia na msamiati wa msingi na maana zake. Hata hivyo, utafiti huu haukuangalia kipengele cha kisintaksia kati ya Kipaje na Kimakunduchi.

### **1.8 Mpangilio/ Mjengeko wa Utafiti**

Utafiti huu unajumuisha sura ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne na ya tano. Hivyo, kila sura inajumuisha vipengele muhimu vya sura nzima.

### **1.9 Muhtasari wa sura**

Sura hii imejadili kwa kina vipengele muhimu vinavyohusiana na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, na mpangilio wa utafiti. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imeangalia mapitio ya kazi tangulizi za wataalamu mbalimbali pamoja na kiunzi cha nadharia kilichotumika katika uchambuzi wa data na mwisho hitimisho.

#### **2.2 Dhana ya Lahaja**

Wataalamu kadhaa wamezungumzia kuhusu dhana ya lahaja, kwa njia tofauti tofauti. Miongoni mwao Onyango (2017) alieleza kuwa lahaja ni tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno zitokanazo na tofauti katika maeneo mbali mbali kwa lugha zenyе asili moja. Hata hivyo, katika utafiti wake huu amefafanua kuwa lahaja ikipata nafasi ya kusanifiwa inakuwa na uwezo wa kuwa lugha kuu na tofauti ndogondogo katika lugha hutegemea maeneo mbalimbali na hutokea kutokana na kutawanyika kwa watu wanaotumia lugha moja, kuingiliana na kuoana kwa watu, dini, elimu pamoja na muachano wa kijiografia. Sambamba na hayo Onyango (ameshatajwa) akielezea zaidi kuwa Kiswahili kina lahaja nyingi na mgawanyiko wake, pia ameweza kuonesha jinsi lahaja hizo zinavyotofautiana katika matumizi ya sauti kati yao na Kiswahili sanifu kama alivyo jaribu kuonesha katika mifano hapa chini.

**KIPATE**  
Baratha  
Uthia

**KISWAHILI**  
Baraza  
Udhia.

Onyango (ameshatajwa) amebainisha kuwa katika lahaja Kipate hutumiwa sauti [th] pale ambapo Kiswahili sanifu hutumia sauti [z], [dh] au [v]. Halikadhalika,

ameonesha kuwa lahaja ya Kiamu inasifa ya kutumia sauti [t] badala ya [č] itumikayo katika Kiswahili sanifu, sambamba na hayo anasema kuwa Kiamu kinasifa ya kudondosha sauti [g] na [l] zinapotokea baina ya irabu kama mifano alivyoiyonesha hapa.

<b>KIAMU</b>	<b>KISWAHILI</b>
Mbeu	Mbegu
Nduu	Ndugu
Mbee	Mbele

Halikadhalika, katika lahaja ya Kivumba anadai kuwa haina sauti [t] inayotumika katika Kiswahili na badala yake hutumia sauti [r] sehemu ya [t]. Aidha, katika lahaja ya Kimrima hutumia sauti [l] pale ambapo Kiswahili kinatumia sauti [r]. Vile vile Onyango (ameshatajwa) katika uainishaji wa lahaja anaelezea kuwa Kihadimu / Kimakunduchi na Kitumbatu ni lahaja moja. Tofauti hizo huweza kujitokeza kati ya lahaja na lahaja, hata kwa jamii yenyе kutumia lahaja moja kama jamii ya wahadimu/ wamakunduchi hutofautiana kifonolojia na hata kimofolojia jambo linalo lazimu kufanyika kwa tafiti mbalimbali za Kilahaja kutokana na muachano wa kijiografia uliopo kama ilivyo kwa Paje na Makunduchi.

Hata hivyo hoja yake kuwa lahaja ya Kihadimu / Kimakunduchi na Kitumbatu kuwa ni lahaja moja kitu ambacho kinahitaji kuhakikiwa na utafiti mwengine kwani Kitumbatu kinapatikana kaskazini mwa kisiwa cha Unguja katika maeneo ya Tumbatu na maeneo jirani lakini Kihadimu/ Kimakunduchi kinapatikana Kusini mwa kisiwa hicho. Onyango (ameshatajwa) katika tafiti yake hiyo tofauti za kimofolojia, kimaana na kimsamiati hazikuhusishwa na kushughulikiwa. Hivyo basi, utafiti huu

wa Onyango ulimsaidia mtafiti kitaaluma katika kushughulikia vipengele vyakifonolojoa, kimofolojia, msamiati na maana zake kati ya Kipaje na Kimakunduchi.

TUKI (1990: 21) inaonesha kuwa lahaja ni kitarafa cha lugha kinachobainika ama Kijamii / Kijiografia na kudhihirishwa na vipengele maalumu vyakisauti na kimuundo. Hivyo basi dhana hii ilimuwezesha mtafiti kupata taaluma katika kudhihirisha utofauti na ufanano uliopo baina ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi. Hichens (1939), Stigand (1915), Chiraghdin (1974) na Ohly (1982), wanakubaliana kwa kueleza kuwa Kingozi / Kingovi kuwa ni lahaja-mama ambayo sasa imekufa. Hata hivyo Knappert (1979) na Sacleux (1939) wao wanaichukulia Kingovi kama rejista ya mashairi tu na si lahaja-mama. Kwa muelekeo wa mawazo hayo sisi hatukubaliani nao kuwa Kingovi ni lahaja mama na wala si rejista ya mashairi kama wanavyodai wataalamu hao bali Kingovi ni lahaja ya kawaida kama zilivyo lahaja nyingine kama Kihadimu na Kitumbatu na wala si rejista kutokana Kingovi kinachukua eneo kubwa la kimatumizi ukilinganisha na eneo la rejista hata hivyo rejista ni mtindo wa uzungumzaji kutokana na shughuli maalumu na eneo maalumu kwa mantiki hiyo Kingovi kitabaki kuwa lahaja ya kawaida mionganoni mwa lahaja za Kiswahili na si lahaja mama kwasababu kinauwiano mkubwa wa kiisimu kati yake na lahaja nyingine za Kiswahili na hutumika zaidi eneo la Tana-Lamu.

Bakari (1985) anapingana na hoja za Stigand (ameshatajwa) kuhusiana na kuwepo kwa lahaja ya Kipate. Bakari (ameshatajwa) aliangalia upande wa vipengele vyafonolojia na mofolojia pekee na akakuta kuwa tofauti ni ndogo sana, hivyo akaona kuwa Kipate si lahaja kamili. Hata hivyo, hakuonesha katika kazi yake ushahidi wa kuwa Kipate si lahaja kamilifu na ukiangaliwa uhalisia ni kwamba Kipate kina kila

sifa ambazo lahaja nyingine zinazo, sifa hizo ni pamoja na kuwa na watumiaji wake, sauti zake na hata kuwa na michakato yake ya utamkaji na uundaji wa maneno yake kama zifanyavyo lugha na lahaja nyingine ulimwenguni kote. Sambamba na hilo Prins (1967) anathibitisha uwepo wa jamii ya wapate kwa kudai kuwa historia inaonyesha kuwa wanajamii wa Kipate waliwahi kuishi sehemu za mto Ozi na Mpekatoni karibu na bonde la mto Tana. Naye Kipacha (2003) analithibitisha hili kwa kusema kuwa Kipate ni Lahaja inayozungumzwa katika kisiwa maarufu cha Pate kilichopo kaskazini mashariki ya Pwani ya Kenya na kiko kaskazini mashariki ya Lamu. Kipate kimeshabihiana kwa karibu sana na Ki-amu na Ki-siu ingawaje zipo tofauti fulani fulani za kimatamshi na kileksika. Kwa kulithibitisha hilo Kipacha (ameshatajwa) ametoa orodha ya leksimu za Kipate kama:-

#### **Jedwali 2.1: Orodha ya leksimu Kipate**

<b>Pa</b>	<b>KS</b>	<b>Tofauti</b>
čwačwa	chura	čw: čø
maao	malalo/mala	l:ø zi
vumi	yumbi	m:mb
meko	jiko	ma-:ji-
ŋkanda	mkondo	ŋ/m; a:o

Vilevile Kipacha (ameshatajwa) ameonesha sifa za kifonolojia na kimofolojia ili kudhihirisha uwepo wa lahaja ya Kipate kama:-

*Sifa Bainifu za Kifonolojia:*

(a) Orodha ya fonimu:

- Hazitofautiani na Kitikuu isipokuwa hakuna utokeaji wa fonimu /n/
- b. Uidentali: t, nd na kibinua ulimi /ndr/
  - c. Udondoshaji wa konsonati /j/ mfano: mai (maji)
  - d. Utokeaji wa fonimu zenyet athari ya Kiarabu /θ/ na /ð/
  - e. Vipasuo mpumuo ph, th, čh
  - f. Kuna utokeaji wa nazali-mora /ɳ/ inayotokana na mchakato wa \*mu-> m >ɳ.

Kinachotokea hapa ni kuwa kuna udondoshaji wa irabu ya juu /u/, halafu umoraishaji (wanamapokeo huita usilabishaji) [m] ambayo baadaye huendana na mahali pa utamkaji wa konsonanti inayofuatia na kuwa [ɳ]

### **2.2.1 Vigezo vya Uainishaji wa Lahaja**

Dhana ya Lahaja imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali kupitia vigezo na mitazamo tofauti miongoni mwa wataalamu ambao wamejaribu kuonesha vigezo vya uainishaji wa lahaja ni pamoja na Abasheikh (1978), Allen na Linn (1986), Faguson (1960) kama walivyo nukuliwa na Kipacha (2003) wanasema kuwa kuna vigezo vikuu viwili vya uainishaji wa lahaja ambavyo ni kigezo pungufu na kile cha uelewano.

#### **2.2.1.1 Kigezo Pungufu**

Kwa mujibu wa Allen na Linn (1986), pamoja na Faguson (1960) wanaamini kwamba lahaja ni kijilugha ambacho hakijaandikwa na hakina maandishi ya kujitegemea, kilugha ambacho hakina maandishi, kwa mantiki hiyo ni kwamba mtazamo huu huichukulia lahaja kama lugha pungufu ambayo haijajikamilisha katika

nyanja za kiuwandishi kwa maana hiyo lahaja hufuata kanuni na sharia za lugha kuu katika kupokea maandishi yake ili kufikisha ujumbe kwa watu wanaoitumia hivi ndivyo ilivyo kwa Kimakunduchi na Kitumbatu kwa Kiswahili sanifu. Hivyo tunaweza kusema kuwa huu ni mtazamo wa kimapokeo ambao umelenga kuidunisha lahaja na badala yake kuikweza lugha kuu. Hata hivyo, Kipacha (2003) anapingana na mawazo ya Allen na Linn pamoja na Faguson (wameshatajwa) kwa kudai kwamba kigezo cha kimaandishi si cha msingi kwa kuwa kuna baadhi ya ‘vilugha’ visivyo rasmi kama Kimvita, Kipokomo, na Kiamu viro katika maandishi. Hata nasi tunakubaliana na madai ya Kipacha (ameshatajwa) kuwa maandishi si kigezo cha kuzigawa na kuzibaini lahaja kwani hata lugha kuu hutumia sauti za nasibu katika maandishi yake, sauti ambazo hazina uhusiano hata kidogo na kile kinacho wakilishwa na sauti hizo, sauti hizohizo ndizo zinazotumiwa na lahaja katika kukidhi mawasiliano kwa jamii lugha husika na huwenda sauti za lahaja zikatofautiana na zile za lugha kuu kwa hiyo lahaja ni bora kuziainisha kwa kutumia kigezo cha muachano wa kijiografia pamoja na tofauti za matamshi kwa wazungumzaji. Kwa mantiki hiyo mtazamo huu unaitukuza na kuikweza lahaja iliyoteuliwa kwa ajili ya shughuli rasmi iwe ni ‘lugha’ kama Kiunguja mjini (1930) na zile zisizoteuliwa zitumike tu katika vitongoji mbalimbali ziwe ndio lahaja.

### **2.2.1.2 Kigezo cha Mlingano**

Allen na Linn (1986) na Faguson (1960) Mtazamo huu unafasiri kuwa lahaja ni lugha yoyote ile iwe imeandikwa au haikuandikwa. Mtazamo huu umeshindwa kutofautisha kati ya lahaja na lugha kuu, kwa sababu zote zinasifa ya kuandikwa kwahiyo haujatubainishia tofauti za msingi zipatikanazo baina ya lahaja na lugha

kuu. Licha ya kupingana nao kwa kipengele hicho lakini kwa kiasi fulani tunaungana nao kwani wakati mwengine lugha au lahaja huweza kubainika kwa kutumia sauti tu bila ya kuwepo kwa maandishi na msikilizaji kumtambua msemaji wake ni muathirika wa jamii lugha gani bila ya kuangalia maandishi ya lugha anayoitumia katika mawasiliano yake.

### **2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Barani Ulaya**

Watafiti wengi ulimwenguni wametafiti lahaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana ama kutofautiana kati yao kiisimu. Mionganoni mwa wataalamu hao waliojaribu kuogelea katika uwanja huo ni pamoja na Martijn (2007) mtalamu huyu alifanya utafiti linganishi katika lahaja za Uholanzi (Netherland) katika utafiti wake huo anasema kuwa Uholanzi na Kaskazini mwa Ubelgiji “Kidachi” ndio lugha rasmi, pia amebaini kuwa lahaja zenyenye ukaribu wa kimaeneo zinafanana, na zenyenye umbali wa kijiografia hutofautiana katika kulithibitisha hili ametoa mfano wa neno kutoka Kingereza ambalo ni “*Stones*”(jiwe) neno hili linatamkwa katika hali tofauti kuanzia lugha kuu hadi lahaja za lugha husika kwani anasema katika lugha kuu hutamkwa [stenə] wakati maeneo ya Kaskazini mwa Netherland (Groningen) neno hili hutamkwa [stain], hata hivyo Kusini mwa Netherland (Limburg) hutamkwa [stEin], vile vile ametoa mfano mwengine ili kudhihirisha hilo ametumia neno “*to drink*” ambalo Kaskazini mwa Holand hutamkwa kama [driŋ? η] wakati Kusini mwa Netherland hutamkwa [driŋke] sawa na lahaja sanifu. Vile vile Martijn (ameshatajwa) anaelezea kuwa Netherland ina jumla ya lahaja 28, lahaja hizo ni pamoja na lahaja za Zuid Holland, Kennemerland, Water land, Zaan, Brambant. Hatahivyo amebaini kuwa lahaja hizo zinatofautiana na kufanana kifonolojia na

kimofolojia kwa kiasifulani katika kulidhihirisha hilo anadai kuwa neno “milk” la Kingereza kwa lahaja ya Veenwouden linatamkwa [mæəlkə] lakini hutamkwa[melək] katika lahaja ya Delft (Zuid Holland) badiliko moja la kimatamshi kutamkwa vyengine unafanywa kama:-

Mælkə .....subst. Θ/ε  
 Melək.....delete. ε

Kortman (2003) alilinganisha maumbo ya maneno na miundo ya sentesi katika lahaja za Kingereza. Katika tafiti yake hii aligundua kuwa magharibi ya Uingereza kuna Makala za kiasi za Kisarufi ambazo ni tofauti na Makala za visiwa vya Ungereza. Hata hivyo, Kortman (ameshatajwa) katika kulidhihirisha hili alitoa mfano ambapo alisema “mfumo wa kisemantiki, majina yanaangaliwa jinsia katika makundi na majina yanayohesabika ambapo tofauti zipo baina ya vitu vyenye uhai na visivyo uhai na kwa binaadamu na asiyekuwa binaadamu ambapo viambishi “she” na “he” wakati kiambishi “she” hutumika kuashiria binaadamu wa kike na “he” hutumika kuashiria binaadamu wa kiume au kwa vyote na hapo ndipo inapoonekana tofauti. Sambamba na hayo alieleza kuwa hali hii si Uingereza tu bali hata Scotland, Ireland ya Kaskazini na Jamuhuri ya Ireland ambako kitenzi cha wakati uliopo huwakilishwa na “s” mwishoni mwa neno au kitenzi husika hata hivyo “s” hutumika kuwakilisha mtu wa tatu umoja itokeapo mwishoni mwa neno hali ambayo katika Kingereza sanifu hujitokeza katika maneno mengine. Tunakubaliana nae kwa kiasi fulani kwani lugha moja na nyingine hutofautiana katika upachikaji na uamilifu wa vimofimu katika muundo wa neno hali ambayo hujitokeza katika lugha ambishi zote duniani kama vile kiarabu kwa mfano /ك/ /ت/ /ه/ /هـ/ hutumika kuwakilisha sifa ya uke, hata hivyo kiambishi /و/ /ؤ/ /هـ/ hutumika kuwakilisha sifa ya kiume. Kwa mantiki hiyo tafiti zote

hizi ni muhimu kwetu kwani zilitusaidia sana na kuwa kama muongozo katika kuionesha michakato mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia tuliyojaribu kuichunguza na kuidhihirisha michakato hiyo kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

#### **2.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Barani Asia**

Watafiti wengi Barani Asia wametafiti lahaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna ufanano na utofautiano baina ya lahaja hizo kiisimu. Miongoni mwao ni pamoja na Alayan (1975) ambaye alifanya utafiti linganishi baina ya Wazungumzaji wa lahaja ya Harb inayopatikana Saudi Arabia. Katika tafiti yake anasema kuwa kabilia la Harb limegawika katika matawi mawili, tawi la Banu salim ambalo ni kabilia maarufu zaidi, lililogawika tena katika makundi mawili kundi la “Maryawiha” (hawazim) pamoja na “Maymun” ilihali tawi la pili la Harb ni Banu Masruh. Pamoja na hayo Alayan (ameshatajwa) katika tafiti yake hii amegundua kuwa lahaja ya Harb inasifa ya kufanana kifonolojia na lahaja za Anaza, kama vile Shammar na lahaja ya Otaiba anasema kuwa lahaja hizi zinatumia vizuiwa kwamizi vilivyo sawa kama vile [k], [g], [ts] na [dz]. Pamoja na hayo Alayan (ameshatajwa) ameeleza kuwa kabilia la Harb na lahaja za Shammar na Anaza zote zinasisitiza matumizi ya konsonanti [b] katika mazingira maalumu kama vile katika neno */bosal/* sawa na neno “*Onion*” kwa */basal/*. Hatahivyo katika utafiti wake huu amegundua kuwa lahaja ya Harb pamoja na lahaja nyingine hutilia mkazo baadhi ya konsonanti za midomo katika sehemu za irabu mfano katika maneno “*gawi*”..... *guwi*. Sambamba na hayo, Alayan anaendelea kutueleza kuwa kimofolojia lugha ya Harb huwa na majina yenye sifa ya uke ambayo huishia na (a, au ah) kama katika neno */nxala/* (Mchikichi), *xsibah*

(kipande cha ubao) wakati katika lahaja ya “Shammar” maneno yenyé sifa kama hii huishia na (ih) na amegundua kuwa lugha ya Harb imefanana kwa ukaribu na lahaja za Anaza pamoja na kabilä la Otaiba. Hata hivyo katika utafiti wake amegundua kuwa lugha ya Harb inafanana katika ngazi ya viambishi tamati kati yake na lahaja ya Shammar na Anaza kama mifano aliyotupa hapa:-

- Harb - hutumia viambishi tamati vifuatavyo (-ih, uh, u, -ha, ni)
- Shammar - hutumia viambishi tamati vifuatavyo (-uh, -ah, -an)
- Anaza - hutumia viambishi tamati vifuatavyo (-ah, -ha, -ni)


Katika data yake hii anatueleza kuwa lugha ya Harb na Shammar hufanana katika kutumia kiambishi tamati (uh), vile vile anatuambia kuwa Harb inafanana na lahaja ya Anaza katika viambishi tamati viwili yaani (-ni, ha). Vilevile katika utafiti wake amegundua ya kuwa kunasifa zinazojibainisha na kupatikana katika kundi la Hijazi sifa hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:- Sauti za kaakaa gumu kuwakilishwa na viwakilishi viwili mfano [k], [g], [k̄], [ḡ]. Vilevile sifa ya kuchukuliana nafasi kwa baadhi ya sauti kama vile sauti za nazali kama vile nafasi ya [m] huweza kuchukuliwa na sauti [n] kama katika maneno yafuatayo /*Dalħamd*/...../ *Dalħand*/ (sifa). Vilevile Alayan (ameshatajwa) katika tafiti yake hii ametubainishia kuwa lugha za Hijazi zinasifa ya urefushaji wa irabu katika vitenzi kama katika neno / *baac* /..... / *biic* / likiwa na maana ya (uza) na / *gaal* /...../ *guul* / sawa na neno la Kiswahili (ongea). Pamoja na hayo, amegundua ya kuwa sauti ya konsonanti [b] baadhi ya wakati hubadilishana nafasi na konsonanti [m] hususani katika kundi la Hijazi la Harb kama katika maneno:-

*Mirzab*.....*Mirzam* (aina ya nyota), mabadilishano hayo ni yakizamani ambayo hutokea katika lahaja za Arabuni Mashariki.

Mishra na wenzake (2011) wamefanya ulinganishi wa kifonolojia baina ya lahaja za Kihindi. Nakwamba walibainisha aina kuu saba za lahaja zinazopatikana India kama vile “lahaja ya Awadhi”, “Bagheli”, “Bhojpuri”, “Bundeli”, “Haryanvi”, “Kanaudi” na “KhariBoli”. Pamoja na hayo wanadai kuwa lahaja ya Awadhi /Awadh huzungumzwa mikoa ya kati ya “Uttar Pradesh” karibu na Wilaya ya “Lucknow” na “Faizabad” na inajumla ya wazungumzaji milioni 2.5. Vilevile wanadai kuwa lahaja ya Bagheli huzungumzwa sehemu za katikati na kusini mwa “Madhya Pradesh” ikiwa na wazungumzaji milioni 2.8. Ilihali lahaja ya Bhojpuri inazungumzwa eneo kubwa la Mashariki ya “Uttar Pradesh” katikati pamoja na Kusini mwa “Bihai na Jhankhand” ikiwa na wazungumzaji milioni 33. Hatahivyo lahaja ya Bundeli wanasema kuwa inazungumzwa Kusini Magharibi mipakani mwa wilaya 3 “Uttar Pradesh” pamoja na maeneo mapana ya Kaskazini mwa “Madhya Pradesh”. Vilevile lahaja ya Haryanavi inayozungumzwa maeneo ya “Haryana”, “Delhi na baadhi ya sehemu za mipakani mwa “Uttar Pradesh”, Himachal Pradesh” na “Uttarakhand” ina wazungumzaji wapatao milioni 8. Nayo lahaja ya Kanaudi wanasema kuwa inazungumzwa Kusini magharibi mwa “Uttar Pradesh” pamoja na “Uttarakhand” ikiwa na wazungumzaji milioni 6. Vilevile lahaja ya Khari Boli wanasema kuwa inatokea sehemu za magharibi ya Uttar Pradesh na “Delhi” na huzungumzwa maeneo mengi ya “Uttarakhand”, Himachal Pradesh, hata hivyo wanasema kuwa lahaja hii ndio lahaja sanifu katika nchi ya India na inakubalika kwa watu wote. Katika uchunguzi wao huo Wamegundua kuwa kuna irabu 10 za msingi na 2 za kukopwa

ambazo zinawakilisha sauti za Kingereza. Irabu zote 10 zina sifa ya kutamkika kinazali kama mchoro unavyoonesha hapa chini

### **Jedwali 2.2: Irabu zote 10 zinavyoweza kutamkika**



Vile vile lahaja zote hizi hutumia irabu msingi ijapokuwa kuna baadhi ya lahaja hizo zinaonesha alofoni tofauti. Pamoja na hayo Mishra na wenzake (wameshatajwa) wamegundua kuwa lahaja ya “Awadhi” inaonesha tofauti huru za alofoni /e:/, o:/ mpishano au tofauti huru na /ja:/, wa:/ kama katika maneno /dja:khau/~/ de: ,khau/. Hatahivyo wanasema kuwa alofoni /e:/, o: / hufupika endapo zitafuatiwa na konsonanti ndefu kama katika maneno /ek: au/~/ /e: kau/. Pia wamegundua kuwa katika lahaja “Bacheli” irabu [e] na [o] hutokea katika kijalizo (complementary) pamoja na zile maarufu kama vile [i] na [u] kama katika /dustana/ dhidi ya /dostana/ (friendship/ urafiki). Vile vile wanatueleza kuwa konsonati [f] na [z] huwa hazipatikani takribani katika lahaja zote isipokuwa katika “Khari-Boil” kwasababu ni sauti zenye asili ya Kiarabu kwamaana zimekopwa.

Shan (2017) alifanya utafiti kuhusu tofauti kati ya lahaja za Kichina. Katika tafiti yake hiyo amedai kuwa jamii lugha ya Wachina ina aina kuu saba za lahaja zikiwemo “Putonghua” (Mandarin), Gan, Kejia (Hakka), Min, Wu, Xiang na lahaja ya Yue (Contonese), vilevile anadai kuwa lahaja hizi zimetofautiana sana, anadai

kuwa licha ya lahaja hizi zinatofautiana sana lakini kwakiasi fulani hufanana katika jambo moja hasa katika mfumo wa maandishi ambao umejikita katika tabia za Wachina (Chinese characters), lakini hutofautiana katika matamshi kutegemea wapi na yupi anaetamka kama neno /mimi/ la Kiswahili linamatamshi tofauti katika lahaja hizo kwani kila moja hulitamka neno hilo kivyake ingawa ni lugha zinazotokana na jamii lugha moja kwa mfano lahaja ya Mandarin neno hili hutamkwa /wo/ lakini kwa lahaja ya Wu hutamkwa /ngu/, ilihali Wamin wanalitamka /gua/, lakini lahaja ya Cantonese wanalitamka /ngo/. Vilevile Shan (ameshatajwa) anaeleza kuwa lugha za China zinatofautiana katika viwango vyta mpando na mshuko wa sauti (tones) amedokeza mfano kwa kusema kuwa lugha ya Mandarin ina viwango vinne vyta toni wakati lugha ya Cantonese ina viwango sita vyta toni. Corley (2015) yeye amefanya utafiti linganishi na kuonesha ufanano na utofautiano kati ya lugha ya Kichina (Mandarin), Kijapani na Kikorea. Katika utafiti wake huo amegundua kuwa Kikorea na Kijapani vinafanana katika maumbo hasa katika upokeaji wao wa viambishi. Sambamba na hayo anasema kuwa Kijapani na Kikorea vinafanana kimsamiati kwa vile zimekopa msamiati kutoka lugha ya Kichina. vilevile Corley (ameshatajwa) amegundua kuwa Kichina hujengwa kwa silabi moja wakati mofimu za Kijapani na Kikorea huwa na mjengeko wa silabi ndefu, pamoja na hayo amebaini kuwa lugha ya Kichina haiendani na uambishaji pamoja na mnyambuliko bali huendana na mfumo wa mofimu nzima (compound morphemes) lakini lugha ya Kijapani na Kikorea huendana na sifa ya uambishaji na mnyambuliko wa viambishi vyta mwisho.

Kwa minajili hiyo basi tafiti zote hizi ni muhimu katika kazi yetu kwa vile ni tafiti linganishi kwani zimelingana sana kiutekelezwaji na tatizo la tafiti hii na

zilimuongoza sana mtafiti katika kushughulikia tatizo hilo kulingana na malengo husika.

## **2.5 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Barani Amerika**

Watafiti wengi Barani Amerika wametafiti lajaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana ama kutofautiana kwa lajaja hizo katika vigezo vyta kiisimu mionganoni mwa watafiti hao ni pamoja na Ash na Boberg (2006) kama walivyonukuliwa na kutumika katika tafiti ya Ali (2015) wanaeleza kwamba wasemaji wa Marekani Kusini huonesha tofauti katika maeneo yao kwa kutumia “diphthong” katika maneno hayo. Tofauti hasa ni Carolina Kaskazini, Kusini na Magharibi ambako irabu unganifu [ai] hutamkwa kama irabu moja [a] ambapo wasemaji wengi huonesha kipengele hiki katika ncha ya maneno na kabla ya konsonanti alionesha lakini si kabla ya konsonanti isompumuo. Kazi hii ni muhimu sana kwani ilikuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji na utatuzi wa tatizo la utafiti wetu kwa vile ilikuwa kama muongozo uliomuongoza mtafiti katika kuzibainisha tofauti za kifonimu zilizopo baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

## **2.6 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi Barani Afrika**

Barani Afrika nako hakukuwa nyuma kuhusu uchunguzi wa lugha na lajaja zake katika kuangalia asili na chimbuko la lugha na lajaja hizo pamoja na miingiliano, miachano na miathiriano yao ya kiisimu baina yao. Hivyo wataalamu mbalimbali waliandika pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za kiulinganishi wa kiisimu Barani Afrika na kuudhihirishia ulimwengu matokeo ya kazi zao na kuwa kama chachu kwa watafiti wengine katika kufanya tafiti nyingine zinazohusiana na ulinganishi wa

kiisimu. Kwa mintarafu hiyo basi katika kuonesha kazi mbalimbali zilizofanywa Afrika tulizigawanya kazi hizo kwa kuzingatia miachano ya kijiografia kama.

### **2.6.1 Kazi Tangulizi Kuhusu ulinganishi wa Kilahaja Afrika ya Kaskazini**

Watafiti wengi Afrika Kaskazini wametafiti lahaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana ama kutofautiana kwa lahaja hizo katika Nyanja mbalimbali za kiisimu mionganoni mwa watafiti hao ni pamoja na, Montes (2015) amefanya utafiti linganishi baina ya lahaja za Kiarabu zipatikanazo miji ya Mediterenia kati Tangier Morocco na Tunis. Katika tafiti yake amegundua kuwa lahaja ya Kiarabu Tangier, Morocco na lahaja ya Kiarabu cha Tunis zote zinatokana na uvamizi wa waislamu wa Kaskazini mwa Afrika mnamo karne ya saba lakini hazitokani na historia ya aina moja. Pia anasema lahaja hizi zinalingana Kimofosintaksia na hazina mfumo wa kubainisha jinsia katika miuundo yake ya maneno.

Sharman (2014) ambaye aliandika kuhusu ulinganishi wa kiisimu baina ya lahaja za Misri (Egypt) na lugha za Kibantu. Katika kazi yake hii amebaini kuwa lugha za Misri zinawiana na lugha za kibantu katika utumiaji wa viambishi awali, vilevile anasema kuwa kihusishi “m” cha Kiswahili – Bantu kimelingana na Konsonanti “m” ya lahaja za Kimisri kwa kudai kuwa kihusishi “m” au “mu” katika lugha za Kibantu hufanya kazi ya kuonesha kitu kuwa kipo ndani / ndani ya kwa mfano “*in the Sky*” huwa kama “Mu – julu” katika lahaja ya Kibantu ya “BoTatwe” hata hivyo katika lahaja za Kimisri hutumika kama “Mu P-T” yaani “*in the Sky*” kwa mantiki hiyo mifano ya virai vyote viwili ni sawa kisarufi na kimuundo ispokuwa neno “Sky” ndio tofauti. Hata hivyo anasema kuwa lahaja za Misri zinafanana Kimsamiati na lugha za Kibantu; mfano neno

NIK ..... NIOKA ..... NYOKA. Vilevile Sharman (ameshatajwa) anatueleza kuwa neno “RA” la lahaja ya Kishona ambalo pia hutumika katika lahaja ya Kono linabeba maana moja ya juu, sambamba na hayo lahaja za Misri hutumia neno BENIA ambalo hubeba maana ya kuchomoza / kuangaza ambapo Kizulu hutumia neno “BANI”, halikakadhalika Sotho Bantu hutumia “BENIA” yenyе maana ya kuangaza

Misri.....WBKH yaani hodari  
 Kishona.....WA + BAKA yaani hodari  
 Kibemba.....WA + BEKA yaani hodari

Ingawa kazi hizi zilifanyika nje ya Afrika ya mashariki lakini ziliwa na umuhimu mkubwa katika tafiti yetu hii kwa vile ni tafiti linganishi na zimepitia vipengele vya kiisumu ambavyo tulivichambua katika tafiti yetu hii.

### **2.6.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Afrika ya Magharibi**

Watafiti wengi Afrika Magharibi wametafiti lahaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana na kutofautiana kwa lahaja hizo katika vigezo vya kiisumu mionganoni mwa watafiti hao ni pamoja na Kaseem na Ekerete (2013) ambao waliangalia lahaja za Kingereza nchini Nigeria kwa kutumia mtazamo wa Kingereza cha Ulimwenguni. Katika uchunguzi wao wamegundua kuwa Kingereza cha Hausa (EHE) kipo karibu sana na RP, kikilinganishwa na Kingereza cha Yoruba (EYE) na kile cha Igbo (EIE). Hatahivyo wamebaini kuwa (EHE) ipo karibu sana na (SBE) yaani (Starndad British English) katika kuzitambua irabu za kati, wazi, na za chini.

Kwa mfano:-

S.B.E - / Kœnfrænt əz/ - (confront us)  
 E. H. E - / Kλánfrænt εz/- (confront us)  
 E. I. E - / Kɔfrænt ɔs/- (confront us)  
 E. Y. E - / Kɔfrænt ɔs/- (confront us)

Vile vile wamebaini kuwa Kihausa kina “pair” tano (5) za monophthongs” zinazotofautiana kiurefu, pamoja na hayo wanasema kuwa Kingereza cha Kaskazini irabu [a] huwa kama [ʌ] wakiwa na maana irabu [ʌ] ya Kihausa ni sawa na lugha ya Kingereza [ʌ] kama katika neno */cut/* katika mazingira mengine. Hivyo wanasema Hausa ndio lugha pekee inayowakilisha[ʌ] ikilinganishwa na lugha nyingine za Nigeria kwa mfano:-

S. B. E - / Mæltɪlætərələzm /  
 E. H. E - / Mæltɪlətərələzm /

Tofauti katika maneno haya ni sauti [æ], [a], [ə] – [l]. Hata hivyo wanaeleza kuwa othografia ya Hausa sauti [p] huwakilishwa na sauti [f] ambayo hulazimika kuwa kipasuo cha midomo. Halikadhalika “E. Y. E” hutumia kitamkwa [s] penye sauti [Č], vile vile sauti [Φ] kwenye herufi ya mwanzo [h], nayo sauti [s] hutumiwa kwenye sauti [z] na hutumia [f] kwenye [v]. Hivyo wanasema kuwa katika lugha ya Kiyoruba sauti [Č], [z], na [v] hazimo. Sambamba na hayo wamegundua kuwa Wayoruba hutamka */gel/* kuliko */gɛ:l/, /sket/* kuliko */skɛ:t/, /fem/* kuliko */fɛ:m/* hivyo wanasema kuwa [ɛ] ni mfumo wa Yoruba Shibboleths. Vilevile Kaseem na Ekerete (wameshatajwa) wamebaini kuwa [ɔ] na [a] ni fonimu za msingi katika Yoruba kuliko ile ya Kingereza [ə], wakiendelea kutueleza kuwa Wayoruba hutumia [ɔ] pahala pa [ʌ]. Mbali na hayo pia wamebaini kuwa Yoruba (E. Y. E) hutofautiana na Starndad English ( S. B. E) kwani wanasema katika jamii ya Wayoruba sauti [ u] hutamkwa midomo ikiwa duara au mviringo wakati [ʊ] ya (S. B. E) inapotamkwa

hukosa mduara. Vilevile katika kazi yao hii wamegundua kuwa “Igbo” ina konsonanti 20 , vile vile wanadai kuwa katika “Igbo” irabu [e] huwakilishwa na alofoni mbili yaani [e] na [ɛ] na wazungumzaji wake huzipa sifa ya ukati, fupi, mbele, na sifa ya ulax kama mifano inavyoonesha hapa:-

S. B. E  
 Paid = hutamkwa hivi /peid/  
 Game = hutamkwa hivi /gelm/

E. I. E  
 Lakini Igbo hutamkwa /ped/  
 Wakati Igbo hulitamkwa / gem/

Tafiti hii ilikuwa kama muhimili mkuu katika kazi yetu hii kwani ilitupa muongozo mkubwa katika kuzibainisha tofauti za kifonimu baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

### **2.6.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilugha Afrika ya Kusini**

Watafiti mbalimbali Afrika ya Kusini wamefanya tafiti linganishi kuhusu lugha na mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana na kutofautiana kwa lugha hizo katika Nyanja za kiisimu mionganoni mwa watafiti hao ni pamoja na. Rycroft (1980) amefanya utafiti linganishi wa utamkaji na lafudhi baina ya lugha ya Ndebele na Zulu, katika tafiti yake hiyo amegundua kuwa lugha ya Ndebele na Zulu zote zinatokana na Proto – Zulu lakini zinatofautiana kwani amebaini kuwa Ndebele hutumia sauti [tsh] pahala ambapo Zulu hutumia sauti [sh], pamoja na hayo amegundua kuwa Ndebele sauti [h] hujitokeza kama kikwamizi cha glota kama Kingereza [h] au Kiskotish [ch], kwa Wazulu halitofauti. Vile vile amegundua kuwa jamii hizi zinatofautiana kimatumizi kati ya sauti [l] na [n] kwani Ndebele hutumia [l] pale Zulu wanapotumia [ n] katika viambishi awali maalumu na katika viwakilishi kama vidokezo vyta mifano aliyotoa inavyoonesha:-

NDEBELE	hutamka ..... / <i>Lin</i> / wakiwa na maana ya (You, plural, or absolute pronoun)
ZULU	hutamka ..... / <i>Nin</i> / wakiwa na maana ya (You, plural, or absolute pronoun)
SOTHO	hutamka ..... / <i>Lena</i> / wakiwa na maana ya (You, plural, or absolute pronoun).

Kwa minajili hiyo basi tafiti hii ni muhimu katika kazi yetu kwani ilitupa mchango mkubwa sana na kuwa kama muongozo wakati mchakato wa tafiti hii ulipokuwa ukiendeshwa na mtafiti katika kulidhihirisha na kulikamilisha lengo la kwanza la tafiti hii ambalo limelenga kubainisha mfanano na utofauti wa fonimu kimatumizi kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

#### **2.6.4 Kazi Tangulizi Kuhusu ulinganishi wa lahaja Afrika ya Mashariki**

Watafiti mbalimbali Afrika ya mashariki wametafiti lahaja mbalimbali, kazi hizo zimegawanywa kimaeneo kulingana na muachano wa Kijiografia kama

##### **2.6.4.1 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Nchini Kenya**

Miongoni mwa watafiti waliojishughulisha na ulinganishi wa lahaja nchini Kenya ni pamoja na, Whiteley (1956) alifanya utafiti kuhusu lahaja ya Kimtang'ata, katika tafiti yake hii ameleezea zaidi juu ya matamshi ya lahaja hiyo. Jambo muhimu aliloligusia ni kwamba lahaja zina sifa zake zenye kutafautiana baina ya lahaja moja na nyingine. Naye Gaithuma (2016) amechunguza athari za kifonolojia za lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu, katika uchunguzi wake huo amefanikiwa kugundua kuwa Kiamu kina fonimu 35 na Kitikuu kina fonimu 34. Pamoja na hayo

ni kwamba alifanikiwa kubaini kuwa lahaja ya Kitikuu ina athari nyingi katika Kiswahili kuliko Kiamu. Hivyo kazi hizi ni muhimu na zilimuongoza vyema mtafiti katika kuzibainisha sifa za kiisimu kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kwa lengo la kuchunguza uwiano na utofauti wa kiisimu uliopo baina ya jamii lugha hizo.

#### **2.6.4.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Lugha na Ulinganishi wa Kilahaja Nchini**

##### **Tanzania**

Watafiti mbalimbali Nchini Tanzania wametafiti lahaja mbali mbali na kugundua kuwa kuna mfanano na utofautiano na hata muathiriano baina ya lugha moja na nyingine ama lahaja na lahaja au lahaja na lugha kuu katika nyanja za kiisimu miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Nyanda (2015) amechunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili Urambo, hivyo kupitia muongzo wa nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia amebaini kuwa kuna athari za kimsamiati kwani anasema kuna baadhi ya Wanyamwezi hufanya makosa ya kuingiza msamiati wa lugha ya Kinyamwezi wakati wanapozungumza Kiswahili kama:-

##### **KINYAMWEZI**

Linolilisata  
Nokokunkuguma

##### **KISWAHILI**

Jino linauma  
Nitakupiga.

Vile vile amegundua kuwa Wanyamwezi hukiathiri Kiswahili kimatamshi kwani wao hutumia sauti [l] sehemu ambapo Kiswahili hutumia sauti [r] na kwamba sauti [gh] hupotoshwa na kuwa [g], halikadhalika sauti [s] hupotoshwa na kuwa [s], vilevile Wanyamwezi wanapojifunza Kiswahili sauti [dh] huipotosha na kuwa [s] kama:-

<i>Dhambi</i>	huwa .....	<i>Sambi</i>
<i>Maradhi</i>	huwa .....	<i>Marasi</i>

Sambamba na hayo Nyanda (ameshatajwa) ameweza kubaini kuwa kuna athari za kimaana zitokanazo na lugha ya Kinyamwezi zinazoingizwa katika Kiswahili sanifu kama:-

<b>KNY</b>	<b>KISW</b>
Namsanga	Nimemkuta
Kuduhu	Hayupo
Igolo	kesho
Igolo	jana.

Naye Magesa (2017) alifanya tafiti linganishi changanuzi wa mofu njeo za Kikara na Kiswahili sanifu, katika tafiti yake hiyo alibaini kuwa kuna utofauti katika utokeaji wa mofu njeo baina ya Kikara na Kiswahili, kwani anatueleza kuwa katika Kikara mofu njeo hutokea baada ya mofu kanushi na kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali, ilihali katika Kiswahili mofu njeo kanushi hutokea mwishoni mwa kitenzi kama kiambishi tamati akilithibitisha hilio ametoa mfano hapa chini;

Kikara <i>/chi-t- e- nok- a/</i>	Kiswahili <i>/ha- tu- chum- i/</i>
-------------------------------------	---------------------------------------

Katika mifano hii Magesa (ameshatajwa) anafafanua kuwa kiambishi [e] kilichopo nyuma ya mzizi wa neno [nok] kinafanya kazi kama njeo katika Kikara, wakati kiambishi [i] kilichopo mwishoni mwa mfano wa Kiswahili ndicho kinachofanya kazi ya mofu njeo kanushi.

Ingawa tafiti ya Nyanda (ameshatajwa) hii ililenga kuonesha athari za Kinyamwezi katika Kiswahili lakini ina umuhimu mkubwa sana katika kazi yetu kwani ilitupa njia

muwafaka katika kuzibainisha tofauti na mfanano wa kifonimu, nayo kazi ya Magesa (ameshatajwa) ilisaidia katika kulinganisha utokeaji wa njeo kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

#### **2.6.4.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Ulinganishi wa Kilahaja Zanzibar**

Visiwani Zanzibar watafiti mbalimbali, wametafiti lahaja mbali mbali na kubaini kuwa lahaja hizo zinafanana na kutofautiana kati yao na hata na lugha kuu yaani Kiswahili kupitia nyanja za kiisimu mionganoni mwa watafiti hao ni pamoja na. Mohamed (1984) alifanya utafiti unaohusiana na lahaja ya Kipemba, Kiunguja mjini pamoja na Kiswahili sanifu. Utafiti wake ulijihuisha zaidi na kuelezea matamshi ya lahaja ya Kipemba, pamoja na kuzungumzia jinsi ukarusha unavyojitokeza ndani ya lugha hizo. Katika uchambuzi wake amedhihirisha mambo makuu mawili. Kwanza misamiati kadhaa ya lahaja ya Kipemba na jinsi inavyotofautiana na Kiswahili sanifu, pia ameonesha mabadiliko ya sauti mbalimbali na jinsi yanavyotofautiana kuanzia mjini hadi vijijini. Vile vile ameonesha kuwa katika lahaja ya Kipemba umilikaji wa vitu hujitokeza ndani ya nomino husika kama “*nyumbayo*” badala nyumba yako, “*pahalape*”, badala ya pahala pake. Naye Juma (2011) alichunguza tofauti za kiisimu kati ya Kiswahili cha Micheweni na Wete. Katika tafiti yake hiyo aliangazia tofauti za kifonolojia, kimsamiati na kimofolojia. Halkadhalika katika kipengele cha msamiati aliangalia maneno yenyeye maana sawa au maana zinazokaribiana na jinsi maneno hayo yanavyotofautiana kimaumbo pia alibainisha tofauti za kimsamiati kupitia vikoa vyya maana. Naye Ali (2015) alichunguza tofauti ya msamiati wa Kipemba cha Kaskazini na Kile cha Kusini. Kupitia nadharia ya isimu linganishi amegundua kuwa Kipemba cha Kaskazini kimehifadhi msamiati wa

Kipemba cha kale wakati kile cha Kusini kinataka kufanana na Kitumbatu lakini kwa kiasi kikubwa anasema kinaelekea kwenye Usanifu. Kana kwamba haitoshi pia aligundua tofauti za kimatumshi kati ya Kiswahili cha Kaskazini na kile cha Kusini kwani anasema kuna baadhi ya sauti baina ya jamii lugha hizo mbili zinakimbiana kama:-

<b>KSW / KSK</b>	<b>KSW/ KUS</b>	<b>TOFAUTI</b>	<b>KSW/ SAN</b>
Bupuru	Bufuru	p/f	Bupuru
Vumbi	Dumbi	v/d	Vumbi
Kofyoka	Gofyoka	k/g	Tapika.

Naye Bakari (2015) alifanya utafiti linganishi wa kiisimu kati ya lahaja ya Kipemba na Kitumbatu, kupitia nadharia ya fonolojia zalishi pamoja na lahaja na ulahajia amefanikiwa kubainisha tofauti kubwa za kifonolojia kati ya jamii lugha hizo na kwamba anasisitiza kuwa tofauti hizo hujitokeza katika idadi na aina za fonimu na hata kimatumizi katika baadhi ya fonimu kama aliyojaribu kutuonesha katika jedwali Na 4.2:-

### **Jedwali: 2.3 Tofauti ya Kimatumizi kwa Sauti zenye Asili ya Kiarabu baina ya Kipemba na Kitumbatu.**

<b>Kipemba</b>	<b>Kitumbatu</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>
[θawabu]	[Sawabu]	<b>Thawabu</b>
[θelaθini]	[Sala s ini]	<b>Thalathini</b>
[θubutu]	[subutu ]	<b>Thubutu</b>
[Aθiri]	[Asiri]	<b>Athiri</b>

Katika data yake hii anaonesha jinsi jamii lugha hizi zinatofautiana katika kimatumizi ya fonimu kwani Kipemba kinatumia sauti [th] sawa na Kiswahili sanifu

lakini Kitumbatu hakina sauti hiyo na badala yake hutumia sauti [s] kuwakilisha sauti [th]. Naye Hassan (2016) ametafiti namna ya ujidhihirishaji wa mofu zinazowakilisha nafsi na njeo katika Kiswahili. Utafiti linganishi wa lahaja ya Kipemba. Kupitia nadharia ya mofolojia, amegundua kuwa kuna tofauti kubwa ya udhihirikaji wa mofu nafsi na njeo baina ya Kipemba na Kiswahili sanifu tofauti hiyo ipo katika idadi kwani anasema Kipemba kinaidadi kubwa ya mofu nafsi kuliko Kiswahili sanifu. Hatahivyo Bakari (2015) amechunguza tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba na Kikojani. Katika tafiti yake hii ametumia nadharia ya mawimbi pamoja na isimu linganishi kupitia nadharia hizi amegundua ya kuwa umbali wa kijiografia, wakati, na kazi au shughuli ndizo hupelekea tofauti za kimsamiati katika lahaja. Vilevile anadai kuwa lahaja hizi zinatofautiana kimaana, kimamatamshi na maumbo ya msamiati. Kwa ujumla ni kwamba kazi hizi ni muhimu kwa utafiti huu kwani zilimsaidia mtafiti kupata muongozo mzuri katika kulinganisha maana za kimsamiati pamoja na kanuni za kifonolojia na mofonolojia zinazotawala maumbo ya mofu zijengazo maneno ya Kiswahili cha Paje na yale ya Makunduchi.

#### **2.6.4.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Kimakunduchi**

Watafiti mbalimbali waliitafiti lahaja ya Kimakunduchi na kubaini kuwa lahaja hii inafanana na kutofautiana kati yake na lugha kuu yaani Kiswahili na hata lahaja ndogondogo zilizotokana na Kiswahili hata vile vilahaja vitokanavyo na lahaja hiyo, watafiti hao ni pamoja na. Mohamed (2013) alifanya tafiti kuhusu athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kinachotumika Shuleni Makunduchi Zanzibar. Katika tafiti yake hii akiongozwa na nadharia ya Umaumbo, amefanikiwa kugunduwa kuwa Kimakunduchi kinafanana na Kiswahili sanifu katika

ubebaji viambishi nafsi zote isipokuwa hutofautiana katika nafsi ya pili wingi na ya tatu umoja kwani anatueleza kuwa Kiswahili sanifu wingi wa nafsi ya pili na umoja wa nafsi ya tatu huwakilishwa na “u” na “a” ilihali Kimakunduchi huwakilishwa kwa “ku” na “ka”. Naye Bauuai (2017) amechunguza muundo wa Kirai nomino katika lahaja ya Kimakunduchi. Katika tafiti yake hii ameongozwa na nadharia ya sarufi miundo virai na x baa. Amebaini kuwa muundo wa Kirai nomino cha Kimakunduchi una sifa ambazo hazipombali na lahaja nyingine pamoja na Kiswahili sanifu na hivyo ameeleza kuwa muundo huo unafanana na ule wa lahaja za Kibantu. Naye Juma (2011) alilinganisha msamati wa Kimakunduchi, Kibwejuu, Kimtende, na Kikizimkazi. Katika tafiti yake hii ameongozwa na nadharia ya Mwachano na Makutano, na kufanikiwa kubaini kuwa Kibwejuu na Kimtende vinatokana na lahaja kuu ya Kimakunduchi na Kikizimkazi si mionganoni mwa lahaja za Kimakunduchi kwani anadai kuwa Kikizimkazi kimeathiriwa mno na Kiunguja mjini. Pamoja na hayo Kipacha (2003) Katika kazi yake anasema Kimakunduchi ni lahaja inayojulikana kwa majina mbalimbali kama vile Kikale, Kikae, au Kihadimu. Pia anasema kuwa lahaja hii inazungumzwa katika sehemu za Bwejuu na katika baadhi ya vijiji vya Jambiani upande wa pwani ya Kaskazini ya Makunduchi na kwa magharibi, huzungumzwa katika sehemu za Kizimkazi na Muyuni pamoja na kisiwa cha Uzi. Hatahivyo Kipacha (ameshatajwa) katika kazi yake hiyo amebainisha orodha ya leksimu za Kimakunduchi kama vile:-

<b>Mak</b>	<b>Ksw</b>	<b>Vidokezo</b>
Kunyono?	Umeniona?	Ku-: u-
Kagwa	bwagwa	ka: bwa
Hamona	nimemuona	ha: ni.

Naye Juma (2006) alichunguza Msamiati na Vitenzi katika Lafudhi za Jambiani, Paje, na Bwejuu Katika Lahaja za Kimakunduchi, katika tafiti yake hiyo aligundua kuwepo kwa lahaja ndogondogo zinazotokana na lahaja kuu ya Kimakunduchi ambazo zina mfanano wa msamiati na maumbo yake katika lahaja za Kijambiani, Kipaje na Kibwejuu. Mfano wa maneno yenyе mfanano ni kama kanamkaza - anampenda, mnafana - mnapendeza. Ingawa vilahaja hivyo hufanana lakini baadhi ya wakati hutofautiana katika maumbo ya maneno mfano wa neno “**evu**”, wote wanatumia mzizi “**evu**” katika vitenzi vyao, mfano wa maneno “**aliolewa**” na “**tuliapa**”.

**Kimakunduchi:** kevukaolegwa, t<sup>e</sup>vutulapa

**Kibwejuu:** kevukaolegwa, kevutulapa 21

**Kipaje:** evugakaolegwa, evugatulapa.

**Kijambiani:** kaolegwa, tulapa (Hawa hawatumii evu wala kevu).

Hivyo kazi hizi zilimsadia sana mtafiti katika kuzibaini sifa bainifu za kifonolojia na kimofolojia pamoja na leksimu zinazopatikana katika lahaja ya Kimakunduchi na kufanikiwa kuyafikia malengo yake la pili na la tatu katika utafiti huu.

## 2.7 Pengo la Maarifa

Baada ya mtafiti kusoma kazi tangulizi za watafiti mbalimbali aligundua kuwa tafiti nyingi za kilahaja zimefanyika ulimwenguni kote kwani mtafiti aliangalia kazi za Barani Ulaya, Asia, Amerika na Afrika kwa ujumla wake. Hata hivyo tafiti linganishi nyingi zao zilizokuwa zimefanywa zilihusu zaidi lahaja ya Kipemba (Bakari 2015, Ali 2015, Juma 2011), Kipemba na Kitumbatu (Bakari, 2015) na chache tu ndizo ziliangazia ulinganishi wa lahaja ya Kimakunduchi (Juma 2011, Juma 2006, Mohamed 2013). Hata hivyo mtafiti aligundua kuwa tafiti hizo ziliangazia zaidi kipengele cha msamiati na chache zililinganisha msamiati na vitenzi na nyingine

kuangazia athari za kiisimu na kuacha pengo kubwa la kiutafiti ambalo lilihitaji kufanyiwa utafiti hasa katika maeneo ya fonolojia na mofolojia zaidi katika vipengele vya fonimu pamoja na michakato ya kimofofonolojia katika ukokotoaji wa maumbo ya ndani ya nomono, vivumishi na vitenzi katika kuyaleta nje pamoja na ulingano wa kimaana katika msamiati wa msingi, maeneo ambayo yalikuwa bado hayajapata fursa ya kuangaziwa kwa kina kati ya Kimakunduchi na vilahaja vyake. Vipengele ambavyo mtarufi aliviona kuwa ni vya muhimu na ipo haja ya kuvifanyia utafiti linganishi. Hivyo utafiti huu ulivishughulikia vipengele hivyo kwa kuangazia mfanano na utofauti wao kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi, kwani mtarufi aliamini kuwa hakuna mtarufi ye yote aliyewahi kuvichunguza na kuvifanyia ulinganifu vipengele hivyo. Ili kuliziba pengo hilo mtarufi aliongozwa na nadharia mbili; Mofofonolojia na isimu linganishi, pamoja na mbinu ya usaili, mahojiano, ushuhudiaji.

## **2.8 Kiunzi cha Nadharia**

Mtarufi katika utafiti wake huu aliongozwa na nadharia mbili zinazoendana na mada husika ambazo ni Nadharia ya Mofofonolojia pamoja na Nadharia ya isimu linganishi.

### **2.8.1 Nadharia ya Mofofonolojia**

Nadharia ya Mofofonolojia ni nadharia ambayo imeasisiwa na Baba wa Sarufi Zalishi, Nikolaj Trubetzkoy, katika mkutano wa kwanza wa wanafilolojia wa Ki-Slavu uliofanyika Prague mnano 1929. Trubetzkoy alitumia neno “mofofonolojia” akiwa na maana ya kuwa ni tawi la isimu litakaloshughulikia matumizi mbalimbali ya mofolojia katika kuchambua na kuonesha tofauti fulani za kifonolojia. Kwa

mujibu wa Trubetzkoy nadharia hii inajengwa na mambo makuu matatu, la kwanza ni kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha, la pili ni kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana na la tatu ni kuchunguza ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu wa kimofolojia. Hata hivyo nadharia hii iliwahi kutumiwa na wataalamu mbalimbali katika kuzichanganua lugha kiisimu miiongoni mwao ni pamoja na Bloomfield (1930) yeche alitumia msamiati wa “mofofonemiki” ambao ulibeba maana sawiya na nadharia ya mofofonolojia ya mwanaisimu Trubetzkoy na ilitumika katika kuchunguza mabadiliko ya sauti kwa mahitajio ya kimofolojia katika isimu ya Kimarekani. Vile vile nadharia hii imewahi kutumiwa na Hassan (2016) katika kuonesha ujidhihirishaji wa mofu zinazowakilisha nafsi na njeo katika tafiti yake linganishi kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Ilimsaidia sana katika kuainisha mlingano wa ujidhihirishaji wa mofu nafsi na njeo baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba, vile vile ilimsaidia na kumuongoza vyema katika kubainisha mabadiliko ya Kimofonojia yanavyoathiri maumbo ya mofu nafsi na njeo baina ya Kiswahihili sanifu na lahaja hiyo. Kwa vile watafiti tangulizi waliitumia nadharia hii katika nyanja hizo. Kutokana na nadharia hii inahusiana na mofofonolojia mtafiti aliona kuwa ni nadharia bora na faafu katika utafiti huu kwani ilimuongoza vyema katika kuyakamilisha pamoja na kuyafikia malengo mawili ya tatizo la utafiti, yaani lengo lakwanza na lapilli yaliyolenga kuchunguza pamoja na kubainisha mfanano na utofauti wa kifonimu kimatumizi pamoja na michakato ama kanuni za kifonolojia na mofofonolojia zinazotawala maumbo ya mofu zinazojenga maneno ya Kiswahili cha Paje na yale ya Makunduchi, kwavile malengo hayo yanakwenda sambamba na mambo ya msingi yatokanayo na nadharia hii. Hivyo basi nadharia hii ilikuwa na

umuhimu mkubwa sana wa kutumika katika kazi hii kwavile ilimuongoza mtafiti katika kubainisha mfanano na utofauti wa matumizi ya fonimu baina ya jamii lugha hizo, sambamba na hayo ilimuongoza vyema mtafiti katika kuibaini michakato ya kimofofonolojia itumikayo katika uundaji au mifanyiko ya maumbo ya maneno baina ya jamii lugha hizo. Licha ya kuwa nadharia hii ilikuwa na umuhimu wa kiasi hicho kwa mtafiti katika utafiti huu lakini kwa upande mwengine bado nadharia hii ilikuwa na kasoro zake katika utafiti huu kwani ilishindwa kumuwezesha mtafiti katika kufikia lengo la tatu la utafiti huu kutokana na kuwa nadharia hii hailengi kuchambua msamiati na maana zake hivyo basi kutokana na upungufu huu juu ya nadharia hii mtafiti alilazimika kuongeza nadharia nyingine ili kufikia na kukamilisha lengo la tatu la utafiti huu na aliona kuwa nadharia ya isimu linganishi ndio nadharia muafaka na faafu zaidi katika kukamilsha lengo husika.

### **2.8.2 Nadharia ya Isimu Linganishi**

Nadharia ya isimu linganishi imeanzishwa katika karne ya 19 na 20 na iliasisiwa na mwanaisimu “Morris Swadesh”. Lengo la kuanzishwa nadharia hii ni kulinganisha lugha pamoja na kuchunguza uhusiano wa lugha hizo kihistoria.

Hata hivyo, nadharia ya isimu linganishi ina majukumu matatu ya msingi ambayo ni kulinganisha mofolojia, sintaksia pamoja na msamiati wa lugha mbili ilikuthibitisha kuwa zina asili moja. Nadharia hii huchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika lugha. Mabadiliko ambayo huleta tofauti kubwa katika lugha lakini kwa kiasi kikubwa tofauti hizo huonekana katika msamiati. Mbali na hayo nadharia hii iliwhi kutumiwa na wataalamu mbalimbali na kufanikiwa kuonesha mlingano uliopo baina ya lugha mbili au zaidi mionganoni mwa wataalamu waliowahi kuitumia nadharia hii

ni pamoja na. Bakar (2015) aliiutumia nadharia hii katika tafiti yake iliyokuwa imedhamiria kuchunguza tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba na Kikojani katika mawasiliano ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba hata hivyo nadharia hii ilimsaidia kuchunguza na kubaini sababu za utofauti wa kimsamiati baina ya jamii lugha mbili hizi, pamoja na hayo ilimsaidia kubaini athari ambazo zinajitokeza katika mawasiliano kati ya Wazungumzaji wa Kipemba na Wakikojani. Pia imemuwezesha kufafanua tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba na Kikojani. Hata hivyo Ali (2015) aliiutumia nadharia hii katika utafiti wake ambao ulilenga kutofautisha msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Na ilimsaidia katika kubainisha tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini kama haitoshi nadharia hii ilimsaidia katika kuelezea sababu mbalimbali zilizopelekeza tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Hivyo nadharia hii ilitumika na ilimuongoza vyema mtafiti katika kufanikisha lengo la tatu la utafiti huu lililodhamiria Kubainisha uwiano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi. Nadharia hii ni muhimu sana katika utafiti huu kwani ilisaidia katika ubainishaji wa ufanano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa jamii lugha mbili hizo kwavile mionganoni mwa kazi za msingi za nadharia hii nipamoja na kulinganisha msamiati wa lugha mbili kazi ambayo imelingana pamoja na kuendana sana na lengo letu la tatu ambalo limejikita katika ulinganishaji wa kimaana kati ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi Kusini Unguja.

## 2.9 Muhtasari wa sura

Sura hii imeonesha kazi tangulizi za wataalamu tofauti ambazo mtafiti alizipitia, pengo la utafiti. Na mwisho, sura hii imeonesha mkabala wa kinadharia ambao uliongoza utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika kufikia malengo ya utafiti huu. Mambo yaliyofafanuliwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu /mkabala wa utafiti, kundi lengwa, njia / mbinu za kukusanya data, sampuli na usampulishaji, aina za data, vifaa vya utafiti, mbinu za uchambuzi wa data na hitimisho la sura.

#### **3.2 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Unguja Mkao wa Kusini Unguja, katika Wilaya ya Kusini Unguja katika kijiji cha Paje na Makunduchi. Mtafiti ameyateua maeneo haya kwa sababu wakaazi wake wengi ni wale wenye asili ya Kusini Unguja na ambao wanaendelea kutunza tamaduni zao yakiwemo matumizi ya lugha zao katika shughuli za kila siku, pamoja na sababu za kiisimu jamii kama vile uwepo wa tofauti ndogondogo za kijiografia na shughuli za kiuchumi. Sababu nyingine ni za kiisimu kama vile: utofauti wa kifonimu na maumbo ya maneno pamoja na maana na miundo ya sentensi zipatikanazo baina ya jamii lugha za maeneo teule.

#### **3.3 Usanifu wa Utafiti**

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unao onesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika (Kothari, 2008). Utafiti huu ulikuwa ni uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo humuamuru mtafiti kuteua sehemu au jambo au kitu maalumu ambacho atakifanya utafiti kati ya vingi vilivyopo ili aweze kukidhi mahitaji ya utafiti wake (Yin, 1994). Aina hii ya usanifu ni muafaka na ni bora zaidi kwa utafiti huu kwa sababu inatoa

fursa kwa mtafiti kulitafiti jambo moja kwa muda wa kutosha na hivyo kupata majibu sahihi ya maswali ya utafiti (Robson, 2007). Cresswel (2009) anaeleza kuwa mbinu hii humuwezesha mtafiti kuzama na kulitafiti jambo moja kwa undani kabisa na kisha kulitolea mahitimisho stahiki. Naye Kothari (2008) anasema kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuufanya utafiti wake kwa gharama nafuu.

### **3.4      Kundi lengwa**

Kundi lengwa ni vitu au watu ambao mtafiti atawatumia ili kupata taarifa kuhusu tatizo la utafiti wake (Caeser 1998). Kundi lengwa la utafiti huu lilikuwa la watu wazima wenye umri kati ya miaka 40 - 70 pamoja na wasomi wa somo la Kiswahili kwa ngazi ya kidato cha tano / sita pamoja na shahada ya kwanza wenye umri kati ya 25 - 39 amba ni wazaliwa wa vitongoji vya Paje na Makunduchi, watoa taarifa hao walipatikana kupitia mtendaji wa kijiji na mara idadi kuwa kubwa mtafiti aligawa nambari kwa watafitiwa wake kuanzia moja hadi thelathini na kuwachagua wale wote waliopata nambari zisizogawika kwa mbili ndio waliotumika katika utafiti huu. Mtafiti aliliteuwa kundi hili kwa sababu alikuwa na mategemeo makubwa ya kupata data halisi na sahihi katika utafiti huu.

### **3.5      Sampuli na Usampulishaji**

Sampuli ni watoa taarifa ambao huchaguliwa kutoka katika kundi maalumu la walengwa wa utafiti. Watoa taarifa hao huchaguliwa kwa lengo la kupata data zitakazomuwezesha kukamilisha utafiti wake (Kothari, 2004; Babbie, 1992; Kothari, 1990) anashauri kuwa watoa taarifa wachache ni bora zaidi kwa ajili ya kujibu maswali ya utafiti. Hata hivyo Sigh (2007) anauelezea usampulishaji kuwa ni

mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Katika utafiti huu mtafiti kupitia mbinu ya usampulishaji lengwa na tabakishi jumla ya watoa taarifa 60 walitumika katika kupata data za utafiti huu wakiwemo wasomi wanye umri kati ya miaka 25 – 39 hii ni kutokana mtafiti anaamini kuwa wazungumzaji wa umri huu mara nyingi wameathiriwa na usasa na hivyo wanaweza kumpatia taarifa za kisasa zitumikazo baina ya lahaja husika, hata hivyo kundi la wazee wenye umri kati ya miaka 40 – 70 nalo lilitumika, hii ni kutokana na kwamba, wazungumzaji wa umri huu wana ujuzi mkubwa wa kuitumia lahaja husika kwavile bado hawajaathiriwa na usasa katika mazungumzo yao na hivyo ilimuezesha mtafiti kupata taarifa za ukweli na za kuaminika. Vile vile uteuzi huu umefanyika kutokana na mjengeko wa mada husika ulivyo ambao kwa kiasi fulani ulihitaji uelewa wa isimu ya lugha walau kwa uchache. Hata hivyo uteuzi huu mdogo wa watoa taarifa ulimuezesha mtafiti kuuliza maswali kwa ufanisi na kwa uwazi, kuepuka msongamano wa watoa taarifa pamoja na kuokoa muda katika uulizaji wa maswali yake yaliyompatia data zilizohusu utafiti wake. Uchanganuzi wa watoa taarifa hao ni kama unavyooneshwa katika jedwali na 3.1 hapo chini.

### **Jedwali Na.3.1: Watoa taarifa**

<b>Watoa Taarifa</b>	<b>KPJ</b>	<b>KMK</b>	<b>Jumla</b>
Wazee (40 hadi 70)	15	15	30
Wasomi (25 hadi 39)	15	15	30
<b>Jumla Kuu</b>			<b>60</b>

### **3.5.1 Sampuli Lengwa**

Ni aina ya sampuli ambayo huteuliwa na mtafiti ili kumpa data za utafiti kwa usahihi na kwa haraka zaidi. Imelazimika kuteuliwa mbinu hii kwasababu mtafiti alitumia muda mfupi na kwa gharama nafuu.

### **3.5.2 Sampuli Tabakishi**

Sampuli tabakishi ni aina ya sampuli ambayo huteuliwa na mtafiti kulingana na matabaka yaliyomo katika jamii, kama vile ya kielimu, mali, jinsia na rika. Sababu ya mtafiti kuteua njia hii ni kwamba ilimpa urahisi wa kuzipata data za viwango tofauti kutoka kwa watafitiwa wake kwavile wametofautiana kiviwango katika elimu, nyadhifa na hata rika zao.

## **3.6 Aina za Data**

Katika utafiti huu mtafiti alitumia data za aina mbili: data za upili na data za msingi kwa lengo la kufanikisha malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni kubainisha mfanano na utofauti wa kifonimu kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi, kulinganisha na kutofautisha kanuni za kimofofonolojia zinazotawala maumbo ya mofu zinazojenga maneno ya Kiswahili cha Paje na yale ya Makunduchi na mwisho ni kubainisha uwiano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Kimakunduchi.

### **3.6.1 Data za Msingi**

Data za msingi kwa kawaida huwa ni data ghafi ambazo zinakusanya kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake ya utafiti na huwa ni data ambazo hazijawahi kukusaywa na mtafiti mwingine yeoyote kwa minajili ya utafiti

kama huu (Kothari, 2008). Data hizi zilikusanywa masikanini ambako watafitiwa teule wanapatikana, ambao mtafiti aliamini kuwa wangempatia data muafaka zilizo msaidia kuyafikia malengo yake ya utafiti. Na mara nyingi data za aina hii hupatikana kupitia mbinu mbalimbali kama vile hojaji, ushuhudiaji, mbinu shirikishi, usaili nk.

### **3.7 Ukusanyaji wa Data**

Data zilikusanywa kulingana na utaratibu ambao ulipangwa na mtafiti. Mtafiti aliwasaili kwa njia ya vikundi, aliwapa karatasi za hojaji zenyе maswali mafupi pamoja na kuwashuhudia watafitiwa wake wakiwa maongezini huku akirekodi sauti za watafitiwa wakiwa katika maongezi yao katika muktadha ulio rasmi na ule usio rasmi. Samamba na hayo mtafiti alielekea maktaba mbalimbali na kuchambua kazi maalumu mbalimbali zilizokuwa zinaendana na tafiti hii.

### **3.8 Mbinu za Ukusanyaji wa Data**

Mbinu za kukusanya data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti. Utafiti huu ultumia mbinu za aina nne ambazo ni usaili, hojaji, ushuhudiaji na uchambuzi wa kazi maalumu. Mtafiti aliamua kutumia mbinu za aina nne kwa ajili ya kupata uthabiti wa matokeo ya utafiti.

#### **3.8.1 Mbinu ya Usaili**

Usaili ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu au barua pepe nk, yanayofanyika baina ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kutafiti linalo kusudiwa (Kombo na Tromp, 2006). Hata hivyo, Kothari (2004) amegawa aina mbili kuu za usaili ambazo ni usaili wa ana kwa ana na usaili

wa simu. Pamoja na aina hizo, mtafiti alitumia usaili wa ana kwa ana na ilitumika kwa watu wazima, ambapo mtafiti aliweza kuwahoji watafitiwa wake hao kwa mapana zaidi na kuweza kuondoa utata kwa urahisi pale ambapo watafitiwa wake wanaposhindwa kufahamu msingi wa swali husika. Vile vile kupitia mbinu hii ya usaili, mtafiti alitumia orodha ya msamiati wa Kiswahihili sanifu na kuwataka watafitiwa wake wampatie maana zitokanazo na msamiati huo zinazowakilishwa na jamii lugha husika, ili zimsaidie mtafiti kubaini mfanano na utofautiano wa kimaana uliopo baina ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi. Sambamba na hayo mtafiti ilimsaidia kupata taarifa zaidi na kwa undani kwa vile mtafiti alipata fursa ya kuuliza maswali mengine ya ziada. Hata hivyo mbinu hii ilikuwa na kasoro fulani kama vile mtafiti alikosa taarifa zilizohusu maandishi ili kubaini uwiano na utofautiano wao kimaandishi na kulazimika kuteuliwa kwa mbinu nyingine ili kupata taarifa za kimaandishi.

### **3.8.2 Mbinu ya Hojaji**

Hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambayo mtafiti huandika maswali na baadae huwapa watoa taarifa ili wajibu na kurudishiwa kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa (Kothari 2004). Hata hivyo, Kothari anaendelea kueleza kwamba mbinu hii hutoa fursa kwa mtafiti kumuuliza mtafitiwa maswali ya ana kwa ana ambayo pia humuwezesha kuona muonekano wa sura ya mtafitiwa pale anapojibu maswali aliyomuuliza. Naye Mosha (2004) anatueleza kwamba mbinu hii ina faida nyingi kama vile ya gharama nafuu na inatumia muda mchache. Hivyo mtafiti aliandaa na kuwapa maswali mafupi mafupi watafitiwa wake ambao ni wasomi kwa vile njia hii inahusiana na uandishi. Mbinu

hii ilitumika kukusanya data zilizohusu kanuni za kifonolojia na mofolojia zinazotawala maumbo ya mofu zinazojenga maneno ya Kiswahili cha Paje na yale ya Kimakunduchi. Data zilizopatikana kuititia mbinu hii zilifaa sana kujibu swali la pili la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha utofauti na mfanano uliopo kuhusu mifanyiko ya kimofofonolojia itumiwayo na kutawala maumbo ya mofu zinazounda maneno ya jamii lugha hizo. Kwa mantiki hiyo basi njia hii ilimsaidia sana mtafiti kwani ilimuwezesha kupata jawabu sahihi na za uhakika na kwa haraka zaidi. Licha ya kuwa mbinu hii ilimsaidia mtafiti kwa kiasi hicho lakini pia ilishindwa kumpatia kwa undani data zinazohusu fonolojia ili mtafiti awezekubaini uwiano na utofauti wa kifonimu baina ya jamii lugha hizo, na hapo ndipo mtafiti alipolazimika kuiteua mbinu ya ushuhudiaji.

### **3.8.3 Mbinu ya Ushuhudiaji**

Mtafiti alilazimika kufika maskanini mwa watoa taarifa na kushuhudia watafitiwa wakiwa maongezini katika muktadha rasmi na usio rasmi kama vile harusini, msibani, viwanjani, maskanini na hata bandarini, hivyo mtafiti ilimlazimu kutumia vifaa vya kunasia sauti vikiwemo simu za mkononi kwa lengo la kurekodi sauti za watafitiwa ili kupata data za kifonolojia na kimofolojia zilizomsaidia kubaini ufanano na utofautiano wa kifonimu baina ya jamii lugha husika. Halikadhalika ilimsaidia mtafiti kubaini michakato ya kimofofonolojia itumiwayo na wanajamii lugha hao katika kuyakokotoa maumbo ya maneno wakati wanapokuwa katika maongezi yao na kuweza kufanikiwa kuyafikia lengo la kwanza na lapili la utafiti huu.

### **3.8.4 Mbinu ya Maktaba / Uchambuzi wa Kazi Maalumu**

Mbinu hii inahusisha mapitio ya kazi mbalimbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia zenye kuhusiana na kazi husika, kazi hizo zaweza kuwa makala, vitabu, magazeti, majarida, tasnifu na nyaraka mbalimbali. Na zinaweza kuhusu nadharia mbalimbali au hata uchambuzi wa dhana zinazohusiana na mada ya utafiti husika kwa namna moja ama nyingine (Kothari, 1990). Hatahivyo Ewan na Calvet (2000) wanaeleza kuwa maktaba ni mahali maalumu palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida na magazeti yenyе taarifa mbalimbali kwa wasomaji na watafitiwa wa kanda tofauti tofauti za taaluma. Uteuzi wa mbinu hii ni kutokana na kuwa ilimsaidia mtafiti kupitia machapisho mbalimbali yenyе hadithi, taarifa za kidini na kijadi zenye matumizi ya lugha ya Kimakunduchi, vilevile ilimsaidia mtafiti kujifunza mengi yaliyomo kwenye kazi za wenzake pamoja na kuzidi kuangalia nadharia na mbinu nyengine ambazo zilihusiana na utafiti wake.

### **3.9 Mbinu za Kuchanganua Data**

Uchambuzi wa data ni kiungo muhimu katika kukamilisha utafiti uliolengwa kufanywa kwa namna moja au nyingine. Babbie (1999) anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo inawezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika. Naye Kothari (2008) anaeleza uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika utafiti ambayo husaidia kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Hivyo kuna mikabala miwili mikuu ambayo hutumika sana katika uchambuzi wa data za kiutafiti ambayo ni uchambuzi wa kimaelezo pamoja na uchambuzi wa kitakwimu. Enon (1998) anaelezea kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti

hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Sambamba na hayo mtafiti katika kuitumia mbinu hiyo wakati wa kuchambua data ameambatanisha na michoro ya majedwali alifanya hivi kutoptana na kuwa tatizo la utafiti wake linahusiana na ulinganishi wa Kiisumu na hivyo uchambuzi wa data za utafiti huu utahitaji ufanuzi zaidi wa kimaelezo kuliko kimahesabu. Hivyo mbinu hii ya maelezo ni muhimu sana kwa mtafiti kwani ilimuongoza vyema na kwa urahisi katika kuzichambua data zilizotokana na maswali ya utafiti huu pamoja na kufikia lengo kuu pamoja na malengo mahsus ambayo mtafiti alidhamiria kwadhati kabisa kuyafanyia kazi na kuyapatia ufumbuzi wa kina.

### **3.10 Muhtasari wa sura**

Sura hii imeonesha mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Mbinu hizo za utafiti zilizosaidia kufanikisha utafitihuu, zimeelezwa na kufafanuliwa namna zilivyotumika. Mbinu hizo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, pamoja na mbinu za kuchanganua data. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

## **SURA YA NNE**

### **UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA**

#### **4.0 Utangulizi**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza uwiano wa kiisimu kati ya Kiswahili kinachozungumzwa Paje na kile cha Makunduchi ili kuona ni kwa kiasi gani vinatofautiana na kufanana. Sura hii inawasilisha pamoja na kuzichakatua data mbalimbali zilizokusanywa uwandani kutoka maeneo yaliyoteuliwa wakati wa utafiti, pamoja na maktabani. Katika utekelezwaji wa kazi hii mtafiti aliongozwa na kiunzi cha nadharia ya isimu linganishi pamoja na mofofonolojia. Vigezo muhimu vilivyotumika kuongoza utafiti huu ni pamoja na msamiati wa lugha mbili ilikuthibitisha kuwa zina asili moja au laa, kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha, mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana na ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu wa kimofolojia. Vigezo hivyo ndivyo vilivyotumika katika kulinganisha utofauti na ufanano wa kifonimu, kanuni za kifonolojia na kimofolojia zinazotumika na kutawala maumbo ya mofu ziundazo maneno pamoja na msamiati wa msingi na maana zake kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

Data iliyokusanywa imewasilishwa na kuchambuliwa kwa misingi ya nadharia ya isimu linganishi pamoja na mofofonolojia. Mbinu ya uchambuzi linganishi ambayo hutumika kulinganisha data kutoka kwa jamii za watu tofauti iliteuliwa na kutumika katika utafiti huu kwa sababu ya uhalisia wa utafiti husika, ambao ulichunguza kwa kulinganisha fonimu, kanuni za kimofofonolojia na msamiati pamoja na maana zake kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi. Sura hii imegawika katika

sehemu kuu tatu kulingana na malengo na maswali ya utafiti husika. Sura ya kwanza inatoa maelezo kuhusu uwiano wa fonimu za kikonsonanti pamoja na fonimu za irabu, tofauti za matumizi ya kifonimu pamoja na kuonesha utofauti wa upachikaji na udondoshaji viyeyusho baina ya mfuatano wa irabu kati ya Kipaje na Kimakunduchi. Sehemu ya pili imejadili uwiano wa viambishi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya maneno, pamoja na kubainisha na kufanua kanuni zinazotawala na kuyakokotoa maumbo ya ndani kwenda ya nje katika kategoria za nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi pamoja na kuonesha kanuni ya ujumla iliyotumika katika ukokotozi husika. Sehemu ya tatu imejadili maneno yanayotofautiana na kulingana kimaumbo na kimaana, na kukasmilisha kwa muhtasari wa sura.

#### **4.1 Uwiano wa Fonimu za Konsonanti Kati ya Kimakunduchi na Kipaje**

Kulingana na lengo la kwanza pamoja na swali la kwanza la utafiti huu, kupitia mbinu za maktabani, ushuhudiaji pamoja na msamiati uliofanyiwa uchunguzi, mtafiti amefanikiwa kubaini kuwa kuna uwiano mkubwa katika mfumo wa sauti za konsonanti baina ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi, kupitia namna na jinsi ya kutamka na kwamba hautofautiani sana na mfumo wa sauti za Kiunguja. Hivyo kupitia data husika mtafiti amebaini kuwa Kiswahili cha Makunduchi kina jumla ya sauti za Konsonanti 23 ambazo ni: [b], [p], [p<sup>h</sup>], [t], [t<sup>h</sup>], [d], [tʃ<sup>h</sup>], [tʃ], [k], [k<sup>h</sup>], [g], [m], [n], [ŋ], [ɳ], [f], [v], [ʒ], [s], [z], [ʃ], [h], [l] pamoja na Viyeyusho viwili ambavyo ni [w], [j]. Hata hivyo Kiswahili cha Paje kina jumla ya sauti za Konsonanti 24 ambazo ni: [b], [p], [p<sup>h</sup>], [t], [t<sup>h</sup>], [d], [tʃ<sup>h</sup>], [tʃ], [k], [k<sup>h</sup>], [g], [m], [n], [ŋ], [ɳ], [f], [v], [ʒ], [s], [z], [ʃ], [h], [l], [r] pamoja na Viyeyusho viwili; [w] na [j]. Kama inavyojidhihirisha katika jedwali na 4.1 pamoja na 4.2 hapa chini.

**Jedwali. Na. 4.1 Sifa za Kimatamshi za Konsonanti na Nusu Irabu za Kimakunduchi**

Namna ya Utamkaji	Mahala pa Kutamkia						
		Midomo	Midomo meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaala ini	Glota
Vipasuo	Sighuna	P		T		K	
	Sigghuna mpumuo	p <sup>h</sup>		t <sup>h</sup>		k <sup>h</sup>	
	Ghuna	B		D		G	
Vizuiwa kwamizwa	Sighuna				tʃ		
	Sighuna mpumuo				tʃ <sup>h</sup>		
	Ghuna				j		
Vikwamizwa	Sighuna		F	S	ʃ		H
	Ghuna		V	Z			
Nazali	Ghuna	M		N	n	ṇ	
Vilainisho	Ghuna			L			
Viyeyusho					J	W	

**Jedwali. Na. 4.2 Sifa za Kimatamshi za Konsonanti na Nusu Irabu za Kipaje**

Namna ya Utamkaji	Mahala pa Kutamkia						
		Midomo	Midomo meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaala ini	Glota
Vipasuo	Sighuna	P		T		K	
	Sigghuna mpumuo	p <sup>h</sup>		t <sup>h</sup>		k <sup>h</sup>	
	Ghuna	B		D		G	
Vizuiwa kwamizwa	Sighuna				tʃ		
	Sighuna mpumuo				tʃ <sup>h</sup>		
	Ghuna				ɬ		
Vikwamizwa	Sighuna		F	S	ʃ		H
	Ghuna		V	Z			
Nazali	Ghuna	M		N	n	ṇ	
Vilainisho	Ghuna			L			
Vimadende	Ghuna			R			
Viyeyusho					J	W	


Kupitia majedwali Na. 4.1 na 4.2 hapo juu, yanaonesha ufanuzi kuwa kupidia namna na mahala pa kutamkia Kiswahili cha Makunduchi kina jumla ya fonimu za Konsonanti 23 na viyeyusho 2 ilihali Kiswahili cha Paje kina fonimu za Konsonanti 24 na viyeyusho 2. Utotauti uliopo ni kwamba Kimakunduchi kina miliki idadi ndogo ya fonimu za konsonanti kikilinganishwa na Kipaje. Kwa vile Kipaje kina sifa ya kumiliki kitamkwa cha umadende [r] ambacho hakipatikani katika wazungumzaji wa Kimakunduchi na badala yake wao hutumia sauti ya kitambaza /l/ katika maumbo yote yanayoambatana na sauti ya kimadende /r/, tafauti hii inatokana na kuwa kila lugha na jamii lugha huchagua sauti izipendazo kutoka katika bohari kuu la sauti, vile vle Kipaje kuathiriwa sana na Kiswahili sanifu pamoja na uwepo wa muachano wa Kijiografia uliopo baina ya jamii lugha mbili hizi. Sambamba na hayo mtafiti amebaini ya kuwa kati ya Kipaje na Kimakunduchi vinalingana kwa kiasi fulani kwa vile vyote havina sifa ya umiliki wa sauti zenye asili ya Uarabu ambazo zimekopwa na kutumika katika Kiswahili sanifu sauti hizo ni kama vile [χ] [ð] na [Ø]. Sambamba na hayo taarifa hizi zinakubaliana na nadharia ya isimu linganishi pamoja na nadharia ya mofonolojia kwa vile nadharia zote kwa umoja wao hulenga kuchunguza ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu wa Kimofolojia pamoja na kuangalia mabadiliko ambayo huleta utotauti katika lugha kupidia ngazi ya kimsamiati. Hata hivyo taarifa za utafiti huu zinakubaliana na tafiti ya, Mulwa (2014) ambaye alichunguza fonolojia ya Nomino – mkopo za Kikamba kutoka Kiswahili, katika kazi yake hiyo amebaini ya kuwa Kikamba cha Kitui ya kati kina jumla ya sauti za konsonanti 19 na anatueleza yakuwa konsonanti hizo huweza kuainishwa kwa kuzingatia jinsi ya kutamka na mahala pa kutamkia, kwa kuzingatia jinsi ya kutamka anaeleza kuwa tunapata vipasuo, vipasuo nazalishi, vikwamizi,

vikwamizo nazalishi, nazali, vilainisho na viyeyusho na kwa kuzingatia mahala pa kutamkia tunapata sauti za konsonanti za meno, konsonanti za midomo, konsonanti za ufizi, kaakaa gumu na konsonanti za kaakaa laini, vile vilw amebainisha kuwa konsonanti za Kikamba zina maumbo mawili umbo sahili ambalo huwakilishwa kwa herufi moja katika tahajia na unukuzi wa kifonetiki akitolea mfano sauti /t/ na /s/ na kwa upande wa umbo changamani amefafanua kuwa konsonanti hizi huwakilishwa na fungu la sauti mbili kama vile /mb/. Naye Matinde (2012) akilishadidia hilo anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ina jumla ya konsonanti 24 ambazo hugawika katika makundi sita ambayo; Vipasuo au Vizuiwa hujumuisha sauti za /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ na /g/, Vizuiwa kwamizwa hujumuisha /ʃ/ na /ʒ/, Kitambaza /l/, Kimadende /r/, Nazali au Ving'ong'o /m/, /n/, /ŋ/, /ɳ/ na Vikwaruzo au Vikwamizwa /f/, /v/, /θ/, /ð/, /ʃ/, /z/, /s/, /x/, /h/ na /x/.

Kwa ujumla ni kwamba kila lugha ina idadi yake ya sauti za konsonanti ambazo huweza kuifananisha ama kuitofautisha na lugha nyingine kama ilivyo kwa Kipaje na Kimakunduchi.


#### **4.1.1 Uwiano wa Fonimu za Irabu Kati ya Kimakunduchi na Kipaje**

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya isimu linganishi pamoja na mbinu za usaili, mahojiano na ushuhudiaji, alibaini kuwa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi vinatofautiana katika mfumo wa irabu kupitia watafitiwa. Mtafiti alibaini kuwa Kipaje kina jumla ya irabu tano (5) ambazo zote zimo katika mfumo wa irabu fupi, ilihali Kimakunduchi kina jumla ya irabu kumi zikiwemo fupi na ndefu kama chati na. 4.1 na 4.2 yanavyodhihirisha ukweli huo hapa chini.



#### **Chati Na. 4.1 Mfumo wa Irabu fupi katika Kipaje na Kimakunduchi**

Chati hili linaonesha uwiano wa fonimu za irabu fupi ambazo zinapatikana baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi ambazo zinatumika katika uundaji wa maneno ambayo hutumiwa na jamii zote mbili katika miktadha tofauti ya kimawasiliano.



#### **Chati Na. 4.2 Mfumo wa Irabu Ndefu za Kimakunduchi:-**

Chati na. 4.2 hapo juu linaonesha mfumo wa irabu ndefu za Kimakunduchi zitumikazo kuundia maneno ambayo hutamkwa kwa kutumia wakaa mrefu ambaa huleta utofauti wa maana, mfano maneno kama /ta:/ (hapana), /nchokoto:/ (nimechokamno) na /ngojaga:/ (ngoeja) ambapo katika maneno haya irabu /a/, /o/ ndio irabu zilizorefushwa.

Hata hivyo irabu ndefu za Kimakunduchi huwa na sifa maalumu za kimatamshi ambapo sifa ya juu inapatikana katika irabu /i:/ na /u:/, sifa ya uchini inajitokeza katika irabu /a:/, sifa ya unyuma pamoja na uviringo zinapatikana katika irabu /ɔ:/

na /u:/ , hata hivyo sifa ya urefu inachangiwa na irabu zote /a:/, /ɛ:/, /i:/, /ɔ:/ na /u:/ kama data zinavyolidhihirisha hilo katika Jedwali Na. 4.3 hapa chini

#### **Jedwali Na 4.3 Matriki ya Irabu Ndefu za Kimakunduchi.**

Irabu	/a/		/a:/	/ɛ/	/ɛ:/	/i/	/i:/	/ɔ/	/ɔ:/	/u/	/u:/
Juu	-		-	-	-	+	+	-	-	+	+
Chini	+		+	-	-	-	-	-	-	-	-
Nyuma	-		-	-	-	-	-	+	+	+	+
Mviringo	-		-	-	-	-	-	+	+	+	+
Urefu	-		+	-	+	-	+	-	+	-	+

Data hizi zilizokusanywa kutoka uwandani zinadhihirisha wazi kuwa Kipaje na Kimakunduchi vinatofautiana katika mfumo wa irabu kwani mtafiti amebaini kuwa Kipaje kina jumla ya irabu tano (5) zikiwa zote ni [a], [ɛ], [i], [ɔ] na [u], ilihali Kimakunduchi kina irabu kumi (10) zikiwemo tano fupi na tano ndefu ambazo hutumika katika mfumo wa mawasiliano pamoja na uundaji wa maneno ya Kimakunduchi irabu hizo ni [a], [ɛ], [i], [ɔ], [u], [a:], [ɛ:], [i:], [ɔ:] [u:]. Tofauti hizo za mfumo wa irabu baina Kipaje na Kimakunduchi zinatokana muachano wa Kijigrafia uliopo baina ya jamii lugha mbili hizi. Pamoja na hayo taarifa hizi zinakubaliana na nadharia ya mofonolojia, ambayo inajikita na uchunguzi wa kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana pamoja na kuangalia ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu kimofolojia ambapo mtafiti imemuongozo kubaini mifumo ya irabu za jamii lugha mbili hizi na uamilifu wake katika lugha. Hata hivyo taarifa za utafiti huu zinakubaliana na taarifa za tafiti ya Mulwa (2014) ambapo anaeleza kuwa Kikamba kina jumla ya vokali saba (7) ambazo ni /a/, /ɛ/, /e/, /i/, /ɔ/, /o/ na /u/. Akiendelea kusitiza kuwa vokali hizi huainishwa kwa kutumia taratibu za mlalo wa ulimi ambao unatupatia vokali za kati,

mbele na za nyuma. Na kutegemea mwinuko wa ulimi tunapata irabu za juu, za kati – juu, kati – chini na za chini, vile vile anaeleza kuwa Kikamba kina wakaa mrefu akitoa mfano wa maneno *uka* [oka] (njoo) na *uuka* [o:ka] (pata wazimu) ambapo urefushaji huu wa vokali /o/ huleta tofauti za kimaana. Ingawa tunaungana na Mulwa (ameshatajwa) katika miktadha hiyo lakini ameshindwa kuonesha ni sababu zipi hasa zinazochangia Kikamba kuwa na irabu zenye wakaa mrefu, hivyo mtafiti anahisi suala hili husababishwa na michakato ya kimofofonolojia katika utamkaji wa maumbo ya maneno, hata hivyo uainishaji wa irabu kufuatia mwinuko wa ulimi hutupatia irabu za juu, za nusu juu, za nusu chini na irabu za chini. Kwa ujumla kila lugha ina mfumo wake wa irabu ambao huitofautisha lugha moja na nyngine.

#### **4.1.2 Tofauti za Matumizi ya Sauti Baina Kipaje na Kimakunduchi**

Kuna tofauti za kimatumshi kati ya Kipaje na Kimakunduchi Kusini Unguja, ambazo hutokana na mpishano wa sauti. Tofauti hizo zinajitokeza zaidi katika sauti za Konsonanti na nusu irabu. Tofauti hizo huyafanya maneno fulani yenye maana sawa au yaliyokaribiana au yaliyotofautiana kimaana yatofautiane katika sehemu fulani tu ya sauti.

#### **4.1.3 Tofauti za Mpishano Huru wa Fonimu [l] na [r]**

Mtafiti baada ya kufika maskanini, kupitia mbini ya ushuhudiaji wa mazungumzo ya watafitiwa wake kupitia miktadha tofauti ilyo rasmi na isiyo rasmi, mtafiti alibaini kuwa baina ya jamii ya wasemaji wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kuna tofauti za kimatumizi kati ya sauti [l] na [r], kwani Wapaje wao hutumia sauti [r] katika mazingira ambamo hutumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu, ilihali Wamakunduchi wao hutumia sauti [l] mahala ambapo Kiswahili sanifu hutumia

sauti [r] kama ambavyo data ya utafiti huu inavyoonesha katika jedwali Na. 4.4 hapo chini

**Jedwali Na 4.4: Utarfauti wa Kimatumizi wa Fonimu {r/l} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KMK	KPJ	TOFAUTI	KISW
Sh <u>u</u> lufu	Sh <u>u</u> rufu	1 / r	Shurufu
Su <u>l</u> uali	Su <u>l</u> uali	1 / r	Suruali
Ko <u>l</u> wa	Ko <u>l</u> wa	1 / r	Korwa

Kupitia mifano ya data za uwandani za utafiti huu hapo juu imedhihirika wazi kuwa wazungumzaji wa jamii ya Kimakunduchi huitumia sauti [l], ambacho ni kilainisho / kitambaza cha ufizi mahala ambapo wazungumzaji wa jamii ya Wapaje huitumia sauti ya kimadende [r] kama inavyotumika katika Kiswahili sanifu, ambapo hupelekea maumbo ya maneno yanayo zalisthwa na jamii lugha mbili hizi kuwa na idadi sawa ya sauti na kuwakilisha maana zilizo sawa kwa jamii zote, lakini hutarfautiana kimofolojia kupitia sauti moja tu. Tafauti hii inatokana na muachano wa kijiografia uliopo baina ya jamii lugha mbili hizi, pamoja na sababu za kiisumu ambapo kila jamii lugha huchagua sauti izipendazo toka bohari kuu la sauti. Hata hivyo taarifa hizi zinakubaliana na nadharia ya mofonolojia kwani nadharia hii hujikita na uchunguzaji wa ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu wa kimofolojia, hivyo imemuongoza vyema mtafiti katika kubaini Kipaje na Kimakunduchi namna vinavyo badilishana na kutarfautiana kimatumizi baina ya sauti {1/ r}. Vile vile taarifa hizi zinakubaliana na taarifa za tafiti linganishi ya Bakari (2015) ambapo alilinganisha baina ya Kipemba na Kitumbatu na ana eleza kuwa kuna utarfauti wa kimatumizi wa sauti {1 na r} baina ya jamii lugha mbili hizi

ambapo Kipemba hutumia sauti /r/ mahala ambapo Kitumbatu hutumia sauti ya kilainisho /l/, hata hivyo mabadiliko ya sauti hizi baina ya jamii lugha mbili hizi hayabadilishi maana ya maneno. Licha ya kuwa tunakubaliana na Bakari (ameshatajwa), lakini pia hakuonesha mambo yanayochangia uwepo wa utofauti huo kimatumizi, bali mtafiti anaona kuwa jambo hili hutokana na sababu za kijiografia kwa vile Tumbatu na Pemba ni visiwa vilivytenganishwa na bahari.

#### **4.1.4 Tofauti za Mpishano Huru wa Fonimu [v] na [p]**

Kupitia mbinu za mahojiano, usaili na ushuhudiaji wa zungumzo ya wazungumzaji, mtafiti alibaini kuwa katika baadhi ya maneno kati ya wazungumzaji wa Kiswahili cha Paje na Makunduchi kuna tofauti za kifonimu katika matamshi ya maneno yao wanayoyatumia katika mawasiliano yao. Mtafiti alibaini kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi katika utamkaji wa maneno yenye sauti ya kipasuo hafifu cha midomo [p] hukibadili kitamkwa hicho na kutumia sauti ya kikwamizi cha mdomo meno [v], ilihali wazungumzaji wa Kipaje hutumia kipasuo hafifu cha midomo [p] katika mazingira hayo hayo kama ambavyo wazungumzaji wa Kiswahili sanifu wanavyokitumia kama ambavyo mifano ya data za uwandani inavyolidhihirisha hilo katika Jedwali Na. 4.5 hapa chini:

#### **Jedwali Na 4.5 Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {v/p} Kati ya Kipaje na**

##### **Kimakunduchi**

KMK	KPJ	TOFAUTI	KISW
Anavika	Anapika	V / p	Anapika
Wanavita	Wanapita	V / p	Wanapita
Vaka rangi	paka rangi	V / p	paka rangi
Tuwavo	Tupo	V / p	Tupo

Mifano kutoka Jedwali Na. 4.5 hapo juu inadhihirisha wazi kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hukibadilisha kitamkwa cha kipasuo nje hafifu cha midomo [p] kinapokuwa katika maumbo ya vitenzi pamoja na vivumishi katika mazingira ya kufuatiwa na irabu ya juu mbele /i/, kati mbele na nyuma /e/ na /o/ pamoja na irabu ya chini /a/, katika mazingira hayo wazungumzaji hao hulazimika kukibadili kipasuo hicho na badala yake kutumia sauti ya kikwamizwa ghuna cha midomo meno /v/ katika mazingira ambayo jamii ya wazungumzaji wa Kipaje hutumia sauti ya kipasuo nje hafifu cha midomo [p] kama kitumikavyo katika Kiswahili sanifu, hata hivyo tofauti hizo za kifonimu hazzoneshi utofauti wa kimaana kwa jamii zote mbili, vile vile tofauti hii inatokana na kuwa Kipaje kuathiriwa sana na Kiswahili sanifu kikilinganishwa na Kimakunduchi. Kwa mantiki hiyo taarifa hizi zinakubaliana na nadharia tumizi ya mofonolojia, ambayo mtafiti ameitumia kwa vile nadharia hii inachunguza ubadilishanaji wa sauti ambao utakua na uamilifu wa kimofolojia kama ambavyo mtafiti alivyo baini katika Kimakunduchi ambacho hukibadili kipasuo hafifu cha midomo [p] na kutumia kikwamizwa ghuna cha midomo meno [v] ambacho kiliendelea kubeba uamilifu wa kimofolojia. Kwa kulishadidia hili Kipacha (2003) anaeleza kuwa tafauti za kiisimu zinajitokeza katika kila tabaka, akitolea mifano huko Tamil, anasema kuwa kuna mgawanyo wa waziwazi katika fonolojia, msamiati na sarufi ya “Brahmin” na wale wasio wa Brahmin. Kwa ujumla ni kwamba jamii lugha moja hutofautiana na nyingine katika matumizi ya kifonimu kama ilivyo kwa Kimakunduchi na Kipaje kuptia sauti {p/v}

#### **4.1.5 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti [ly] na [l]**

Kupitia mbinu za usaili, mahojiano pamoja na ushuhudiaji wa maongezi ya watafitiwa, mtafiti aliweza kubaini kuwa kuna utofauti mkubwa wa kimatumizi kati ya sauti [ly] na [l] baina ya Kipaje na Kimakunduchi. Mtafiti kwa kupitia watafitiwa husika, aligundua kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hutumia sauti [ly] mahala ambapo wazungumzaji wa Kipaje na Kiswahili sanifu hutumia sauti [l], kama mifano kupitia Jedwali Na. 4.6 linavyoonesha hapa chini.

#### **Jedwali Na 4.6: Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {ly/l} kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KMK	KPJ	TOFAUTI	KISW
Kulya	Kula	ly / l	Kula
Lyangu	Langu	ly / l	Langu
Lyenu	Lenu	ly / l	Lenu
Lyako	Lako	ly / l	Lako
Lyolyote	Lolote	ly / l	Lolote
Lilya	Lile	ly / l	Lile
Lilyolyo	Hilohilo	ly / l	Hilohilo
Linalyotendeka	Linalotendeka	ly / l	Linalofanyika
Vyakulya	Vyakula	ly / l	Vyakula

Data za hapo juu zinadhihirisha wazi kuwa kuna utofauti wa kimatumizi kati ya sauti {ly / l}, kwani wazungumzaji wa Kimakunduchi hutumia sauti [ly] ambapo huichanganya sauti ya kitambaza [l] na kiyeyusho [j] na kuunda sauti moja [ly] itokanayo na vitamkwa viwili badala ya [l] pekee katika maneno ambayo wazungumzaji wa Kipaje hutumia sauti [l] pekee kama sauti hiyo inavyotumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu. Tofauti hii inatokana na kanuni ya uyeyushaji na

udondoshaji wa vitamkwa, mtafiti amebaini kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi wameathiriwa na mchakato wa uyeyushaji wakati irabu ya juu mbele [i] inapo tanguliwa na sauti ya kitambaza [l] kisha kufuatiwa na irabu isiyofanana nayo kisifa katika umbo la ndani la neno hivyo wakati wa kuyapeleka nje irabu hiyo hubadilika na kupokea sura ya kiyesho [j] na kusababisha kiyeyusho hicho [j] kuungana na kitambaza [l] na kuunda fungu moja la sauti[ly] ilihali jamii ya wazungumzaji wa Kipaje huidondosha irabu ya juu mbele [i] ambayo imo katika umbo la ndani wakati wa kilipeleka neno husika katika umbo la nje. Data ambazo zinakwenda sambamba na nadharia ya mofofonolojia ambayo inalenga kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapo ungana pamoja na kuangalia ubadilishanaji wa sauti wenye kuleta uamilifu wa kimofolojia kama ambavyo mtafiti alivyo baini mabadiliko ya [i] kuwa [j] na kuunda [ly] katika Kimakunduchi, halikadhalika katika Kipaje huidondosha irabu [i] katika umbo la nje. Hata hivyo data hizi zinakubaliana na taarifa za Bakari (2015) ambaye alibaini kuwa wazungumzaji wa Kipemba hutumia na kutamka sauti [l] pekee kama itumikavyo katika Kiswahili sanifu ilihali wazungumzaji wa Kitumbatu hutumia na kutamka sauti [l] huku wakiichanganya na sauti ya kiyeyusho [j] na kuunda fungu moja la sauti [ly] kama ilivyo kwa Kimakunduchi na Kipaje.

#### **4.1.6 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti [fw] na [f]**

Mbinu ya ushuhudiaji kuititia kurekodi sauti na maongezi ya watafitiwa, mtafiti aliweza kubaini utofauti wa kimatumizi kati ya sauti [fw] na [f] uliopo baina ya wazungumzaji wa Kipaje na wale wa Kimakunduchi kwa baadhi ya maneno. Kwa kuititia data za uwandani mtafiti aligundua kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi

katika maongezi yao hutumia kundi la sauti [fw] na kuwa kama sauti moja katika mazingira ambayo wazungumzaji wa Kipaje hutumia sauti [f] kama ambavyo sauti hiyo inavyotumika katika Kiswahili sanifu. Data za uwandani zilizomo katika Jedwali Na. 4.7 zinalithibitisha hilo.

**Jedwali Na 4.7: Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {fw/f} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KMK	KPJ	TOFAUTI	KISW	TAF
Fwa	Kufa	fw / f	Kufa	Kuaga dunia
Mufwana	Mfana	fw / f	Mumependeza	Kupendeza
Ifwana	Ifana	fw / f	Imefana	Imechangamka

Data hizo hapo juu zinadhihirisha wazi kuwa kati ya Kimakunduchi na Kipaje kuna tofauti za kimatumizi kati ya sauti /fw/ na /f/. Kimakunduchi kimebainika kuwa katika baadhi ya maneno yake, sauti ya kikwamizi cha mdomo meno /f/ huchanganywa na sauti ya kiyeyusho cha midomo /w/ na kuunda fungu moja la sauti moja na kutumika sauti hiyo katika mazingira ambayo Kipaje na Kiswahili sanifu hutumia sauti moja tu ya kikwamizi cha mdomo meno /f/ pasi na kuandamana na kiyeyusho cha midomo /w/. Tofauti hii inatokana na kanuni za uyeyushaji kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi na kanuni ya udondoshaji kwa wazungumzaji wa Kipaje, ambapo wazungumzaji wa Kimakunduchi hulazimika kuiyeyusha irabu ya juu nyuma [u] na kuwa kiyeyusho cha midomo [w] katika mazingira ya kutanguliwa na sauti ya kikwamizwa hafifu cha midomo meno [f] na kisha kufuatiwa na irabu zinazotofautiana nayo kisifa wakati wa kulitoa umbo la ndani kwenda la nje, ilihali wazungumzaji wa Kipaje hulazimika kiudondosha irabu ya juu nyuma [u] katika mpaka wa mofimu moja wakati wa kuyapeleka nje maumbo ya maneno katika

maongezi yao. Pamoja na hayo taarifa hizi zinaenda sambamba na nadharia ya mofofonolojia ambayo hujishuhulisha na uchunguzi wa mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana na hivyo imemuongoza vyema mtafiti katika kubaini mabadiliko ya irabu ya juu nyuma [u] na kuwa kiyeyusho cha midomo [w] kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi halikadhalika kubaini badidiliko la udondoshwaji wa irabu ya juu nyuma [u] ikiwa katika mfuatano wa irabu mbili kwa wazungumzaji wa Kipaje. Hata hivyo Bakari (2015) katika tafiti yake iliyofanya ulinganishi kati ya Kipemba na Kitumbatu, ameeleza kuwa wazungumzaji wa Kipemba hujitofautisha kwa kutumia [sh] katika maneno kama [moshi] na [mpishi] ilihali wazungumzaji wa Kitumbatu hutumia sauti[s] pekee katika maneno hayo hayo kama [mosi] na [mpisi]. Kwa ujumla kila lugha huwa na utaratibu wake wa mpangilio wa vitamkwa vyake na namna ya kuvitumia vitamkwa hivyo kama ilivyo kwa Kimakunduchi na Kipaje.

#### **4.1.7 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti {vw /v}**

Mtafiti kupitia mbinu za hojaji na ushududiaji wa maongezi ya watafitiwa katika muktadha rasmi na usio rasmi, alibaini kuwa kunatofauti za kimatumizi kati ya sauti /vw/ na /v/, kwa vile jamii ya Kimakunduchi hukichanganya kitamkwa cha kikwamizi cha mdomo meno /v/ na kiyeyusho cha midomo /w/ na kuunda fungu moja la sauti /vw/ na hutumika fungu hilo la sauti katika mazingira ambayo jamii ya Kipaje hutumia sauti /v/ pekee kama itumikavyo katika mazingira ya Kiswahili sanifu. Mifano ya data katika Jedwali Na. 4.8 inadhihirisha hilo.

**Jedwali Na 4.8 Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu {vw/v} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KMK	KPJ	TOFAUTI	KISW	TAF
Vwaa	Vaa	vw/ v	Vaa	Kujivalisha kitu
Uvwi	Uvi	vw / v	Uvi	Mdudu
Vimekwivwa	Vimewiva	vw/ v	Vimewiva	Kuwiva chakula

Data hizi zinadhihirisha pamoja na kufafanua kuwa Kimakunduchi kinautaratibu wa kuzikutanisha sauti ya kikwamizi cha mdomo meno /v/ na kiyeyusho cha midomo /w/ na kuwa kama fungu moja la sauti /vw/ na kutumika sauti hiyo katika mazingira ambayo jamii ya Wapaje hutumia sauti /v/ pekee kama itumikavyo katika Kiswahili sanifu. Tofauti hii inatokana na kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hufanya mchakato wa uyeyushaji wa irabu ya juu nyuma [u] pale inapotanguliwa na sauti ya kikwamizi cha mdomo meno [v] na kisha kufuatiwa na irabu isiyofanana nayo katika umbo la ndani la neno, hivyo irabu hii hupokea sura ya kiyeyusho cha midomo [w] wakati wa kuyapeleka nje maumbo hayo, ilihali wazungumzaji wa Kipaje hulazimika kuidondosha irabu hiyo katika mazingira ya kutanguliwa na kikwamizi cha midomo meno [v] na kufuatiwa na irabu nyingine isiyofanana nayo kisifa. Data hii inakubaliana pamoja na kwenda sambamba na nadharia ya mofonolojia ambayo hujikita na uchunguzi wa mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana, hivyo imemuongoza mtafiti katika kubaini mabadiliko yanayosababishwa na kanuni za uyeyushaji pamoja na udondoshaji ambazo zimechangia utokeaji wa utofauti baina ya Kimakunduchi na Kipaje.

#### **4.1.8 Tofauti za Kimatumizi Kati ya Sauti {pj/t}**

Kupitia mbinu ya mahojiano pamoja na ushuhudiaji kwa kurekodi sauti na maongezi ya watafitiwa, mtafiti alibaini kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hutumia sauti /pj/ katika kuwakilisha sauti ya kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kimatamshi katika baadhi ya maneno, ilihali jamii ya Kipaje hukitamka na kukitumia kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kama kinavyotamkwa na kutumika katika Kiswahili sanifu. Kama inavyooneshwa na Jedwali Na: 4.9 hapo chini..

#### **Jedwali Na 4.9 Tofauti ya Kimatumizi ya Fonimu pj/t Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>TOFAUTI</b>	<b>KISW</b>
Zopya	Zote	pj / t	Zote
Yopya	Yote	pj / t	Yote
Sopya	Sote	pj / t	Sote
Nyopya	Nyote	pj / t	Nyote
Vyopya	Vyote	pj / t	Vyote

Data za uwandani hapo juu zinadhahirisha wazi kuwa Kimakunduchi hukichanganya kipasuo hafifu cha midomo /p/ na kiyeyusho cha kaakaa gumu /j/ kuwakilisha kipasuo hafifu cha ufizi /t/ katika baadhi ya maneno na kutamkwa /pj/ na kutumika katika mazingira ambayo jamii ya Kipaje hutumia sauti ya kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kama kitumikavyo katika Kiswahili sanifu. Tofauti hizi zinachangiwa na muachano wa kijiografia uliopo baina ya jamii lugha mbili hizi, hata hivyo data hizi zinakubaliana na nadharia ya mofonolojia ambayo huchunguza ubadilishanaji wa sauti ambaou utakua na uamilifu wa kimofolojia katika lugha ambapo mtafiti amefanikiwa

kuyabaini mabadiliko ya kipasuo hafifu cha ufizi [t] kuwa [py] katika maongezi ya wazungumzaji wa Kimakunduchi.

#### **4.2 Uwiano wa Michakato na Kanuni za Kifonolojia na Mofolojia Bainya Kipaje na Kimakunduchi**

Sehemu hii inahusiana na lengo la pili pamoja na kulijibu swali la pili la utafiti huu yanayohusu jinsi michakato ya kikanuni za kifonolojia na kimofolojia inavyotawala ukokotoaji wa maumbo ya ndani ya maneno na kuyaleta nje baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kama inavyooneshwaa hapa chini.


##### **4.2.1 Uwiano Katika Udondoshaji Irabu [i]**

Udondoshaji ni mfanyiko unaohusishwa sana na muundo mwafaka wa silabi (Schane, 1973). Wazungumzaji wa Kimakunduchi na wale wa Kipaje hufanana katika hali ya kudondosha irabu [i] wakati wa kuyakokotoa maumbo ya ndani na kuyaleta nje. Hali hii hutokea wakati ambapo irabu ya juu mbele [i] ikiwa imetanguliwa na sauti ya konsonanti ya nazali ya ufizi [n] katika mofu ya kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja na kisha kufuatiwa na konsonanti nyengine kama mifano katika Jedwali Na. 4.10 hapo chini

##### **Jedwali Na. 4.10 Uwiano Katika Udondoshaji Irabu ya Juu Mbele [i] Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>KISW</b>
Nfiki	Nfiki	Nimefika
Nlya	Nla	Nimekula
N'gu	n'gu	Nimeanguka

Kanuni ya ujumla



Kupitia data hizi za uwandani, kanuni hii ya ujumla inafafanua kuwa kati ya jamii ya Wapaje na Wamakunduchi zina sifa zinazowiana katika udondoshaji wa irabu ya juu mbele [i] katika mazingira ya kutanguliwa na sauti ya konsonanti ya nazali ya ufizi /n/ katika kukiwakilisha kiambishi nafsi ya kwanza umoja [ni]


Pia katika jamii ya Wapaje na Wamakunduchi hali ya udondoshaji wa irabu ya juu [i] hujitokeza mara chache na kwa maneno machache irabu hii hudondoshwa katika lahaja zote mbili iwapo na iwapo tu irabu hiyo itakuwa mwanzoni mwa kitenzi husika kama mifano katika Jedwali Na. 4.11 hapo chini inavyoonesha.

#### **Jedwali Na 4.11 Uwiano Katika Udondoshaji Irabu ya Juu Mbele [i] Ikiwa**

##### **Mwanzoni Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KMK	KPJ	KISW
Ngia	Ngia	Ingia
Ngieni	Ngieni	Ingieni

Kanuni ya ujumla



Kanuni hii inadhihirisha wazi kuwa kati ya wazungumzaji wa Kipaje na Kimakunduchi huwiana katika udondoshaji wa sauti ya irabu juu mbele [i] pale inapokuwa mwanzoni mwa kitenzi husika katika mazingira ya kufuatiwa na sauti ya nazali ya kaakaalaini katika umbo kitenzi husika. Taarifa hizi zinaenda sambamba na nadharia ya mofonolojia ambayo inajikita na maumbo ya mofimu katika lugha pamoja na kuangalia mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana kama ambavyo imejitokeza katika Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi. Massamba (2011) analithibitisha hili huku akitueleza kuwa udondoshaji mwanzo hujitokeza katika baadhi ya lugha ambapo sauti au silabi zinazotokea mwanzoni hudondoshwa akitoa mfano toka lugha ya Kingereza kama

<i>[ I am going ]</i>	linaweza kuwa	<i>[ I'm going ]</i>	“ninakwenda”
<i>[ I have no money ]</i>	linaweza kuwa	<i>[ I've no money ]</i>	“sina pesa”

Katika mifano ya Kingereza aliyotoa tunaona kwamba katika neno “am” sauti ya kwanza inadondoshwa na kubaki sauti [m] ambayo huunganishwa na sauti [I] na kuwa “I'm” hata hivyo [I] na [m] zimetanganishwa na kidogo kwa alama ya mkatojuu kuonesha kwamba hayo ni maneno mawili tofauti. Vile vile tunaona neno “have” sauti mbili za mwanzo [h] na [a] zimedondoshwa hivyo tunapata “I've” kama maneno mawili yaliyotenganishwa alama ya mkato juu. Kwa ujumla ni kwamba udondoshaji wa vitamkwa mwanzoni ni suala ambalo linajitokeza katika lugha nyingi ulimwenguni kama ilivyo kwa Kipaje na Kimakunduchi.

#### **4.2.2 Uwiano Katika Udondoshaji Nazali {m / n}**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji na mahojiano mtafiti alibaini kuwa jamii ya Wapaje na Wamakunduchi wanashabihiana katika udondoshaji wa nazali m/n na kuyafanya


maumbo ya maneno ya Kiswahili kukokotolewa kutoka umbo la ndani kwenda la nje na kupokea sifa ya kudondoshwa kwa sauti hizo za nazali katika baadhi ya maneno yanayotumiwa na jamii hizo kama data zilizokusanywa kutoka uwandani zinavyoonesha katika Jedwali Na. 4.12 hapa chini.

**Jedwali Na 4.12 Uwiano Katika Udondoshaji Nazali {m/n} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

KISW	KMK	KPJ
Jamvi	Javi	Javi
Anza	Aza	Aza
Chumvi	Chuvi	Chuvi
Mjenzi	Mjezi	Mjezi
Ujenzi	Ujezi	Ujezi
Chenza	Cheza	Cheza

Data hizi zinaonesha wazi kuwa lahaja za Kipaje na Kimakunduchi zina sifa ya kudondosha sauti za nazali m/n pale ambapo sauti hizo zinapofuatiwa na sauti ya kizuiwa kwamizi cha mdomo meno [v] na kizuiwa kwamizi cha ufizi [z] kama kanuni ya ujumla inavyo fafanua hapa chini:-

### Kanuni ya jumla



Kanuni hii inafafanua kuwa katika jamii ya wazungumzaji wa Kipaje na Kimakunduchi nazali m/n hulazimika kudondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na sauti za kikwamizwa cha midomo meno [v] na kile cha ufizi [z]. Matinde (2012) anaeleza kuwa udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio Fulani cha kiisimu katika silabi au neno, hali hii hutokana na sauti moja kuathiri nyingine hivyo ni kwamba ili neno lifuate muundo unaokubalika katika lugha husika, sauti moja hulazimika kuachwa au hudondoshwa. Tunakubaliana na mawazo ya Matinde (amshatajwa) ya kwamba ili muundo wa neno usomeke vizuri kwa kufuata sheria za lugha husika shariti sauti moja ilazimike kuachwa au kudondoshwa kama zilivyobainika nazali {m/n} kati ya Kiswahili cha Paje na kile Makunduchi, hata hivyo uchambuzi wa taarifa hizi unakubaliana na nadharia ya mofonolojia ambayo hushuhulika na mabadiliko ya sauti ambayo yatakua na uamilifu wa kimofolojia kama ambavyo mtafiti alivyo baini mabadili ya nazali m/n kati ya Kipaje na Kimakunduch.


#### **4.2.3 Tofauti Katika Udondoshaji Nazali {m /n}**

Mbinu ya usaili na mahojiano zimemuwezesha mtafiti kubaini kuwa jamii ya wazungumzaji wa Kimakunduchi hudondosha sauti za nazali [m] na [n] katika baadhi ya nomino na kusababisha nomino hizo kupokea matamshi tofauti na yalivyo katika jamii ya wazungumzaji wa Kipaje na hata Kiswahili sanifu kama ambavyo data katika Jedwali Na. 4.13 zinavyo lithibitisha hilo hapa chini.

#### **Jedwali Na 4.13 Utوفauti wa Udondoshaji Nazali {m/n} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

<b>KISW</b>	<b>KPJ</b>	<b>KMK</b>
Nchi	Nchi	Chi
Ncha	Ncha	Cha
Mnyama	Mnyama	Nyama

Data hizi za uwandani zinadhahirisha wazi kuwa Kiswahili cha Paje na Makunduchi hutofautiana katika mchakato wa udondoshaji wa nazali katika baadhi ya nomino kwa vile data zinaonesha kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hudondosha nazali [m] na [n] pale tu sauti hizo zinapofuatiwa na sauti za kaakaa gumu [ʃ] na [ŋ] ilihali jamii ya Kipaje huyatamka na kuyatumia maneno hayo kama ilivyo katika Kiswahili sanifu. Udondoshaji huo hufanywa kama kanuni ya ujumla inavyoonesha hapa chini:-



Kanuni hii inafafanua kuwa katika Kimakunduchi wazungumzaji wake hulazimika kufanya udondoshi wa sauti za nazali m / n iwapo na iwapo tu sauti hizo zitakuwa zimefuatiwa na sauti za kaakaa gumu mbili yaani sauti [ʃ] na [ŋ] katika muundo wa nomino husika. Hata hivyo taarifa hizi zinaendana na nadharia ya mofofonolojia ambayo huchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapo ungana pamoja na kuchunguza ubadilishanaji wa sauti ambao utakua na uamilifu wa kimofolojia kuitia misingi hii mtafiti alifanikiwa kubaini sauti za nazali {m/n} zinavyokumbana na badiliko la udondoshwaji zinapokuwa mwanzoni mwa baadhi ya nomino za Kimakunduchi pale zinapofuatiwa na vitamkwa nya kaakaa gumu [ʃ] na [ŋ] badiliko ambalo halipatikani kwa wazungumzaji wa Kipaje. Massamba (2011) anatueleza kuwa katika Kiswahili maneno mengi yanayoishia na irabu [u] na machache yanayoishia na irabu [i], hasa yale yenyeye asili ya Kiarabu, hutamkwa pasi na irabu hizo kusikika akitoa mfano wa maneno hayo ni kama [mwalimu], [hususani] na [fahamu], akiendelea kufafanua zaidi ana dai kuwa irabu [u] na [i] zilizoko mwisho wa maneno hayo hufifishwa katika utamkaji wake, udondoshaji wa namna hii ndio ujulikanao kama udondoshaji mwisho, ambao unajitokeza hata katika Kingereza. Licha ya kuwa massamba ametueleza aina hii ya udondoshaji lakini hajatoa nisababu

zipi zinazochangia udondoshwaji na ufifishwaji wa irabu hizo, hata hivyo mtafiti anaona kuwa jambo hili huchangiwa na utofauti wa kisarufi uliopo baina ya lugha kopaji na kopwaji. Kwa ujumla kila lugha ina namna yake ya udondoshaji kama ilivyo katika Kimakunduchi katika kuzidondosha nazali {m/n} zinapokuwa mwanzoni mwa baadhi ya nomono.


#### **4.2.4 Utofauti Katika Udondoshaji Kitambaza na Kimadende [l] na [r]**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti alibaini kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hudondosha sauti ya kilainisho/kitambaza [l] pamoja na sauti ya kimadende [r] pale ambapo sauti hizo zinapotanguliwa au zinapozitangulia irabu /a/, /i/ na /u/. Udondoshaji huo husababisha muundo wa neno husika kuwa na mfuatano wa irabu mbili kwa wakati mmoja na hata kuunda irabu ndefu. Sifa ambayo haijitokezi kwa wazungumzaji wa Kipaje na badala yake huzitumia sauti hizo kama zitumiwavyo katika Kiswahili. Kama mifano ya data zilizomo katika Jedwali Na. 4.14 zinavyodhahirisha hilo hapa chini.

#### **Jedwali Na 4.14 Utofauti wa Udondoshaji Kitambaza na Kimadende {r/l} Kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>KISW</b>
Hausi	Harusi	Harusi
Ka:tasi	Karatasi	Karatasi
Vu:ga	Vuruga	Vuruga
Sauji	Saruji	Saruji
Usi:fu	Usilifu	Usilifu
Afiki	Rafiki	Rafiki

Data hizi zinadhihirisha wazi kuwa wazungumzaji wa Kimakunduchi hudondosha sauti ya kilainisho [l] na kimadende [r] pale ambapo sauti hizo zitakuwa baina ya irabu mbili au pale tu sauti hizo zitakapo kuwa mwanzoni mwa neno husika. Kama kanuni ya ujumla inavyofafanua zaidi hapa chini:-



Kanuni hii ya ujumla inathibitisha kuwa katika Kimakunduchi sauti ya kilainisho/kitambaza [l] pamoja na kimadende [r] hudondoshwa na wazunguzaji wa Kimakunduchi katika mazingira ya kutanguliwa na kufuatiwa na irabu /i/, /a/, /u/, udondoshaji wa sauti hizo husababisha umbo la ndani linapofika nje kupokea muundo wa kuwa na irabu ndefu ndani yake. Pia taarifa hizi zinaendana na kuafikiana na nadharia ya mofonolojia ambayo hujushuhulisha na uchunguzi wa mabadiliko ya sauti wakati mofimu zinapo ungana pamoja na kuangalia ubadilishanaji wa sauti ambao utakua na uamilifu wa kimofolojia, mambo haya yalimuongoza mtafiti na kufanikiwa kubaini badiliko la udondoshaji wa sauti za utambaza [l] na umadende [r] badiliko ambalo linaleta uamilifu wa kimofolojia kwa jamii ya Kimakunduchi jambo ambalo halipatikani katika jamii ya Kipaje. Pamoja na

hayo taarifa hizi zinakubaliana na taarifa za Athuman (2015) katika tafiti yake amboyo imechunguza athari za kiisimu za Kiswahili katika Kiyao, ambapo alibaini kuwa katika Kiswahili kuna maneno baadhi ya sauti hudondoshwa na kuziacha vokali zikiwa zinafuatana baada ya maneno hayo kutoholewa na kutumika katika Kihaya akilishadidia hili ametoa mfano kuwa maneno [bahasha] na [mahafali] ya Kiswahili hutamkwa [baasha] na [maafali] katika Kihaya hivyo katika maumbo hayo sauti [h] imedondoshwa na kuziacha irabu pekee, kama mtafiti alivyolibaini badiliko hilo katika Kimakunduchi.

#### **4.2.5 Uwiano Katika Udondoshaji Njeo Iliyopita Timilifu [me]**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji wa maongezi ya watafitiwa. Mtafiti alifanikiwa kubaini kuwa Kipaje na Kimakunduchi zinawiana katika sifa ya udondoshaji wa kiambishi njeo iliyopita “me” katika baadhi ya maumbo ya vitenzi kama ambavyo data zilizomo kwenye Jedwali Na. 4.15 zinavyolihitisha hili hapa chini.

#### **Jedwali Na 4.15 Uwiano Katika Udondoshaji Kiambishi Njeo Iliyopita Timilifu [me] kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>KISW</b>
Zenee	Zienee	Zimeenea
Zozo	Ziozo	Zimeoza
Kuzu	Kuzuzu / kuyuzu	Umeuza / umeiyuza
Kuzono	Kuzono	Umeziona
Zingii	Zingii	Zimeingia

Data hizi zinadhihirisha wazi kuwa wazungumzaji wa Kipaje na wale wa Kimakunduchi wanawiana katika kudondosha kiambishi njeo “me” iliyopita katika maumbo ya vitenzi ambavyo wazungumzaji wa Kiswahili sanifu huitamka na

kuitumia njeo hiyo. Hata hivyo taarifa hizi zinakwenda sambamba na nadharia ya mofonolojia ambayo inajikita na uchunguzi wa muundo wa mofimu katika lugha pamoja na kuangalia ubadilishanaji wa sauti ambao utakua na uamilifu wa kimofolojia, nadharia ambayo mtafiti aliitumia na kumuongoza katika kubaini matumizi ya mofimu ya njeo iliyopita [me] katika jamii ya Wapaje pamoja na kubaini udondoshwaji wa mofimu hiyo katika jamii ya wazungumzaji wa Kimakunduchi. Hata hivyo Matinde (2012) anaeleza kuwa viambishi vya njeo na hali huonesha wakati au hali ya kutendeka kwa kitendo, kwa kulithibitisha hilo ameonesha aina za njeo kuwa ni wakati uliopo ambao unawakilishwa na kiambiashi [na], njeo iliyopita inayowakilishwa na kiambishi [li], njeo ijayo inayowakilishwa nakiambishi [ta] na kumalizia na njeo iliyopita timilifu ambayo huwakilishwa na kiambishi [me] mfano [Nimemuona], [Wamenikuta]. Kwa ujumla ni kwamba katika lugha yoyote ile huwa na viambishi vyenye kuonesha wakati na kutumika kwa watumiaji wa lugha husika kama ilivyo kwa wazungumzaji wa Kipaje ambapo hukitumia kiambishi hicho [me] katika mawasiliano yao ilihali jamii nyingine hukidondosha kiambishi hicho kama ilivyo kwa wazungumzaji wa jamii ya Kimakunduchi.

#### **4.2.6 Utofauti Katika Udondoshaji Njeo Iliyopita Timilifu [me]**

Kupitia nadharia ya mofonolojia na isimu linganishi pamoja na mbinu za usaili na ushuhudiaji maongezi ya watafitiwa, mtafiti alibaini kuwa kati ya Kipaje na Kimakunduchi vinatofautiana katika udondoshaji wa njeo iliyopita “me” kwa vile mtafiti amegundua kuwa Kipaje kinasifa ya kuidondosha njeo iliyopita “me” katika

mazingira ambayo Kimakunduchi na Kiswahili sanifu hukitumia kiambishi hicho kama ambavyo data zinavyolidhihirisha hilo hapa chini:-

Mifano namba 16

KMK	KPJ	KISW
<u>Kumelima</u>	kulimi	<u>umelima</u>
<u>Kumesoma</u>	kusomo	<u>umesoma</u>
<u>Kmekwimba</u>	kusikwimba	<u>umeshaimba</u>

Data hizi za uwandani zinadhahirisha wazi kuwa wazungumzaji wa Kipaje hudondosha kiambishi njeo iliyopita “me” katika maumbo ambayo jamii ya wanzungumzaji wa Kimakunduchi na Kiswahili sanifu hukitumia kiambiambishi hicho katika mfumo wa kimawasiliano. Taarifa hizi zinakwenda sambamba na nadharia ya isimu linganishi pamoja na nadharia ya mofonolojia ambazo zinajikita katika kuchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika lugha mabadiliko ambayo huleta tofauti kubwa katika msamati, vile vile zinajishughulisha na mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana. Kwa minajili hiyo nadharia hizi zilimuongoza mtafiti katika kubaini kuwa Kipaje kinapokea badiliko la udondoshwaji wa njeo [me] ilihali Kimakunduchi hubaki na matumizi ya njeo [me] katika maumbo na mazingira ambayo wazungumzaji wa Kipaje hukidondosha kiambishi hicho.


#### **4.2.7 Uwiano Katika Ukakaishaji wa Nazali ya Ufizi /n/**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji mtafiti amebaini kuwa ukakaishaji wa namna hii hutokea katika maneno mengi ya wazungumzaji wa Kimakunduchi na Kipaje ambapo sauti ya nazali /n/ inayotolewa na kutamkiwa katika tuta la ufizi hubadili

muelekeo wake wa kimatamshi na kupokea matamshi ya kakaa gumu kutokana na ujirani na muathiriano wake na irabu ya juu mbele /i/ ambayo hupokea usilimisho mbele na kuwa /j/ na kuisababisha nazali /n/ kuhama katika sehemu yake ya asili kimatamshi na kutamkiwa katika sehemu ya kaakaas gumu na kuwa / jn / kama ambavyo mifano aktiak jedwali na.4.17 inavyoonesha hapa chini.

#### **Jedwali na 4.17 Data za Mchakato wa Ukaakaishaji wa Nazali /n/**

<b>Umbo la ndani</b>	<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>MATAMSHI</b>
N i + ende	Nyende	Nyende	/ njende/
Ni + uzu	Nyuzu	Nyuzu	/ njuzu/
Ni + aga	Nyaga	Nyaga	/ njaga/
Ni + evu	Nyevu	Nyevu	/ njevu/



Kanuni hii ya ujumla inafafanua kuwa sauti ya nazali /n/ katika jamii ya Kimakunduchi na Wapaje baadhi ya wakati nazali ya ufizi /n/ hulazimika kupokea usilimisho wa ukakaishaji pale inapofuatiwa na irabu juu mbele /i/ ambayo hupokea matamshi ya kiyeyusho /j/ na kisha kuiathiri nazali ya ufizi [n] na kupokea matamshi ya kakaa gumu na kutamkika kama /jn/. Taarifa hizi zinaendana na nadharia ya mofonologija inayohusika na uchunguzaji wa ubadilishanaji wa sauti wenye kuleta uamilifu wa kimofologija, kuitia nadharia hii mtafiti alibaini kuwa lahaja zote mbili zinapokea badiliko la kitamkwa [n] kinachotamkwa katika tuta la ufizi na badala

yake kutamkiwa katika kakaagumu baada ya kufuatiwa na irabu ya juu mbele [i], hata hivyo taarifa hizi zinawiana na tafiti ya Athuman (2015) anaeleza kuwa katika muktadha wa utohoaji hususan wakati Kiya kinapotohoa maneno ya Kiswahili yenye sauti za kakaa laini kama vile [k], sauti hizo zinaenda kuwa za kaakaa gumu /č/ kama katika mifano aliyotoa hapo chini.

<b>Kiswahili</b>	<b>Kiyo</b>
<i>Kibatali</i> .....	<i>chibatali</i>
<i>Kiatu</i> .....	<i>chilatu</i>

Kwa ujumla ni kwamba lugha nyingi ulimwenguni hukumbana na mchakato wa ukakaishaji ambapo kiambishi kisicho cha asili ya kakaa hufanywa kuwa cha kakaa kama ilivyo nazali [n] katika Kipaje na Kimakunduchi.


#### **4.2.8 Uwiano Katika Ukakaishaji wa Kiambishi cha Njeo Ijayo “ta”**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji wa mazungumzo ya watafitiwa, mtafiti alibaini kuwa jamii za Wamakunduchi na Wapaje wanapokuwa katika maongezi ya kawaida wanasisya ya ukakaishaji wa kiambishi cha njeo kinachowakilisha wakati ujao “ta” katika mazingira ambayo kitamkwa cha kipasuo hafifu cha ufizi [t] kinapofuatiwa na irabu ya juu mbele [i] pamoja na irabu ya chini mtandazo [a] katika umbo la ndani la neno husika na kwavile irabu ya juu mbele hupokea usilimisho mbele /j/ na kukifanya kipasuo hafifu cha ufizi [t] kupokea matamshi ya kizuiwa kwamizi cha kaakaa gumu [ʃ] kama mifano katika Jedwali na. 4.18 inavyodhihirika hapo chini.

#### **Jedwali na 4.18 Uwiano Katika Ukakaishaji Njeo Ijayo “ta”**

<b>Umbo la ndani</b>	<b>KPJ</b>	<b>KMK</b>	<b>TAF</b>
Wati+aokuja	Wachaokuja	Wachaokuja	Watakaokuja
Wati+aouka	Wachaokuja	Wachaokuja	Watakaokuja
Wati+aosoma	Wachaosoma	Wachaosoma	Watakaosoma

### Kanuni ya jumla



Kanuni hii ya ujumla inafafanua kuwa sauti ya kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kinapofuatiwa na irabu ya juu mbele /i/ katika umbo la ndani, kipasuo hicho hupata usilimisho wa kaakaa gumu na kutamkwa kama [ʃ] wakati wa kupelekwa katika umbo la nje la neno husika kwa wazungumzaji wa Kiswahili cha Paje na wale wa Kimakunduchi. Hata hivyo taarifa hizi zinakwenda sambamba na nadharia ya mofonologija ambayo inashughulika na mabadiliko ya sauti wakati mofimu zinapoungana pamoja na ubadilishanaji wa sauti hizo ambazo zitakuwa na uamilifu wa kimofolojia, kuitia nadharia hii mtafiti alibaini badiliko na nazali [n] ambacho ni kitamkwa cha ufizi kinachopokea usilimisho wa ukakaishaji baada ya kufuatiwa na irabu ya juu mbele [i] kwa jamii zote mbili kati ya Kipaje na Kimakunduchi.

#### 4.2.9 Uwiano Katika Mvutano/Muongano wa Irabu Katika Vitenzi


Mbinu ya ushuhudiaji na mahojiano zilimuwezesha mtafiti kubaini kuwa jamii ya Wamakunduchi na Wapaje wanawiana katika mchakato wa kimvutano wa irabu katika baadhi ya vitenzi. Badiliko hilo hutokea pale ambapo irabu mbili zinapokabiliana katika vitenzi husika, hususani irabu ya juu na ya chini. Irabu ya juu /i/ huvutana na irabu ya chini /a/ na matokeo yake kuzalika irabu ambayo si ya juu wala chini bali irabu inayozalika hapo ni /ɛ/ ambayo kimsingi irabu hii katika jedwali

la irabu msingi ipo katika kiwango cha nusu chini kama data katika jedwali na.4.19 zinavyodhahirika.

#### **Jedwali na 4. 19 Mivutano ya Irabu Katika Kimakunduchi na Kipaje.**

Umbo la ndani	Matokeo ya mvutano	Umbo lisikikalo KMK / KPJ
Wa + iba	We + iba	Webi
Wa + inda	We + inda	Wende
Ka + iba	Ke +iba	Kebi
Wa + isha	We +ishi	Wesi

Kanuni ya jumla




Kanuni hii ya jumla inafafanua kuwa Makunduchi pamoja na Paje huathiriwa na mchakato wa mvutano/ munganiko wa irabu katika kuyakokotoa baadhi ya maumbo ya vitenzi kutoka umbo la ndani kwenda nje. Mvutano huo hutokea pale ambapo irabu ya chini mtandazo /a/ inapokabiliana na irabu ya juu mbele /i/ zikiwa katika mpaka wa mofimu moja katika mazingira ya kutanguliwa na kiyeyusho cha midomo /w/ pamoja na kipasuo hafifu cha kaakaa laini /k/ na kisha kufuatiwa na kipasuo ghuna cha midomo /b/, nazali ya ufizi /n/ na kikwamizi hafifu cha ufizi /s/. Mvutano huo hupelekea kuzaliwa kwa irabu ya kati /ɛ/ yenye sifa ya nusu chini ambayo ni

tofauti na irabu za awali. /a/ + /i/ = /ɛ/. Taarifa hizi zinakubaliana na nadharia ya mofonolojia ambayo inachunguza muundo wa mofimu pamoja na mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana, hivyo mtafiti kupitia nadharia hii alibaini kuwa lahaja zote mbili hukumbana na mchakato wa mvutano wa irabu ambapo irabu ya juu mbele [i] inapokabiliana na irabu ya chini [a] hutokea badiliko la kuzalika irabu ya kati mbele [e]. Hata hivyo Matinde (2012) anaeleza kuwa mvutano wa irabu hutokea pale ambapo irabu mbili zinapokabiliana katika maneno, hususan irabu ya juu na ya chini. Irabu ya juu, huvutana na irabu ya chini, matokeo ni kwamba tunapata irabu ambayo si ya juu wala ya chini bali ipo katikati ya irabu hizo ambayo ni /ɛ/. Kwa ujumla ni kwamba mvutano wa irabu ni tukio linalozikumba lugha nyingi zikiwemo Kipaje na Kimakunduchi.

#### **4.2.10 Uwiano Katika Mchakato wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Nomino**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji ilimuwezesha mtafiti kubaini kuwa jamii zote mbili kati ya Wamakunduchi na Wapaje zinawiana katika mchakato wa uyeyushaji wa nomino “mtoto” ambapo jamii zote neno hili hulitamka “mwanakele” nomino ambayo katika muundo wake wa ndani ulikuwa / mu+anakele/ nomino hii ilipokea mchakato wa uyeyushaji pale ambapo irabu ya juu nyuma /u/ ilipo kabiliana na irabu ya chini mtandazo /a/ isiyofanana nayo kisifa basi irabu ya juu nyuma /u/ ililazimika kubadilika na kupokea umbo la kiyeyusho cha midomo /w/ kama kanuni ya ujumla ya mchakato huu inavyojipambanua hapa:

### Kanuni ya ujumla



Kanuni hii ya ujumla inajifafanua kuwa irabu ya juu nyuma /u/ hubadilika na kuwa kiyeyusho cha midomo /w/ pale ambapo ilipokabiliana na irabu ya chini /a/ irabu ambayo haifanani nayo kisifa katika mazingira ya kutanguliwa na konsonati ya nazali ya midomo /m/. Sambamba na hayo uchanganuzi huu umewiana na nadharia ya mofofonolojia inayojihuisha na uchunguzi wa ubadilishanaji wa sauti pamoja na mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimu zinapoungana, hivyo mtafiti kupitia nadharia hii alibaini kuwa irabu ya juu nyuma [u] hubadilika na kuwa kiyeyusho cha midomo (w) pale inapokabiliana na irabu ya chini [a] katika lahaja zote mbili. Hata hivyo Matinde (2012) anakubaliana na hayo kwa kueleza kuwa uyeyushaji ni badiliko ambalo husababisha baadhi ya irabu kugeuka na kuwa viyeyusho /j/ au /w/ zinapokabiliana katika mazingira maalumu.

#### **4.2.11 Utufauti Katika Mchakato wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Vivumishi Vimilikishi**


Kupitia mbinu ya ushuhudiaji mtafiti alibaini kuwa jamii ya Wamakunduchi huiyeyusha irabu ya juu mbele /i/ na kuwa kiyeyusho cha kaakaa gumu /j/ pale wanapoyakokotoa maumbo ya vivumishi vimilikishi kutoka maumbo ya ndani kwenda ya nje, ilihali jamii ya Wapaje huidondosha irabu ya juu hiyo katika

ukokotoaji wa maumbo ya vivumishi vimilikishi wakati wa kuyapeleka maneno katika umbo la nje yaani umbo lisikikalo katika matamshi kama ambavyo data katika Jedwali na.4.20 zinavyodhihirisha suala hilo.

#### **Jedwali na 4.20 Utarfauti wa Uyeyushaji wa Vivumishi Vimilikishi**

Umbo la ndani	KMK	KPJ	KSW
Li + enu	Lyenu	Lenu	Lenu
Li + angu	Lyangu	Langu	Langu
Linali + otendeka	Linalyotendeka	Linalotendeka	Linalotendeka
Lili + a	Lilya	Lile	Lile
Li + ako	Lyako	Lako	Lako

Kanuni ya ujumla



Kanuni hii ya ujumla inajifafanua kuwa jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili cha Makunduchi huiyeyusha irabu ya juu mbele /i/ na kuifanya irabu hiyo kupokea sura ama umbile la kiyeyusho cha kaakaa gumu /j/ katika mazingira ya irabu hiyo kutanguliwa na kitambaza cha ufizi /l/ na kisha kufuatiwa na irabu za kati /e/ na /o/ pamoja na irabu ya chini mtandazo /a/ katika ukokotoaji wa maumbo ya vivumishi vimilikishi. Uchanganuzi wa taarifa hizi umeenda sambamba na nadharia ya mofonologija ambayo hushughulika na mabadiliko ya sauti yanayotokea wakati mofimmo zinapoungana mabadiliko ambayo huleta uamilifu wa kimofologija, hivyo

kupitia nadharia hii mtafiti alibaini kuwa katika jamii ya wazungumzaji wa Kimakunduchi hutokea badiliko la uyeyushaji wa irabu ya juu mbele inapokabiliana na irabu za kati katika maumbo ya vivumishi ilihali jamii ya Wapaje huidondosha irabu hiyo katika maumbo ya vivumishi vimilikishi.

#### **4.2.12 Utofauti wa Uyeyushaji Katika Maumbo ya Vitenzi Vinavyochukua**


##### **Viambishi Nafsi**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji na hojaji mtafiti amebaini kuwa kunatofauti za kiuyeyushaji kati ya wazungumzaji wa Kiswahili cha Paje na wale wa Makunduchi kwani mtafiti aligundua kwamba jamii ya Wamakunduchi wanaiyeyusha irabu ya juu nyuma /u/ na kuwa kiyeyusho cha midomo /w/ katika mazingira ya kutanguliwa na nazali ya midomo /m/ na kisha kufuatiwa na irabu isiyofanana nayo kisifa hususani irabu ya kati /e/ katika kuyakokotoa maumbo ya vitenzi kutoka umbo la ndani kwenda nje, ilihali jamii ya Wapaje wao huiacha irabu hiyo kama ilivyo na badala yake huidondosha irabu inayofuatia wakati wa kulipeleka neno hilo katika umbo la nje kama mifano toka data zilizomo kwenye Jedwali na 4.21 inavyoonesha.

##### **Jedwali na 4.21 Utofauti Katika Uyeyushaji Katika Mnyambuliko wa Vitenzi**

Umboa la ndani	KMK	KPJ	KISW
Mu + enda wapi	Mwenda wapi	Munda wapi	Mnaenda wapi
Mu + endacheza	Mwendacheza	Mundacheza	Mnaendacheza
Mu + endazenu	Mwendazenu	Mundazenu	Mnaendazenu

Kanuni ya ujumla



Kanuni inajifafanua kuwa katika jamii ya Wamakunduchi wanapokuwa katika mawasiliano yao huiyeyusha irabu ya juu nyuma /u/ katika mazingira ya kutanguliwa na nazali ya midomo /m/ na kisha kufuatiwa na irabu ya kati mbele /e/ katika mazingira hayo irabu ya juu nyuma /u/ hubadilika na kuwa kiyeyusho cha midomo /w/ wakati wa kuyakokotoa maumbo ya vitenzi kutoka umbo la ndani kuja nje. Uchambuzi huu unakwenda sambamba na nadharia ya mofonolojia ambayo inahusu ubadilishanaji wa sauti ambao utakuwa na uamilifu wa kimofolojia, kama ambavyo mtafiti alivyobaini badiliko la irabu ya juu nyuma [u] kuwa kiyeyusho cha midomo[w] baada ya kukabiliana na irabu ya kati [e] kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi.

#### **4.2.13 Uwiano Katika Ung'oekaji wa Viambishi Nafsi**

Kupitia mbinu ya usaili na ushuhudiaji wa mazungumzo ya watafitiwa, mtafiti amegundua kuwa kati ya Kimakunduchi na Kipaje vinauwiano wa kiasi pamoja na tofauti chache katika ung'oekaji wao wa viambishi nafsi ya kwanza, ya pili na yatatu katika hali ya umoja na wingi baina ya jamii lugha hizo kama data za uwandani kupitia Jedwali Na 4.22 zinavyoonesha hapa chini:-

**Jedwali Na 4.22 linaonesha ug'oekaji wa viambishi nafsi kati ya Kipaje na Kimakunduchi**

Viambishi Nafsi	Viyakinishi						Vikanushi					
	KMK		KPJ		KISW		KMK		KPJ		KISW	
	U	W	U	W	U	W	U	W	U	W	U	W
1(ni)- (tu)	N m ny na cha	Tu tu tu tu tu	N ny na sa	Tu tu tu tu	Ni Tu		Si	Ha	Si	Ha	Si	Ha
2 (u)- (m)	U Ku We	M mwe	U Ku We	Mu	U	M	Hu	Ha	Hu	Ha	Hu	Ha
3(a)-(wa)	Ka Ke	We Wa	Ka Ke	We Wa	A	Wa	Ha	Ha	Ha	Ha	Ha	Ha

Data zilizomo katika jedwali na. 4.22 zinadhihirisha wazi kuwa kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi, kuna mfanano na utofautiano katika ung'oekaji wao wa viambishi awali nafsi ya kwanza, ya pili na yatatu katika hali ya umoja na wingi katika uyakinishi na ukarusha wakati wa kuyakokotoa maumbo ya vitenzi kama ambavyo ufanuzi unavyodhihirisha hayo hapa chini.

**4.2.14 Uwiano Wa Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Kwanza (ni)**

Kiambishi awali nafsi ya kwanza umoja (ni) cha Kiswahili sanifu huwakilishwa kwa maumbo tofauti baina ya jamii lugha zote mbili kati ya Wanajamii wa Paje na wale wa Makunduchi, kwani data za uwandani katika jedwali na.4.22 zinadhihirisha kuwa jamii ya Wamakunduchi inakiwakilisha kiambishi hicho kwa maumbo matano tofauti ambayo ni (n), (m), (na), (ny) na (cha) na huwakilishwa na (tu) katika wingi wake. Halikadhalika kwa jamii ya Wapaje nao hukiwakilisha kiambishi hicho kupitia

maumbo manne tofauti kama vile (n), (ny), (na) na (sa) na kuwakilishwa na (tu) katika wingi wake kama ilivyo katika Kimakunduchi, kama mifano toka jamii lugha zote mbili inavyolidhihirisha katika jdwali na.4.23 hapa chini.

#### **Jedwali na 4.23 Uwiano Katika Ung'oekaji Alomofu za Nafsi ya Kwanza (ni)**

Kiambishi nafsi ya kwanza (ni)	KMK	KPJ	KISW
Nfiki	Nfiki	<b>Nimefike</b>	
Nja	Nja	<b>Nimekuja</b>	
Nyuzu	Nyuzu	<b>Nimeuza</b>	
Nyiende	Nyiende	<b>Nimekwenda</b>	
Nyiuku	Nyiuku	<b>Nimeondoka</b>	
<b>Nasumka</b>	<b>Nasumka</b>	<b>Naondoka</b>	

Data hizi katika 4.23 zinaonesha kuwa kati ya Kipaje na Kimakunduchi vinawiana katika alomofu za ung'oekaji wa nafsi ya kwanza ambapo jamii zote mbili hutumia maumbo matatu yaliyofana kuwakilisha nafsi ya kwanza umoja maumbo hayo ni [n], [ny] na [na]. Hivyo taarifa hizi zinaendana na nadharia ya mofonolojia ambayo huchunguza muundo wa mofimu katika lugha. Vile vile taarifa hizi zinaendana na taarifa za Bakari(2015) katika ulinganishaji wake kati ya Kipemba na Kitumbatu, amebaini kuwa Kipemba kina maumbo mawili yanayowakilisha nafsi ya kwanza umoja maumbo hayo ni[n] na [ni], hata hivyo Kitumbatu nacho hukiwakilisha kiambishi nafsi ya kwanza umoja kupitia maumbo mawili tofauti ambayo ni {n} na [na].

#### **4.2.15 Utotfauti katika alomofu za ung'oekaji nafsi ya kwanza (ni)**

Kupitia data za uwandani zinabainisha kuwa Kiswahili kinacho zungumzwa na jamii ya Wapaje na kile cha Wamakunduchi hutofautiana katika ung'oekaji wa kiambishi

awali kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja kwani mtafiti kupitia mbinu ya usaili na ushuhudiaji alibaini kuwa jamii ya Wamakunduchi hutumia kiambishi (m) kuwakilisha nafsi ya kwanza umoja, ilihali jamii ya Wapaje hutumia kiambishi (n) kuwakilisha nafsi ya kwanza katika maumbo ambayo Wamakunduchi hutumia (m). Vilevile mtafitia alibaini yakuwa jamii ya Wamakunduchi hutumia kiambishi (cha) katika mazingira na maumbo ambayo jamii ya Wapaje hutumia kiambishi (sa) kuwakilisha nafsi ya kwanza umoja kama mifano kutoka data za uwandani inavyodhihirisha katika jedwa na.4.24 hapa chini.

#### **Jedwali na 4.24 Utotauti wa Ung'oekaji wa Alomofu za Nafsi ya Kwanza (ni)**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>KISW</b>
Mmekulya	Nli	Nimekula
Mmeludi	Nsirudi	Nimerudi
Mmelima	Nlimi	Nimelima

Pamoja na hayo Kipaje kinajipambanua kwa kutumia kiambishi [sa] katika kukiwakilisha kiambishi nafsi ya kwanza umoja, ilihali Kimakunduchi hutumia Kiambishi [cha] katika kukiwakilisha kiambishi cha nafsi ya kwanza [ni] kitumikacho katika Kiswahili sanifu kama mifano katika Jedwali na. 4.25 inavyodhihirisha hilo hapa chini.

#### **Jedwali na 4.25 Utotauti wa Alomofu “cha”/ “sa” Katika Kukiwakilisha**

##### **Kiambishi Nafsi ya Kwanza (ni)**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>KISW</b>
Chakusumka	Sakusumka	Nitaondoka
Chakuviga	Sakupiga	Nitakupiga
Chadumba	Sadumba	Nitakubali
Chaigoma	Saigoma	Nitaiweza

#### **4.2.16 Uwiano Katika Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Pili [u]**

Kupitia jedwali na 4.22 data za uwandani zinaonesha wazi kuwa kati ya Kipaje na Kimakunduchi kuna uwiano mkubwa katika ung'oekaji wao wa kiambishi awali nafsi ya pili umoja kwa vile mtafiti aligundua kuwa kiambishi awali nafsi ya pili umoja {u} cha Kiswahili sanifu katika jamii lugha zote mbili Kipaje na Kimakunduchi huwakilishwa na maumbo matatu yaliyofanana katika jamii lugha zote mbili tafitiwa yanayowakilisha kiambishi nafsi ya pili umoja {u}, maumbo hayo ni pamoja na (u), (ku) na (we) maumbo hayo hujidhihirisha kama mifano kutika Jedwali na. 4.26 inavyoonesha hapo chini.

#### **Jedwali na. 4.26: Uwiano wa Alomofu Zinazoonesha Ung'oekaji Kiambishi**

##### **Nafsi ya Pili [u]**

Kiambishi awali nafsi ya pili umoja U	KMK	KPJ	KISW
	<b>Uka</b>	<b>Uka</b>	<b>Uondoke</b>
	<b>Ufike</b>	<b>Ufike</b>	<b>Ufike</b>
	<b>Kumelima</b>	<b>Kulimi</b>	<b>Umelima</b>
	<b>Kumesoma</b>	<b>Kusomo</b>	<b>Umesoma</b>
	<b>Kumekwimba</b>	<b>Kusikwimba</b>	<b>Umeshaimba</b>
	<b>Wenda skuli</b>	<b>Wenda skuli</b>	<b>uende skuli</b>
	<b>Weuka</b>	<b>Weuka</b>	<b>Uondoke</b>

#### **4.2.17 Utotofauti Katika Ung'oekaji Nafsi ya Pili {m} wingi**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji na hojaji, mtafiti alibaini kuwa Kipaje na Kimakunduchi vinatofautiana katika ung'oekaji wa kiambishi nafsi ya pili wingi {m}. Kwa vile mtafiti alibaini ya kuwa jamii lugha mbili hizi zinatofauti chache tu katika kukiwakilisha kiambishi nafsi ya pili wingi, mtafiti alibaini kuwa jamii ya Wapaje hutumia umbo {mu} kuwakilisha kiambishi nafsi ya pili {m} ya Kiswahili

sanifu, ilihali jamii ya Wamakunduchi hukiwakilisha kiambishi hicho kupitia maumbo mawili tofauti kama vile {m} na {mwe} kama mifano kutoka jedwali na. 4.27 inavyo dhihirisha hili hapa chini.

#### **Jedwali na 4.27 Utotfauti wa Alomofu Zinazowakilisha Nafsi ya Pili wingi (m)**

Kiambishi awali nafsi ya pili {m} wingi	KMK	KPJ	KISW
<b>mwende wapi</b>	<b>munda wapi</b>	<b>mnaenda wapi</b>	
<b>mwenda cheza</b>	<b>munda cheza</b>	<b>mnaenda cheza</b>	
<b>Mwendazenu</b>	<b>Mundazenu</b>	<b>mnaenda zenu</b>	

#### **4.2.18 Uwiano Katika Alomofu za Ung'oekaji Nafsi ya Tatu Umoja na Wingi (A-WA)**

Data za jedwali na 4.22 hapo juu zilizokusanywa kupitia mbinu za usaili na hojaji pamoja na kurekodi sauti za maongezi ya watafitiwa zimedhihirisha kuwa lahaja za Kipaje na Kimakunduchi zinawiana katika ung'oekaji wa kiambishi nafsi ya tatu umoja na wingi hukidhihirisha kiambishi awali nafsi ya tatu umoja A cha Kiswahili sanifu kupitia maumbo mawili tofauti ambayo ni {ka} na {ke}. Sambamba na hayo, jamii lugha hizi mbili zimewiana katika kukiwakisha kiambishi cha nafsi ya tatu wingi {wa} cha Kiswahili sanifu kupitia maumbo mawili tofauti kama vile {we} na {wa} kama mifano ya data katika jedwali na. 4.28 zinavyolidhihirisha hili hapa chini.

### **Jedwali na 4.28 Uwiano wa Alomofu Zinazowakilisha Viambishi Nafsi ya Tatu**

#### **Umoja na Wingi (A-WA)**

<b>KMK</b>		<b>KPJ</b>		<b>KISW</b>	
<b>U</b>	<b>W</b>	<b>U</b>	<b>W</b>	<b>U</b>	<b>W</b>
<b>Kanalala</b>	<b>Wanalala</b>	<b>Kanalala</b>	<b>Wanalala</b>	<b>Analala</b>	<b>Wanalala</b>
<b>Kanachowea</b>	<b>Wanachowea</b>	<b>Kanasema</b>	<b>Wanasema</b>	<b>Anasema</b>	<b>Wanasema</b>
<b>Kanalola</b>	<b>Wanalola</b>	<b>Kanatizama</b>	<b>Wanatizama</b>	<b>Anatizama</b>	<b>Wanatizama</b>
<b>Kebi</b>	<b>Weki</b>	<b>Kebi</b>	<b>Weki</b>	<b>Ameiba</b>	<b>Wameiba</b>
<b>Kenende</b>	<b>Wende</b>	<b>Kende</b>	<b>Wende</b>	<b>Ameondoka</b>	<b>Wameondoka</b>
<b>Kesi</b>	<b>Wesi</b>	<b>Kesi</b>	<b>Wesi</b>	<b>Amemaliza</b>	<b>Wamemaliza</b>

#### **4.2.19 Utofauti Katika Ung'oekaji wa Viambishi vya O-rejeshi vya Ngeli ya A-WA (Ye – O)**

Kupitia nadharia ya mofolojia na isimu linganishi pamoja na mbinu za usaili , mtafiti amegundua kuwa Kimakunduchi na Kipaje vinatofautiana katika ung'oekaji wao wa viambishi vya “o”-rejeshi katika ngeli ya (A- WA) katika umoja na wingi kulingana na kiambishi njeo kitakachofuatana nacho kama ifuatavyo.

##### **4.2.19.1 Utofauti Katika Ung'oekaji Viambishi O-rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li)**

Kupitia watafitiwa, mtafiti amebaini kuwa kuna tofauti katika ung'oekaji wa viambishi vya o-rejeshi kwa vile Kimakunduchi hutumia kiambishi “e” kuwakilisha kiambishi “ye” katika umoja wa ngeli ya A-WA, vile vile kiambishi “o” huwakilisha kiambishi “o” cha wingi wa o-rejeshi kulingana na njeo iliyopita “li” ilihali Kipaje hutumia kiambishi cha o-rejeshi “lo” kwa umoja na wingi kama data katika jedwali na.4.29 na jedwali na. 4.30 zinavyoonesha hapa chini.

**Jedwali na 4.29 Ung'oekaji wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li)**

**Kimakunduchi.**

<b>KMK</b>		<b>KISW</b>	
<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
Aekuja	Waokuja	Aliyekuja	Waliokuja
Aeuka	Waouka	Aliyeondoka	Walioondoka
Aesoma	Waosoma	Aliyesoma	Waliosoma

Halikadhalika maumbo ya o-rejeshi yanawakilishwa na kipaje kulingana na njeo iliyopita ni kama yanavyo dhihirishwa katika jedwali na. 4.30 hapa chini.

**Jedwali na 4.30 Ung'oekaji wa O-Rejeshi Kulingana na Njeo Iliyopita (li)**

**Kipaje.**

<b>KPJ</b>		<b>KISW</b>	
<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
Alokuja	Walokuja	Aliyekuja	Waliokuja
Alouka	Walouka	Aliyeondoka	Walioondoka
Alosoma	Walosoma	Aliyesoma	Waliosoma

Majedwali namba 4.29 na 4.30 hapo juu zinadhihirisha wazi kuwa kuna utofauti mkubwa katika ung'oekaji wa viambishi vya o-rejeshi katika ngeli ya A-WA kwa vile data kutoka uwandani zinaonesha kuwa Kipaje hutumia kiambishi "lo" katika umoja na wingi kama kiambishi cha o-rejeshi katika ngeli ya A-WA, ilihali Kimakunduchi hutumia kiambishi "e" cha umoja na kiambishi "o" hutumika kuonesha wingi wa o-rejeshi katika ngeli ya A-WA kulingana na njeo iliyopita "li". Kihore na wenzake (2003) wanaeleza kuwa viambishi virejeshi ni vile vinavyowakilishwa vitajwa katika umbo hasa la kitenzi wakilithibitisha hili wanatoa mifano toka lugha ya Kiswahili kama;

Wa + o → wo → o wa-li- <b>o</b> - kuja,	ch + o → cho, ki-li- <b>cho</b> - potea
U + o → wo → o u-li- <b>o</b> -anguka	i + o → yo, i-li- <b>yo</b> - simama
Li + o → lo, li-li- <b>lo</b> - nunuliwa	vi + o → vyo, vi- li- <b>vyo</b> - letwa

Tunakubaliana nao kuwa viambishi vya o-rejeshi kuwa hujitokeza katika vitenzi na hufanya kazi ya kurejelea vitajwa kulingana na ngeli za nomino pamoja na viambishi njeo vitakavyoandamana navyo kama ilivyokuwa kwa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

#### **4.2.19.2 Utofauti Katika Ung'oekaji Viambishi vya O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta)**

Kupitia watoa taarifa pamoja na nadharia za mofolojia na isimulinganishi mtafiti alibaini kuwa Kipaje na Kimakunduchi hukimbiana katika ung'oekaji wao wa viambishi vya o-rejeshi kulingana na kiambishi cha njeo ijayo katika maumbo yao ya vitenzi. Wazungumzaji wa Kipaje wanapotaka kutumia o-rejeshi katika muda ujao hutumia kiambishi “cho” na kukibebesha majukumu mawili kwa wakati mmoja; kwanza, kuonesha njeo ijayo na hapohapo kufanya kazi ya o-rejeshi katika hali ya umoja na kiambishi “o” hutumika kama o-rejeshi ya wingi katika ngeli ya A-WA, ilihali wazungumzaji wa Kimakunduchi wao hutumia kiambishi “e” katika umoja na kiambishi “o” hutumika katika hali ya wingi kama data katika Jedwali na 4.31 zinavyodhahirisha.

**Jedwali na 4.31:Ung'oekaji Wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta) Katika Kimakunduchi.**

<b>KMK</b>		<b>KISW</b>	
<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
Achaekuja	Wachaokuja	Atakayekuja	Watakaokuja
Achaeuka	Wachaouka	Atakayeondoka	Watakaoondoka
Achaesoma	Wachaosoma	Atakayesoma	Watakaosoma

**Jedwali na 4.32:Ung'oekaji wa O-rejeshi Kulingana na Njeo Ijayo (ta) Katika Kipaje.**

<b>KPJ</b>		<b>KISW</b>	
<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
Achokuja	Wachaokuja	Atakayekuja	Watakaokuja
Achouka	Wachaouka	Atakayeondoka	Watakaoondoka
Achosoma	Wachaosoma	Atakayesoma	Watakaosoma

Data za uwandani hapo juu zinaonesha wazi kuwa Kipaje na Kimakunduchi vinaukimbiano kiasifulani katika ung'oekaji wa O-rejeshi kulingana na njeo inayowakilisha wakati ujao kwani data zinaonesha kuwa jamii lugha hizi zinawiana katika upokeaji wa kiambishi cha o-rejeshi katika hali ya wingi ambacho ni "o" ilihali katika umoja zinatofautiana kwa vile Kimakunduchi hupokea kiambishi "e" kama kiambishi cha o-rejeshi ilihali jamii ya Kipaje wao hutumia kiambishi "cho" kama kiambishi cha njeo ijayo na hapo hapo hutumika kama kiambishi cha o-rejeshi katika hali ya umoja katika vitenzi vinavyoonesha muda ujao.

#### **4.3 Uwiano wa Kimaana Bainya Msamiati wa Kiswahili cha Paje na Kile cha Makunduchi.**

Sehemu hii inajibu lengo la tatu pamoja na swali la tatu la utafiti huu yanayohusu uwiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

##### **4.3.1 Msamiati wa Msingi Ulionfanana Kimofolojia na Kimaana**

Kupitia mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji mtafiti amebaini kuwa kuna msamiati wa msingi unaofanana kimofolojia na kimaana baina ya jamii ya Wapaje na Wamakunduchi wanapokuwa katika mawasiliano yao ya kawaida kama data zilizomo katika Jedwali na 4.33 uwandani zinavyolidhihirisha hilo hapa chini

##### **Jedwali na 4.33: Msamiati Ulionfanana Kimofolojia na Kimaana Bainya Kipaje na Kimakunduchi.**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>
Chaki	Chaki	kifaa cha kuandikia/ mdudu
Kinga	Kenga	Tizama
Kimeo	Kimeo	Kilimi
javi	javi	kifaa kinachosukwa kwa mlala
Javi	Javi	kikao cha mazikoni
Kitungu	Kitungu	Kitovu
Kiganja	Kiganja	kiungo cha mwili
Chaka	Chaka	haraka / upesi
Wivu	Wivu	mapenzi yaliyopindukia
Mvyazi	Mvyazi	Mzazi
Chembe	Chembe	punje/ mbegu
Tuwale	Tuwale	nyama za baharini
Toji	Toji	tone la maji
Chakiza	Chakiza	chafua/ kuchafua sehemuiliyo safi
Bigili	Bigili	mtego/mawe yaliyokusanywa kuonesha mpaka wa shamba
Chaga	Chaga	Kimepotea

Data hizo kutoka uwandani zinaonesha kuwa watumiaji wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi wanafanana kimofolojia kupidia idadi ya sauti ziundazo msamiati huo, mpangilio sawa wa sauti hizo katika uundaji wa msamiati husika. Hata hivyo msamiati huo huwakilisha maana iliyo sawa katika lahaja zote mbili katika kimawasiliano. Taarifa hizi zinaenda na nadharia ya isimu linganishi ambayo hujishuhulisha na ulinganishi wa kimofolojia pamoja msamiati wa lugha ili kuthibitisha kuwa zina asili moja, hivyo mtafiti aliitumia nadharia hii katika kulinganisha msamiati wa lahaja mbili hizi na kubaini kuwa zinalingana kimofolojia na kimaana. Juma(2011) katika kulinga Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kikizimkazi alibaini kuwa Kimakunduchi kinawiana na Kimtende na Kibwejuu lakini kinatofautiana na Kikizimkazi na kutueleza kuwa Kimtende na kibwejuu ni lahaja za Kimakunduchi na Kikizimkazi si mionganoni mwa lahaja hizo hii ni kutokana na kuwa kimeathiriwa zaidi na Kiunguja.

#### **4.3.2 Msamiati wa Msingi Uliotofautiana Kimofolojia kwa Sauti Moja Lakini**

##### **Hufanana Kimaana**

Kupitia ushuhudiaji, maktabani na usaili mtafiti amebaini kuwa kati ya jamii ya Kipaje na ya Kimakunduchi kuna msamiati wa msingi unaotumiwa na jamii hizi ambao unatofautiana kimofolojia kupidia sauti moja tu lakini maumbo hayo yanawasilisha maana iliyosawa kwa jamii zote mbili kama ambavyo data zilizomo katka jedwali na.4.34 zinavyodhahirisha hilo hapa chini.

**Jedwali na 4.34 Msamiati Uliotofautiana Kimofolojia Lakini Unafanana**

**Kimaana**

<b>KMK</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>
Afiki	Rafiki	Rafiki
Hausi	Harusi	Harusi
Venya	Penya	Penya
Chi	Nchi	Nchi
Vita	Pita	Kupita
Soto	Kushoto	upande wa kushoto
Mosi	Moshi	Moshi

Data hizi kutoka uwandani zinadhihirisha kuwa baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kuna msamiati unao tofautiana kimofolojia kupitia sauti moja tu aidha tofauti hiyo itakuwa mwanzoni au katika kutohana na udondoshwaji, licha ya kutofautiana kwao huko lakini huwakilisha maana moja kwa lahaja zote mbili. Nadharia ya isimu linganishi imehusika na hili kwa vile hulenga kuchunguza mofolojia ya lugha mbili katika kuthibitisha kuwa msamiati wa lugha mbili una asili moja au ala. Hata hivyo taarifa hizi zinaendana na taarifa za Bakari(2015) katika ulinganishi wake baina ya Kitumbatu na Kipemba ambapo alibaini kuwa kati ya lahaja mbili hizi kuna vitenzi vinavyolingana kimaana na kutofautiana kumuundo kwa baadhi ya sauti, kila kitu kinalinga isipokuwa sauti moja akilishadidia hili alitoa mfano wa msamiati huo Kipemba husema [changa] wakati Kitumbatu neno hilo hilo hulitamka kama [chanja] hivyo tofauti inayojitokeza na sauti [g] kwa Kipemba na [j] kwa Kitumbatu, hii ni kutohana na mwachano wa kijiografia uliyopo baina ya lahaja mbili hizi.

### **4.3.3 Msamiati wa Msingi Uliotofautiana Kimofolojia Moja kwa Moja Lakini Hufanana Kimaana**

Baada ya mtafiti kuzitathmini data za uwandani na maktabani na kupitia ushuhudiaji na mahojiano mtafiti alibaini kuwa baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi unatofautiana kimofolojia kwa neno lote lakini maumbo hayo huwakilisha maana iliyosawa katika mawasiliano kwa jamii zote mbili tofauti ambazo zinachangiwa na uwepo wa mwachano wa kijiografia baina ya lahaja mbili hizi kama data katika jedwali na. 4.35 zinavyolidhihirisha hili hapa chini.

### **Jedwali na 4.35 Msamiati Uliotofautiana Kimofolojia Moja kwa Moja na Kufanana Kimaana**

KMK	KPJ	TAF
Tohio	Mpumbavu	Mpumbavu
Kuwapa	Kutafuta	Kutafuta
Chimwene	Askari	Askari
Tena	Tahiri	tahiri/jando
Bokoa	Pasua	pasua / katiza /njia za mkato
ng'ung'ujika	nung'unika	nung'unika/lalamika

Data hizo zinaonesha kuwa Kiswahili kinachozungumzwa Paje na kile cha Makunduchi vinawiana katika uwakilishi wa maana lakini vinatofautiana katika mofolojia ya msamiati husika kwavile kila jamii inatumia muundo wake katika kuuwakilisha msamiati huo, hatahivyo kunamsamiati unaojitokeza katika Kimakunduchi tu ambao mofolojia yake haijitokezi katika Kipaje wala Kiswahili sanifu mfano wa msamiati huo ni pamoja na *kuwapa, chimwene, tohino, tena*. Vile vile kuna msamiati ambao unapatikana katika lahaja ya Kimakunduchi ambao unawakilisha maana tofauti na zitumikazo katika Kiswahili mfano wa maneno hayo ni

kama “*tena*” ambalo kwa Kimakunduchi lina maanisha ‘*tahiri*’ lakini maana ya Kiswahili ya neno hilo ni ‘*zaidi*’ au ‘*engeza*’. Taarifa hizi zinakubaliana na nadharia ya isimu linganishi ambayo inalinga mofolojia pamoja na msamiati wa lugha mbili ili kuthibitisha kuwa zina asili moja au la, hata hivyo Bakari(2015) katika kulinganisha Kipemba na Kitumbatu alibaini kuwa baina ya lahaja mbili hizi kuna naomino zinazotofautiana kimaumbo na kulingana kimaana akitolea mfano hilo anasema Kipemba hutumia neno ‘*athari*’ ilihali Kitumbatu hutumia ‘*asari*’licha ya kutofautiana kimofolojia lakini maumbo hayo yanawakilisha maana inayolingana kwa jamii zote mbili.

#### **4.3.4 Msamiati wa Msingi Uliofanana Kimofolojia Lakini Umetofatiana**

##### **Kimaana**

Kupitia ushuhudiaji na mahojiano mtafiti pia alibaini kuwa baina ya Kiswahili kinachozungumzwa Paje na kile cha Makunduchi kuna msamiati wa msingi unaotumiwa na jamii zote mbili katika mawasiliano yao ya kila siku ambao umefanana kimofolojia lakini unawakilisha maana tofauti baina ya wazungumzaji wa jamii hizo mbili kama ambavyo data katika jedwali na. 4.36 zinavyoonesha hapa chini.

### **Jedwali na 4.36 Masamiati Uliofanana Kimofolojia Lakini Maana Tofauti**

<b>KMK</b>	<b>TAF</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>
Bwaga	wali laini	bwaga	kuangusha kitu
Buga	Hangaika	buga	suruali pana zaidi
Chewa	Kuchelewa	chewa	aina ya samaki
Haha	Njaa	haha	hangaika/teseka
taa	kukataa jambo	taa	kifaa cha kumurikia
Ima	simama/wima	ima	au/ ama/ kiunganishi
Kamba	nazi iliyokauka maji	kamba	yakufungia kitu
Tena	kutahiri/jando	tena	engeza/zaidi
Kitu	paka mweusi	kitu	kifaa
Vita	Kupita	vita	mapigano
Vika	Kupika	vika	kuvisha kitu
Nyama	ni mnyama mweyewe	nyama	kitoeleo/mboga
Afiki	Rafiki	afiki	kukubaliana na jambo
Kipanga	kifuu cha nazi	kipanga	kifaa cha kukatia
Chaka	taka/hitaji	chaka	pori/mwitu
Kosa	kukosha kitu	kosa	tatizo/kukosea
Wivu	kuwiva chakula	wivu	mapenzi yaliyozidua

Data hizi zinaonesha kuwa kati ya Kipaje na Kimakunduchi kuwa kuna maumbo ya maneno ambayo hutamkwa na kuandikwa sawasawa baina ya lahaja zote mbili lakini huwakilisha maana tofauti za kimatumizi baina yao. Kipaje kimejifungamanisha zaidi na Kiswahili sanifu kimaumbo na uwakilishaji wa kimaana baina ya kiashiria yaani umbo neno na kiashiriwa yaani kitu kinacho kusudiwa ilihali Kimakunduchi kimejifungamanisha kimofolojia tu lakini kujipambanua na Kiswahili sanifu katika uwakilishaji wa maana, hili linatokana na kuwa Kipapaje kimeathiriwa sana na Kiswahili sanifu kuliko Kimakunduchi. Hivyo kupitia nadharia ya isimu linganishi mtafiti alibaini kuwa Kipaje kinajipambanua kati yake na Kimakunduchi na kujitegemea kimaana kama ambavyo nadharia hii inavyojikita na uchunguzaji wa msamiati wa lugha mbili ili kubaini kuwa zina asili moja pamoja na kuchunguza

mabadiliko ambayo hutokea katika lugha na kuleta tofauti kubwa katika msamati kama ilivyo kwa Kipaje na Kimakunduchi. Hata hivyo taarifa hizi zina afikiana na tafiti ya Ali (2015) ambaye alilinganisha Kipemba cha Kaskazini na Kusini na kueleza kuwa kunatofauti kubwa baina ya maeneo haya, kwani amebaini kuwa Kipemba cha kaskazini kinahifadhi msamati wa kipemba cha kale (lahaja) ambapo kile cha Kusini kinataka kufanana na Kitumbatu lakini kwa kiasi kikubwa kinaelekea kwenye usanifu, kama ambavyo mtafiti alivyo baini katika Kimakunduchi na Kipaje.

#### **4.4 Muhtasari wa Sura**

Katika sura hii, uwasilishaji na uchambuzi wa data umeoneshwa na kufanya utafiti huu kukamilika. Malengo mahususi matatu ya utafiti huu yamekamilishwa na kwa kila lengo limejibiwa kwa namna yake kwasababu kila moja linajitegemea kimantiki katika kuonesha ulinganifu wa kiisimu uliopo baina ya Kiswahili kizungumzwacho Paje na kile cha Makunduchi. Sura inayofuata inahu muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

## SURA YA TANO

### UTANGULIZI, MUHTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

#### **5.1 Muhtasari wa jumla**

#### **5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini uwiano na utofauti wa kiisimu uliopo baina ya Kiswahili kinachozungumzwa Paje na kile cha Makunduchi Kusini Unguja. Utafiti huu una malengo mahususi matatu yakiwemo: Kubainisha mfanano na utofauti baina ya fonimu za Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi, kulinganisha na kutofautisha kanuni za kifonolojia na mofofonolojia zinazotawala maumbo ya mofu zinazojenga maneno ya Paje na yale ya Makunduchi na tatu ni kubainisha uwiano na utofautiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi.

#### ***Matokeo ya lengo mahususi la kwanza na swali la kwanza la utafiti***

Baada ya uchunguzi wa kina kufanyika kuhusu uwiano na utofauti wa kifonimu baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi mambo kadhaa yamebainika;

Kwanza imedhihirika wazi kuwa kuna tofauti ndogo ya umiliki wa fonimu za konsonanti inayojitokeza kati ya Kiswahili cha Paje na cha Makunduchi kwa vile matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa Kimakunduchi kina jumla ya fonimu za konsonanti 23 na viyeyusho 2, ilihali Kipaje kina jumla ya fonimu za konsonanti 24 na viyeyusho 2, tofauti inajitokeza pale ambapo Kipaje kina sifa ya umiliki wa kitamkwa cha umadende /r/ ambacho hakipatikani katika jamii ya Kimakunduchi, pamoja na hayo Kimakunduchi kinaongezeko la fonimu za ziada ambazo zinasifa ya

kuungana kati ya konsonanti za asili zinapokabiliana na viyeyusho na kuunda fungu moja la fonimu kama vile [ly], [vy], [fw]. Hata hivyo imebainika kuwa jamii zote mbili hazina sifa ya kumiliki sauti zenye asili ya Uarabu zilizokopwa na kutumika katika Kiswahili sanifu sauti hizo ni kama vile [γ] [ð] na [Ø]. Pamoja na hayo, matokeo hayo yanabainisha kuwa Wamakunduchi wanajitofautisha kati yao na Wapaje katika umiliki wa fonimu za irabu kwani data zinaonesha kuwa Kipaje kinamiliki irabu tano (5) tu ambazo zote ni fupi wakati Kimakunduchi kinamiliki irabu kumi (10) ambazo tano fupi na tano ni irabu ndefu.

Pili ni kwamba matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa jamii ya Wamakunduchi inajitofautisha na jamii ya Wapaje katika matumizi ya fonimu kwani data zilizokusanywa zinadhihirisha kuwa Kimakunduchi hutumia fonimu ya kitambaza [l] pale ambapo jamii ya Wapaje hutumia fonimu ya kimadende [r] kama ambavyo Kiswahili sanifu hutumia. Vile vile Wamakunduchi wanajitofautisha na Wapaje, kwa vile jamii hiyo hutumia fonimu ya kikwamizwa ghuna cha midomo meno [v] katika mazingira ambayo jamii ya Wapaje hutumia fonimu ya kipasuo hafifu cha midomo [p], vile vile matokeo yanatubainishia kuwa jamii lugha mbili hizi zinatofautiana katika matumizi ya [ly] na [l], kwani imegundulika kuwa Wazungumzaji wa Kimakunduchi hutumia fonimu [lj] ambayo inamchanganyiko wa fonimu ya kitambaza [l] na kiyeyusho [j] na kuunda fonimu moja [lj] itokanayo na vitamkwa viwili badala ya [l] pekee, ilihali jamii ya Kipaje hutumia fonimu moja [l] tu kama ilivyo katika matumizi ya Kiswahili sanifu, vile vile matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa Wamakunduchi wanajitofautisha kwa kutumia fonimu ya [fw] ilijojumuisha kitamkwa cha mdomo meno /f/ na kiyeyusho cha midomo /w/ na

kuunda fungu moja la fonimu [fw] na kutumika fungu hilo katika baadhi ya maneno ambayo jamii ya Wapaje hutumia fonimu /f/. Sambamba na hayo Wamakunduchi wanajipambanua na Wapaje kwani matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa jamii hiyo inautaratibu wa kuchanganya kitamkwa cha kikwamizi cha mdomo meno /v/ na kiyeyusho cha midomo /w/ na kuunda fungu moja la fonimu [vw] na kutumika fungu hilo katika mazingira ambayo jamii ya Wapaje hutumia sauti [v], pamoja na hayo ni kwamba jamii ya Wamakunduchi inajitofautisha na jamii ya Wapaje kwavile matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa Wamakunduchi fonimu inayozalika kutokana na kitamkwa cha kipasuo hafifu cha midomo /p/ pamoja na kiyeyusho cha kaakaa gumu /j/ na kutamkwa kama [pj] na kutumika katika mazingira ambayo jamii ya Kipaje hutumia sauti ya kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kama kitumikavyo katika Kiswahili sanifu.

***Matokeo ya lengo mahususi la pili na swalí la pili la utafiti***

Baada ya uchunguzi wa kina kufanyika kuhusu uwiano na utofauti wa kanuni za kifonolojia na kimofolojia zinazotumika na kutawala maumbo ya mofu ziundazo maneno baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kuna mambo kadhaa yamebainika;

Kwanza ni kwamba matokeo yanabainisha kuwa jamii zote mbili Wapaje na Wamakunduchi wanawiana katika udondoshaji wa irabu ya juu mbele /i/ iwapo na iwapo inapotanguliwa na kitamkwa cha nazali ya ufizi /n/ pale ambapo kitakuwa mwanzani mwa kitenzi katika kukiwakilisha kiambishi nafsi ya kwanza umoja [ni], vile vile matokeo yanatubainishia kuwa jamii hizo zimewiana katika udondoshaji wa nazali m/n, nazali hizi hulazimika kudondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na

sauti ya kikwamizwa cha midomo meno /v/ na kile cha ufizi /z/. Hata hivyo matokeo yanatubainishia kuwa jamii ya wazungumzaji wa Kimakunduchi hujipambanua katika kuzidondosha sauti za nazali [m] na [n] katika baadhi ya nomino, ilihali Wapaje wao huzitamka na kuzitumia nazali hizo katika nomino ambazo Wazungumzaji wa Makunduchi huzidondosha sauti hizo, vile vile matokeo yanabainisha kuwa Wamakunduchi wanajitofautisha kwa kuzidondosha sauti za kilainisho/kitambaza /l/ na kimadende /r/ sauti ambazo hutumiwa na jamii ya Wapaje katika mazingira na maumbo ambayo Wamakunduchi huzidondosha sauti hizo. Vilevile matokeo ya utafiti yanatubainishia kuwa Kipaje na Kimakunduchi vinawiana katika sifa ya udondoshaji wa kiambishi njeo iliyopita timilifu “me” katika baadhi ya maumbo ya vitenzi, hata hivyo matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa jamii ya Wapaje inajitofautisha na jamii ya Wamakunduchi kwa vile wazungumzaji wa Kiswahili cha Paje hudondosha kiambishi njeo iliyopita timilifu “me” katika maumbo ambayo Kimakunduchi na Kiswahili sanifu hukiingiza na kukitumia kiambishi hicho, pamoja na hayo matokeo yanabainisha kuwa jamii zote mbili zinawiana katika ukakaaishaji wa nazali ya ufizi /n/ pale inapofuatiwa na irabu ya juu mbele /i/ na kusababisha sauti hiyo kupokea matamshi ya kiyeyusho /j/ na kisha kutamkwa kama /ŋ/, sambamba na hayo jamii hizi zinawiana katika ukakaaishaji wa sauti ya kipasuo hafifu cha ufizi /t/ kinachowakilisha njeo ijayo pale tu kinapofuatiwa na irabu ya juu mbele /i/ katika umbo la ndani, na kupelekea kipasuo hicho hupata usilimisho wa kaakaa gumu na kutamkwa kama [ʃ] katika umbo la nje. Vilevile matokeo yanatuonesha kuwa Kiswahili cha Paje na Makunduchi vinawiana katika mchakato wa mvutano/ munganiko wa irabu katika baadhi ya maumbo ya vitenzi, mvutano huo hutokea pale ambapo irabu ya chini

mtandazo /a/ inapokabiliana na irabu ya juu mbele /i/ zinapokuwa katika mazingira ya mpaka wa mofimu moja na matokeo yake kuzaliwa irabu /ɛ/ ambayo ni yenyé sifa ya nusu chini.

Pia Wamakunduchi na Wapaje wanawiana katika mchakato wa uyeyushaji wa nomino “mtoto” ambapo jamii zote neno hili hulitamka “mwanakele” nomino ambayo katika muundo wake wa ndani ulikuwa /mu+anakele/ nomino hii ilipokea mchakato wa uyeyushaji pale ambapo irabu ya juu nyuma /u/ ilipo kabiliana na irabu ya chini mtandazo /a/ isiyofanana nayo kisifa na kupelekea irabu ya juu nyuma /u/ kupokea sura ya kiyeyusho cha midomo /w/ katika umbo la nje la nomino husika. Licha ya kuwiana hapo, hata hivyo matokeo yanaonesha kuwa Kiswahili cha Makunduchi kinajipambanua na kile cha Paje kwavile jamii ya Wamakunduchi huiyeyusha irabu ya juu mbele /i/ na kuifanya ipokee sura ama umbile la kiyeyusho cha kaakaa gumu /j/ katika mazingira ya kutanguliwa na kitambaza cha ufizi /l/ na kisha kufuatiwa na irabu za kati /e/ na /o/ pamoja na irabu ya chini mtandazo /a/ katika ukokotoaji wa maumbo ya vivumishi vimilikishi, sambamba na hayo matokeo yanadhihirisha kuwa jamii ya Wamakunduchi inajipambanua na Wapaje katika mchakato wa uyeyushaji katika maumbo ya vitenzi kwavile imebainika kuwa jamii ya Wamakunduchi huiyeyusha irabu ya juu nyuma /u/ na kuwa kiyeyusho cha midomo /w/ katika mazingira ya kutanguliwa na nazali ya midomo /m/ na kisha kufuatiwa na irabu isiyofanana nayo kisifa hususani irabu ya kati /e/ katika kuyakokotoa maumbo ya vitenzi kutoka umbo la ndani kwenda nje.

Pia matokeo yanabainisha kuwa jamii ya Kimakunduchi inajipambanua na ile ya kipaje kwa kuwa na umiliki wa alomofu tano zinazo wakilisha mofimu ya nafsi ya

kwanza umoja (ni) alomofu hizo ni (n), (m), (cha), (na) na (ny), ilihali jamii ya Wapaje inamiliki maumbo manne ya alomofu yanayowakilisha mofimu ya nafsi ya kwanza umoja (ni) maumbo hayo ni pamoja {n}, {ny}, {na} na {sa}, sambamba na hayo jamii jimii hizo zinakimbiana katika matumizi ya maumbo ya alomofu nafsi hayo kwani Wamakunduchi hutumia alomofu {m} pale ambapo Wapaje hutumia {n}, vilevile Wamakunduchi hutumia alomofu {cha} pale ambapo Wapaje hutumia umbo {sa} katika kuiwakilisha nafsi ya kwanza umoja (ni), pamoja na kutofautiana kwao huko katika kiambishi kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja lakini jamii hizi mbili zinawiana katika uwakilishaji wa nafsi ya kwanza wingi ambapo jamii zote hutumia kiambishi (tu) kuiwakilisha nafsi hiyo katika hali ya wingi.

Vile vile Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi vinawiana katika umiliki wa maumbo matatu ya alomofu zinazowakilisha mofimu ya nafsi ya pili umoja maumbo hayo ni pamoja na {u}, {ku} na {we} katika mazungumzo ya kawaida kama ambavyo matokeo ya utafiti yanavyoonesha, licha ya kuwiana kwao huko katika nafsi ya pili umoja lakini jamiii hizi zinakimbiana na kujipambanua katika uwakilishaji wa nafsi ya pili wingi kwani matokeo yanatubainishia kuwa jamii ya Wamakunduchi inatumia alomofu {mwe} kuiwakilisha mofimu ya nafsi ya pili (m) wingi, ilihali jamii ya Wapaje wao hutumia alomofu {mu} kuiwakilisha mofimu ya nafsi ya pili wingi.

Halikadhalika jamii hizi mbili zinafungamana katika ung'oekaji wa viambishi nafsi ya tatu umoja na wingi kwavile matokeo yanaonesha kuwa Wapaje na Wamakunduchi hutumia alomofu mbili {ka} na {ke} kuwakilisha nafsi ya tatu

umoja (A), vilevile hutumia alomofu {we} na {wa} kuiwakilisha nafsi ya tatu wingi (WA) katika mazungumzo yao.

Katika kuyakamilisha matokeo ya lengo na swali la pili ni kwamba jamii ya Wamakunduchi inajipambanua kwa kujitofautisha na Wapaje katika ung'oekaji wa o-rejeshi katika ngeli ya (A- WA) kulingangana na njeo iliyopita "li" kwavile matokeo yanabainisha kuwa Wamakutuchi hutumia kiambishi "e" umoja na "o" wingi kuwakilisha o –rejeshi katika ngeli ya (A – WA), ilihali Wapaje wao hutumia kiambishi "lo" kuwakilisha o – rejeshi umoja na wingi katika ngeli hiyo hiyo. Pamoja na hayo jamii hizi zinatofautiana na kuachana katika ung'oekaji wa o – rejeshi katika ngeli ya (A – WA) kulingana na njeo ijayo (ta) kwani matokeo yanabainisha kuwa Wamakunduchi wao hutumia kiambishi "e" umoja na "o" wingi kulingana na njeo ijayo, ilihali Wapaje wao hutumia Kiambishi "cho" kama kiambishi cha umoja cha o – rejeshi pamoja na njeo ijayo vile vile hutumia kiambishi "o" huwakilisha hali ya wingi.

#### ***Matokeo ya lengo mahususi la tatu na swali la tatu la utafiti***

Baada ya uchunguzi wa kina kufanyika kuhusu uwiano wa kimaana baina ya msamiati wa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kuna mambo kadhaa yamebainika;

Matokeo yanaonesha kuwa Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kuna msamiati unaowiana kimofolojia na kimaana baina ya jamii lugha hizo, vile vile imebainika kuwa baina ya jamii ya Paje na ile ya Makunduchi kuna msamiati unaotofautiana kimofolojia kupitia sauti moja tu lakini huwakilisha maana moja kwa

jamii zote mbili, pamoja na hayo matotokeo yamebainisha kuwa kati ya jamii ya Paje na ile ya Makunduchi kuna msamiati unaowiana kimaana lakini unatofautiana katika mofolojia yao kwavile kila jamii inatumia muundo wake katika kuuwakilisha msamiati huo kimamatamshi na hata kimaandishi na mwisho ni kwamba imebainika kuwa kati ya jamii ya Paje na ile ya Makunduchi kuwa kuna maumbo ya maneno ambayo hutamkwa na kuandikwa sawasawa baina ya jamii hizo lakini huwakilisha maana tofauti baina yao.

### **5.3 Hitimisho**

Kwa ujumla, utafiti huu umejaribu kutoa tathmini kuhusu uwiana wa kiisimu kati ya Kipaje na Kimakunduchi. Tumeona kuwa kuna tofauti nyingi zimejitokeza za kifonimu na matumi yake, michakato ya kifonolojia na mofolojia pamoja na za kimaana katika msamiati wa msingi ambazo pia kwa namna moja ama nyingine zinatofautiana na Kiswahili sanifu, hivyo kama wadau wa isimu kuna maswali mengi ya msingi ambayo tunapaswa kujiuliza.

Swali la kwanza la kujiuliza ni; kwa nini Kiswahili cha Kimakunduchi kinatofautiana kwa kiasi kikubwa na Kipaje na hata Kiswahili sanifu? Au katika Mkoa wa Kusini Unguja je kuna lahaja zaidi ya moja? Au kuna lahaja na vilahaja vyake?

Swali la pili la kujiuliza ni; ipi nafasi ya Kiswahili sanifu, katika kuondosha na kuziunganisha jamii lugha mbili hizo kimawasiliano?

Utafiti wa kina unahitajika na kwa vile tumeshapendekeza kuwa tafiti zaidi juu ya suala hili zinahitajika na kwa vile majibu ya maswali hayo yanahitaji utulivu,

umakini na uchunguzi wa kina zaidi. Matarajio yetu ni kwamba utafiti wa kina utabainisha tofauti nyingine zaidi na kupata ufumbuzi wa kina zaidi.

Zaidi kuhusu tofauti za kiisimu baina ya Kiswahili kinachozungumzwa Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na Kimakunduchi na vilahaja vyake. Kwa mantiki hiyo tunatarajia kuwa utafiti huu utakuwa ni chachu kwa watafiti wengine katika kuchunguza chimbuko na asili ya Kipaje na Kimakunduchi. Kwa kiasi Fulani matokeo ya uchunguzi huo yataisaidi jamii kuelewa asili na chimbuko la Kipaje na Kimakunduchi.

#### **5.4 Mapendelekozo kwa ajili ya tafiti zaidi**

Utafiti huu ulifanywa kwa kuoneshwa uwiano wa kiisimu baina ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi kusini Unguja. Vipengele vilivyo chunguzwa ni pamoja na fonimu, michakato ya kimofofonolojia pamoja na maana katika msamiati wa msingi, hivyo tunapendekeza tafiti nyingine linganishi zifanyike kwa baadhi ya vipengele vya fonolojia vipande kama vile silabi na mijengeko yake, fonolojia arudhi pamoja na kipengele cha sintaksia ambavyo hatujavishughulikia katika tafiti hii. Pili tumebaini kuwa Kimakunduchi kina vilahaja zaidi ya kimoja ndani yake hivyo tunapendekeza eneo hili ni vizuri kufanyiwa uchunguzi wa kiutafiti. Pia mtafiti anapendekeza uchunguzi zaidi unahitajika kuhusu asili ya watu na chimbuko la lahaja na vilahaja katika maeneo ya mkoa wa kusini Unguja. Vile vile mtafiti anapendekeza tafiti za kina zifanyike kuhusu nafasi ya Kiswahili sanifu katika kuziunganisha lahaja hizo mbili kimawasiliano.

### **MAREJELEO**

- Allen, J. (1993). *Swahili Origins, Swahili Culture and the Shungwaya Phenomenon.* London.
- Ash, S. na Boberg, C. (2006). *Southern Dialect.en* wikipedia.org/wiki/Southern American English.
- Ashton, E. O. (1971). *Swahili Grammar.* London: Burke's Peerage Ltd.
- Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Research.* London: Wadsworth Publishing Company.
- Bakar, K. B. (2015). “Ulinganishi wa Kiisimu kati ya Lahaja ya Kipemba na Kitumbatu.” (Tasnifu ya uzamili haijachapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Bakari, M. (1985). *The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects.* Dietrich Reimer Verlag. Berlin.
- Besha, R. M. (1989). *A Study of Tense and Aspect in Shambala.* Berlin: Dietrich Verlag.
- Chiragdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi. OUP.
- Cooley, L. na Lewkowic, J. (2004). *Dissertation writing in Practice* (2nd eds). Turning ideas into Text Hongkong University Press China.
- Cresswel, J. W. (2003). *Research Design* (2<sup>nd</sup>Eds). California: SAGE Publications.

- Cressswel, J. W. and Miller, D. L. (2000). *Determining Validity in Qualitative Inquiry*. California: SAGE Publications.
- Cressswel, J. (1998). *Qualitative Inquiry and Research Design choosing among Five Traditions*. California: Sage Publications.
- Enon, J. (1995). *Educational Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Uganda.
- Enon, J. (1998). *Reseach Methods in special Education and Field Study*. London: Sage Publications. Hichens, W. (1939). *Al -Inkishafi*. London: The Sheldon Press.
- Juma, H. K. H. (2011). “Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba.” (Tasnifu ya M.A Kiswahili haijachapishwa) Chuo kikuu Huria cha Tanzania.
- Juma, H. K. H. (2011). “Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba.” (Tasnifu ya M.A Kiswahili haijachapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Juma, M. A. (2006). “Msamiati na Vitenzi katika Lafudhi za Jambiani, Paje, na Bwejuu Katika Lahaja za Kimakunduchi.” Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.
- Juma, M.A. (2011). “Ulinganishi wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kizimkazi.” Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Karanja, P. & Habwe, J. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers. Ltd.

Kaseem, O. & Ekerete, J. (2013). *Nigerian Accents of English in the Context of World English*. Lagos: Published by Sciedu Press.

Kihore, Y. & wenzake (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kombo, D. K, and Tromp, D. I. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing Introduction*. Nairobi: Paulines Publicantions Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Reseach Methods*. New Delhi: New age Intenational Publishing Ltd.

Kothari, R.C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: New Age Publishers Limited.

Maganga, C. I. (1991). “A Study of Mophophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi.” Un Published PhD Thesis University of Dar es Salam.

Magesa, J. P (2017). “Ulinganishi Changanuzi wa Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili.” Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massammba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia*. Dar es Salaam. TATAKI.

Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Mwanza: Mwanza Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mgullu, R. S. (1999). *MTAALA WA ISIMU: Fonetiki, Fonolojia na Mofonolojia ya Kiswahili*. Nairobi: EALB.

Mohammed, S. S. (2013). “Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika Shulenii Makunduchi Zanzibar.” Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mosha, P. T. M. (2004). “Investigative Journalism and rruption Struggle challenges within Post Reform Print Mass Media in Tanzania”. A Deserition Submitted in Partial fulfillment of the Reguirement for the Degree of Master of Arts (Development Studies) of the University of Dar es Salaam.

Ohly, R. (1982). *Swahili the diagram of Crisis*. Beitrage zur Afrikanistik Band 15, Wien.

Onyango, V. O. (2017). *Daftari la Isimu kwa Wanafunzi wa Shule za Upili*. Ariba Book Publisher limited.

Polomé, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center for Applied Linguistics.

- Robson, C. (2007). *How to do a Research Project: A Guide for Undergraduate Students*. Carlton Victoria: Blackwell Publishing.
- Sacleux, Ch. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Paris: Institute D'ethnologie.
- Sengo, (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Researched Product.
- Sengo, T.Y. S. (2011). *Kiswahili na Uswahili ni Utambulisho wa Utamaduni na Utaifa*. Alhuda
- Sharman, F. (2014). *Linguistic Ties between Ancient Egyptians and Bantu, Universal*. Florida: Publisher Boca Raton.
- Sigh, K. (2007). *Qualitative Social Research Methods*. Indian: SAGE Publication. World Journal of English language (2013) Nigerian Accents of English in the context of World English. Online Published.
- Stigand, C. (1915). *A Grammar of Dialectical Changes in the Kiswahili Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Whiteley, W. (1969). *The Rise of a National Language*. London: Methuen.
- Wright, H. (1984). *Early Seafarers of the Comoro Islands*. The Dembeni Phase of the 1Xth- XV the Centuries AD, *Azania* 19: 13-59.
- Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds). Thousands Oaks Calif: SAGE publishers

## VIAMBATANISHO

### **KIAMBATANISHO NA . I**

#### **Muongozo wa Maswali ya Usaili.**

Maswali yafuatayo yatakuwa ni muongozo kwa mtafiti wakati wa usaili kwa watafitiwa wake. Data za Uwandani katika Kiswahili cha Paje na Kimakunduchi Kusini Unguja.

1. Tamka maneno yafuatayo kama yanavyotamkwa katika lugha yako.
 

i) Shurufu .....	ii) Suruali.....	iii) Korwa .....
iv) Saruji .....	v) Kupika .....	vi) Kupita .....
vii) Kupaka rangi.....	viii) Kula .....	ix) Lile .....
x) Lako.....	xi) Lenu .....	xii) Kufa .....
xiii) Kufana .....	xiv) Vaa .....	xv) Uvi .....
xvi) Vimewiva .....	xvii) Fatilia .....	xviii) Zote .....
xix) Nyote .....	xx) Vyote .....	xxi) Sote .....
xxii) Usilifu.....	xxiii) Rafiki .....	xxiv) Vurugu .....

2. Maneno yafuatayo yanaandikwaje? katika muktadha wa kimatumizi katika lugha ya Kiswahili unayoitumi.

- |                  |                  |                   |                  |
|------------------|------------------|-------------------|------------------|
| i) Jamvi .....   | ii) Anza.....    | iii) Chumvi.....  | iv) Mjenzi ..... |
| v)Ujenzi.....    | vi) Chenza.....  | vii) Nchi.....    | viii) Ncha.....  |
| ix) Mnyama.....  | x) Harusi.....   | xi) Karatasi..... | xii) Vuruga..... |
| Xiii)Saruji..... | xiv)Usilifu..... | xv)Rafiki.....    |                  |

xvi)Zimeenea.....	xvii)Zimeoza.....
xviii)Umeuza/umeiyuza...../.....	xix)Umeziona.....
xx)Zimeingia.....Xxi)Umelima.....Xxii)Umesoma.....	
.....Xxiii) Umeshaimba.....	
xxiv)Nimefika.....	Xxv)Nimekuja.....
xxvi)Nimeuza..... Xvii)Nimekwenda.....	
xxviii) Nimeondoka..... Xxix) Naondoka.....	
Xxx)Nimekula..... XXXi)Nimerudi.....	
xxxii Nimelime..... XXXiii) Nitaondoka.....	
xxxiv)Nitakupiga.....	xxxv)Uondoke.....
Xxxvi)Ufike.....	.xxxvii)Umelima.....
xxxviii)Umesoma.....	Xxxix)Umeshaimba.....
xxxx)uendeskuli.....	xxxxi)Uondoke.....
Xxxxii)mnaendawapi..... xxxxiii)mnaendacheza.....	
xxxxiv)mnaendazenu.....	
xxxxv)Amemaliza/Wamemaliza...../.....	
Xxxxvi)Analala/Wanalala...../.....	
xxxxvii)Anasema/Wanasema...../.....	
xxxxviii)Anatizama/Wanatizama...../.....	
Xxxxiv)Ameiba/Wameiba...../.....	
xxxxvii)Ameondoka/Wameondoka...../.....	
xxxxviii)Aliyekuja/Waliokuja...../.....	

Xxxxx)Aliyeondoka/Walioondoka...../.....  
 xxxx)Aliyesoma/Waliosoma...../.....  
 XXXXXi)Atakayesoma/Watakaosoma...../.....  
 xxxxii)Atakayekuja/Watakaokuja...../.....  
 xxxxiii)Atakayeondoka/Watakaoondoka...../.....

3. Toa maneno yanayotumika katika jamii yako katika miktadha ifuatayo na maana zake za kimatumizi.

a) Mavuvini

.....  
 .....  
 .....

b) Msibani

.....  
 .....  
 .....

c) Elimu

.....  
 .....  
 .....

d) Harusini

.....  
 .....  
 .....

e) Kilimo

.....  
.....  
.....

4. a) Je, kunanyimbo zozote ambazo huimbwa katika harakati za kimaisha katika jamii yako?

Ndio [ ]

Hapana [ ]

- b) Kama jawabu lako ni ndio. Toa mfano wa nyimbo zitumikazo katika miktadha ifuatayo.

- i. Bembezo za Watoto.
- .....  
.....  
.....

Nyimbo za harusi.

.....  
.....  
.....

Kilimo.

.....  
.....  
.....

Mavuvini.

.....  
.....  
.....

## **KIAMBATISHO NA. II**

### **Muongozo wa maswali ya Hojaji**

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti wa “ Uwiano wa kiisimu uliopo kati ya Kiswahili cha Paje na kile cha Makunduchi Kusini Unguja.

Tafadhalii unaombwa ujibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa mchango na matokeo yatakayosaidia kuleta mafanikio katika lugha ya Kiswahili.

Majibu yatakayopatikana yatatumika kwa ajili ya taaluma na yatakuwa siri baina ya mtafiti na watafitiwa.

#### **A) TAARIFA ZA MTAFITIWA.**

Weka alama ya vyema (✓) mahala panapo husika.

Umri .....

Jinsia      Mke [ ]      Mume [ ]

Kijiji unachoishi..... Mkoa.....

Wilaya ..... Kiwango cha elimu .....

Kazi.....

#### **B) MASWALI YA HOJAJI**

1. a) Je ni mzaliwa na mkaazi wa kijiji ulicho kitaja hapo juu?

Ndio [ ]

Hapana [ ]

b) Kama jawabu lako ni ndio. Andika hadithi ama historia fupi inayohusiana na kijiji chako pamoja na wakaazi wake.

.....  
.....  
.....

2. a) Je kuna sherehe zozote za kijadi au mila na desturi zifanyikazo katika Jamii yako?

Ndio [ ]

Hapana [ ]

- b) Kama jibu lako ni ndio. Elezea kwa kifupi sherehe moja wapo ihusuyo mila na desturi inayofanyika katika Jamii yako.
- .....  
.....  
.....

AHSANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO

**KIAMBATANISHO NA. III**

**ORODHA YA MSAMIATI UNAOTUMIKA KATIKA SHUGHULI MBALI  
MBALI KATIKA KISWAHILI CHA PAJE NA KILE CHA MAKUNDUCHI  
KUSINI UNGUJA**

1. SHUGHULI ZA HARUSI

<b>KISW</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>	<b>KMK</b>	<b>TAF</b>
Mahari				
Walii				
Biharusi				
Bwanaharusi				
Kungwi/ Nyakanga				
Talaka				
Eda ya talaka				
Fungate				
Vigelegele				
Chai ya lozi				
Karamu				
Asumini				
Vikuba				
Shanga				
Kisutu				
Sare				
Sanduku				
Bikra				
Akidi				
Mbanjo				
Busu				

Kipini				
Kidani				
Shedo				
Mekapu				
Kadi				
Kikuku				
Singo				
Idhini				
Posa				
Uradi				
Shemeji				
Mama mkwe				
Baba mkwe				
Mshenga				

## 2. SHUGHULI ZA MAZISHI/ MSIBANI

KISW	KPJ	TAF	KMK	TAF
Sanda/ Bafta				
Kuhani				
Tusi/ Jeneza				
Kukafini				
Maiti				
Karafuu maiti				
Jamvi				
Mwanandani				
Mbono				
Matanga				
Kizuka				
Marehemu				
Kaburi				
Pamba				

Yatima				
Urithi				
Khitma				
Khalili				

### 3. SHUGHULI ZA KILIMO NA UFUGAJI

<b>KISW</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>	<b>KMK</b>	<b>TAF</b>
Mbolea				
Mbegu				
Pembejeo				
Hekari				
Zizini				
Malishoni				
Shamba				

### 4. SHUGHULI ZA KIELIMU

<b>KISW</b>	<b>KPJ</b>	<b>TAF</b>	<b>KMK</b>	<b>TAF</b>
Peni/kalamu				
Daftari/buku				
Dawati/ deksi				
Mstari/rula				
Ada				
Chaki				
Bakora				
Kengele				
Liwali/kiongozi				
Kipindi				
Asembuli/mstarini				
Skuli/shule				
Muhutasari				
Kitabu cha kiada				

Kitabu cha ziada				
Mapumziko				
Darasa				
Likizo				
Kalamu ya risasi				
Sare				
Nembo				
Alama za maendeleo				
Kifutio ubao				
Ubao				
Muhula				
Kikokotoo				
Kifutio daftari/buku				
Mahudhurio				
Zamu za masomo				
Nukta				
Kituo kidogo				
Fungua, funga semi				
Imla				
Jaribio				
Uchelewaji				
Utoro				

### 5. SHUGHULI ZA KIIBADA

KISW	KPJ	TAF	KMK	TAF
Rakaa				
Dua				
Sunna				
Faradhi				
Jamaa				
Imamu				
Nia				

### 6. SHUGHULI ZA KIUTAMADUNI NA KIJAMII

KISW	KPJ	TAF	KMK	TAF
Makopa				
Gauni				
Jadi				
Familia				
Ukoo				
Ami				
Haloo				
Vika				
Pika				

### 7. SHUGHULI ZA KIUVUVI

KISW	KPJ	TAF	KMK	TAF
Mashua				
Boti				
Karabu				
Boya				
Jarife				
Mshipi				

Ngalawa				
Mtumbwi				
Nyavu				
Umangu				
Ndoana				
Msao/mlezi				
Chambo				
Nahodha				
Baharia				
Matlai				
Mwanashanga				
Mmande				
Kusi				
Kaskazi				
Kongwa				
Shuwari				
Wando				
Mtando				
Raba				
Kasia				
Pondo				
Rumada				
Kana				
Fashini				
Staa/ staha				
Kalafati				
Kudeheni				
Kukisi				
Nanga				
Mlingoti				

Foromali				
Destuli				
Tanga				
Joshi				
Demani				
Hamlawi				
Sharuti				
Amara				
Kiwindu				
Mchoro				
Teku				
Ngisi nyamvi				
Ngisi koroma				
Mkizi				
Mkure				
Mkonge				
Taa				
Mkunga				
Papa				
Hongwe				
Nguru				
Chewa				
Mzia				
Bombwa				
Bamvua				
Dago				
Korija				
Kufriji				
Kicho				

## 8. SHUGHULI ZA KISIASA

KISW	KPJ	TAF	KMK	TAF
Vita				
Jimbo				
Ukereketwa				
Kiongozi				
Kampeni				
Uchaguzi				
Sera				

**AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATANISHO NA IV**



*Mtafiti akihojiana na Bi Mtumwa Anta Makunduchi Kishunga Mbuzi (Tarehe  
12/10/2018 Saa 6:21 Mchana)*

**KIAMBATANISHO NA V**

*Mtafiti akihojiana na Bw. Saleh Kassim Sose kuhusu msamiati wa mavuvini akiwa  
katika Bandari ya Kigaeni Makunduchi (Tarehe 12/10/2018 Saa 7:28 Mchana)*

**KIAMBATANISHO NA VI**



*Mtafiti akiwa na watafitiwa wake baada ya mahojiano Kijijini Paje (Tarehe*

*13/10/2018 Saa 5:30 Asubuhi)*

## KIAMBATANISHO NA VII



*Mtafiti akishuhudia mazungumzo ya watoa taarifa katika maskani ya Kishunga*

*Mbuzi Makunduchi (Tarehe 12/10/2018 Saa 7:56 Mchana)*

**KIAMBATANISHO NAVIII**

*Mtafiti akihojiana na watoa taarifa kuhusu msamiati utumikao harusini Nganani*

*Makunduchi (Tarehe 12/10/2018 Saa 9:28 Jioni)*